# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

### Kikao cha Tano – Tarehe 8 Aprili, 2024

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

### MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa maswali, tunaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mheshimiwa Dkt. Ritta.

*(Hapa Mheshimiwa Mbunge hakusimama kuuliza swali lake)*

**NAIBU SPIKA:** Dkt. husikii?

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, sikusikia.

Na. 52

**Ujenzi wa Barabara ya Mtandika hadi Nyanzwa – Kilolo**

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI** aliuliza:-

Je, lini Barabara ya Mtandika hadi Nyanzwa - Kilolo itajengwa kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wakala ya Barabara za Vijijini na Mijini *(TARURA)* Mwaka wa Fedha 2023/2024 imetenga kiasi cha shilingi milioni 61 kwa kazi za kuchonga barabara kilomita tano na kuweka changarawe kwenye sehemu korofi katika barabara hii. Pia, kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 imeweka katika mipango kiasi cha shilingi milioni 150 kwa ajili ya kuchonga barabara kilomita saba na kuweka changarawe sehemu korofi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia *TARURA* imepanga kufanya usanifu wa kina wa barabara hii katika bajeti ya Mwaka wa Fedha 2025/2026 ili kujua kiasi cha fedha kitakachohitajika na kisha kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake. Naomba Barabara hii iweze kupitika kwa sababu hali yake ni mbaya sana. Sasa naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; Barabara ya Ilula – Image - Ibumu ni ahadi ya Serikali ya muda mrefu sana, lakini kwa

sasa hivi hali yake ni mbaya sana, haipitiki na wananchi wamekuwa wakipata shida sana. Je, lini Serikali itatimiza ahadi yake? Kwa sababu hii barabara ikijengwa ni pamoja na kumuenzi *Eng.* Patrick Mfugale ambaye anaishi katika hilo eneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; Barabara ya Kitowo – Kihesa - Mgagao – Mwatasi - Masisiwe ambayo inakwenda mpaka Idete ni barabara ya kiuchumi, lakini ina hali mbaya sana na haipitiki. Je, Serikali iko tayari angalau kujenga zile sehemu korofi tu ili iweze kupitika wakati huu kwa sababu mabasi hayapiti? Wananchi wanapata shida sana hata wanaokwenda kujifungua, wagonjwa na wazee. Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kuja katika Mkoa wetu wa Iringa ajionee hali mbaya ya barabara jinsi ili aweze kusaidia wananchi, nao waweze kufaidika na Serikali yao na uchumi uweze kujengeka?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge anafanya kazi kubwa sana ya kuwatetea wananchi wake. Mara kwa mara tumekuwa tukiwasiliana akinieleza changamoto za miundombinu katika eneo lake la uwakilishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu swali lake la kwanza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Ilula – Image – Ibumu tayari imeanza kujengwa baada ya kupokea fedha jumla ya shilingi milioni 150 za dharura. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba fedha hizi tayari zimeshatolewa na ujenzi wa barabara hii umeshaanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la pili, napenda kumjibu Mheshimiwa Mbunge kwamba Barabara hii ya Kitowo – Masisiwe – Mwatasi imetengewa bajeti ya shilingi milioni 36.8 katika

Mwaka wa Bajeti 2023/2024 kwa ajili ya kuchonga kilomita nane za barabara na kuweka kifusi kwa kilomita mbili kwenye maeneo korofi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali inatambua umuhimu wa barabara hizi kwa Uchumi, lakini pia kwa ustawi wa wananchi na inafanyia kazi kwa kadri fedha inavyopatikana kwa kufanya marekebisho na kujenga katika maeneo ya barabara ambazo zina changamoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba, nikitoka hapa nikikaa kwenye kiti changu tutazungumza ili tupange ratiba nzuri ya mimi kufika katika eneo lake ili kuona changamoto za wananchi na kuzitafutia suluhu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Mtaturu kwa niaba ya Mheshimiwa Martha Gwau.

Na. 53

**Kujenga Madaraja Barabara za Singida**

**MHE. MARTHA N. GWAU K.n.y. MHE. MIRAJI J. MTATURU** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga madaraja kwenye Barabara za Misughaa hadi Kikio na Matongo hadi Mpetu – Singida?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa vivuko na madaraja katika Jimbo la Singida Mashariki. Katika mwaka wa fedha 2023/2024, jumla ya shilingi milioni 435 zimetumika katika ujenzi wa madaraja katika Barabara ya Mpetu – Matongo - Misughaa – Msule - Sambaru, Mungaa – Ntuntu - Mang'onyi na Lighwa – Ujaire. Utekelezaji wake umefikia asilimia 90. Serikali kupitia

Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini imeweka katika mpango wake kwa mwaka wa fedha 2024/2025, jumla ya shilingi bilioni 1.11 kwa ajili ujenzi wa madaraja katika Wilaya ya Ikungi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Barabara za Misughaa - Kikio na Matongo - Mpetu kuna uhitaji wa jumla ya madaraja matatu ambayo ni Daraja la Mto Matongo lenye urefu wa mita 65, Daraja la Mto Isanja lenye urefu wa mita 45 na Daraja la Mto Siuyu lenye urefu wa mita 30. Kutokana na ukubwa wa madaraja haya usanifu wa kina unahitajika kufanywa. *TARURA* imeanza kutekeleza kazi ya usanifu wa madaraja haya kwa lengo la kupata gharama halisi za ujenzi wake.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Martha.

**MHE. MARTHA N. GWAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa Bajeti ya *TARURA* katika Wilaya ya Ikungi ni ndogo na kwa kuwa muunganiko wa eneo na eneo umekuwa ni changamoto kwa haya madaraja. Je, ni upi mpango wa Serikali katika kujenga madaraja haya ili kuunganisha vijiji, kata pamoja na wilaya?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Mheshimiwa Mtaturu kashawasilisha bajeti ya Madaraja matano ambayo ni Matongo – Mpetu, Misughaa – Ntutu, Misughaa – Kikio, Kimbwi na Lighwa na kwa umuhimu wake na udharura wake na kwa sababu bajeti tayari ipo mezani, tunataka kujua, je, ni lini Serikali itafanya uharaka wa kujenga hayo madaraja ili kuunganisha vijiji na kata hizi? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Tumekuwa tukiwasiliana na Mheshimiwa Mtaturu mara kwa mara akinieleza changamoto hizi za miundombinu kwenye jimbo lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nijibu swali lake la kwanza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina mpango wa kuhakikisha kwamba inajenga na inaboresha miundombinu katika maeneo yote nchi nzima. Barabara hizi za wilaya zina jumla ya urefu wa kilometa 144,429 na ni mtandao mkubwa ambao unahitaji bajeti kubwa. Mpaka muda huu tayari Mheshimiwa Rais amehakikisha Bajeti ya *TARURA* inaongezeka kutoka bajeti ya awali ambayo ilikuwa ni shilingi bilioni 275 mpaka sasa tunavyoongea bajeti ya *TARURA* ni shilingi bilioni 710.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, pale inapotokea dharura, Serikali inapeleka fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba mawasiliano hayakatiki kwa wananchi, kwa maana ya barabara hizi zenye umuhimu na ambazo zinahitajika kujengwa ili ziunganishe kijiji na kijiji na kata na kata. Nimhakikishie pia Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali itafanyia kazi ujenzi wa madaraja na miundombinu yote ambayo ni muhimu kwa ajili ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la pili Mheshimiwa Mbunge ameuliza kuhusu madaraja matatu. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kama nilivyosema bajeti ya dharura imeongezwa kutoka shilingi bilioni 21.2 mpaka sasa imefika shilingi bilioni 52.6, yote hii ni kwa sababu Serikali inataka pale inapotokea dharura, basi inapeleka fedha kwa ajili kushughulikia udharura huo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ahsante sana, umejibu vizuri sana. Tunaendelea na Ofisi hiyo hiyo, Mheshimiwa Kimea.

*(Mheshimiwa Dkt. Alfred J. Kimea hakuwepo ndani ya Ukumbi wa Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kimea, hayupo, kwa niaba.

Na. 54

**Ukarabati Hospitali ya Magunga – Korogwe**

**MHE. RASHID A. SHANGAZI K.n.y. MHE. DKT. ALFRED J. KIMEA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itafanya ukarabati mkubwa wa Hospitali kongwe ya Magunga – Korogwe?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Korogwe ilianza kutoa huduma mwaka 1952 kama Kituo cha Afya na baadaye kupandishwa hadhi na kuwa hospitali. Aidha, Hospitali hii ni miongoni mwa hospitali 50 kongwe ambazo Serikali ilizifanyia tathmini kwa ajili ya ukarabati mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali imetoa shilingi bilioni 16.5 kwa ajili ya kufanya ukarabati wa hospitali kongwe 19. Aidha, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali imetenga shilingi bilioni 27.9 za ukarabati wa hospitali kongwe 31 zilizobaki ikiwemo Hospitali ya Magunga katika Halmashauri ya Mji wa Korogwe ambayo imetengewa shilingi milioni 900. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa majibu mazuri sana ya Serikali. Kwanza, tunashukuru kwa kuona umuhimu wa Hospitali hii ya Magunga. Kwa kweli ni hospitali ya kimkakati kwa sababu ipo katikati ya Mji wa Korogwe, lakini kwenye njia kubwa ya kwenda Arusha na kuja Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina swali moja la nyongeza, vipo vituo vya afya ambavyo ni vikongwe sana ambavyo vingine pia vilianza tangu wakati wa ukoloni kikiwemo Kituo cha Afya cha Mlalo ambacho na chenyewe kimechakaa sana kinahitaji ukarabati mkubwa. Je, ni lini Serikali sasa itakarabati kituo hiki? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Serikali hii ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imeweka kipaumbele katika kukarabati hospitali zote chakavu ili ziweze kuwa na hadhi ya Hospitali za Halmashauri na kutoa huduma bora kwa wananchi. Kwa hiyo, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, tayari tulishaainisha hospitali zote kongwe 50 kote nchini. Fedha zinaendelea kutafutwa kwa ajili ya kuzikarabati kwa awamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na Kituo cha Afya cha Mlalo ambacho ni chakavu, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, baada ya kumaliza ukarabati wa hospitali kongwe za halmashauri hizi 19 zilizobaki, tunakwenda kuanza kukarabati vituo vya afya vikongwe. Nimhakikishie Mheshimiwa Shangazi tutakipa kipaumbele Kituo cha Afya cha Mlalo ili kiweze kukarabatiwa na kiweze kutoa huduma bora kwa wananchi. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kisangi.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza. Je, Serikali ina mpango gani wa kuiongeza na kuipandisha hadhi Zahanati ya Ununio ambayo itawasaidia sana wananchi wa Tegeta, Boko, Ununio, Mtongani na Kunduchi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikipandisha hadhi baadhi ya zahanati kuwa kituo cha afya. Moja ya vigezo ambavyo vinatumika ni ukubwa wa eneo ambapo zahanati ipo, kama linatosha kujenga miundombinu ya kituo cha afya, pia idadi ya wananchi wanaohudumiwa katika eneo hilo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutakwenda kulifanyia kazi suala la Zahanati ya Ununio.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina uhakika sana na ukubwa wa eneo lake kwa sababu napafahamu. Kama eneo litakuwa linatosheleza lakini pia kama litakidhi vigezo vingine basi Serikali italifanyia kazi ili kuweza kuipandisha hadhi na kama haikidhi tutaona namna nzuri zaidi ya kuhakikisha kwamba wananchi wanapata huduma bora za afya. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bupe.

*(Hapa Mheshimiwa Mbunge hakusimama kuuliza swali la nyongeza)*

**NAIBU SPIKA:** Hivi jamani huwa hamnisikii huko?

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuja Mkoani Rukwa aliahidi kujenga kituo cha afya katika Kata ya Kasanga. Je, ni lini ujenzi huo utaanza? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahadi za viongozi wetu wa Kitaifa zinapewa kipaumbele katika mipango ya utekelezaji. Naomba nimhakikishie Mbunge kwamba, hii ni ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ahadi zote za Viongozi wa Kitaifa tumezipa kipaumbele, tumeshaziorodhesha, tunatafuta fedha kwa ajili ya kwenda kujenga vituo hivyo. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie kwamba, tutahakikisha

fedha inapatikana mapema iwezekanavyo na Kituo cha Afya cha Kasanga kinajengwa kwa ajili ya huduma za wananchi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hassan.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, Kituo cha Afya cha Tarafa ya Matemanga kina wodi moja tu ya kujifungulia akinamama, hakuna wodi ya watoto, ya akinamama na ya akinababa. Je, ni lini Serikali itatoa fedha ya kujenga wodi hizo? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Afya cha Tarafa ya Matemanga kama ambavyo baadhi ya vituo vya afya kote nchini havina miundombinu ya kutosha na hasa wodi za watoto na wodi za wanaume.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Ofisi ya Rais, TAMISEMI imeshafanya makadirio ya fedha zinazohitajika kwa ajili ya kukamilisha miundombinu inayopungua kwenye vituo vya afya. Hiki Kituo cha Afya cha Matemanga ni miongoni mwa vituo ambavyo vimeshawekewa mpango huo. Kwa hiyo, tutaendelea kutafuta fedha ili tukajenge majengo hayo ili wananchi waweze kupata huduma hizo. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Ighondo.

Na. 55

**Ununuzi Majenereta – Hospitali ya Ilongero**

**MHE. ABEID R. IGHONDO** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kununua Jenereta katika Hospitali ya Ilongero na Vituo vya Afya Mgori, Makuro na Msange - Jimbo la Singida Kaskazini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Singida Ilongero pamoja na Kituo cha Afya Msange vimeshapokea jenereta kutoka Bohari Kuu ya Dawa *(MSD)* na taratibu za ufungaji zinaendelea. Kituo cha Afya Mgori kitapokea mgao wa jenereta katika Mwaka wa Fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Serikali kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri ya Singida itatenga bajeti kwa ajili ya ununuzi wa jenereta la Kituo cha Afya Makuro.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ighondo.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali madogo mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; nakiri kwamba tumepokea *standby generators* katika Hospitali ya Wilaya na Kituo cha Afya Mgori. Majenereta haya bado hayajaanza kutumika kwa kipindi kirefu sasa kutokana na kukosekana vile vibanda vya kuweka *standby generators.* Je, ni lini Serikali itaweza kujenga hivyo vibanda ili haya majenereta yaweze kutumika na kule kwenye Vituo vya Afya vya Mgori na Makuro ambavyo havina?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Hospitali ya Wilaya pamoja na vituo vya afya vyote vilivyopo katika Jimbo la Singida Kaskazini havina vyumba vya kuhifadhia maiti. Je, ni lini Serikali itajenga *mortuary* ili kuepusha usumbufu unaotokea pindi inapotokea dharura?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba kutumia nafasi hii kumwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Singida kwamba, Mheshimiwa Rais ameshapeleka fedha, majenereta yamenunuliwa kwa ajili ya hospitali ya wilaya na vituo vya afya. Kazi yake ni kujenga kibanda kwa ajili ya kuweka jenereta, ili wananchi waanze kupata huduma. Kwa hiyo, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, namwelekeza kwamba ndani ya siku 45, mwezi mmoja na nusu, ahakikishe amekamilisha ujenzi wa vibanda hivyo na majenereta hayo yafungwe yaanze kutoa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kuhusu majengo ya kuhifadhia maiti. Serikali inaendelea kutafuta fedha na kujenga miundombinu hiyo katika vituo vyetu kwa awamu. Pia, tunaendelea kusisitiza kwamba, mapato ya ndani ya halmashauri yatumike kwa ajili ya kujenga baadhi ya miradi ikiwemo majengo haya muhimu katika jamii zetu ya kuhifadhia maiti. Kwa hiyo, halmashauri ianze kufanya tathmini hiyo, lakini kama uwezo hautaruhusu, basi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa itaunga mkono juhudi ambazo watakuwa wameanza utekelezaji wake. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Mheshimiwa Zahor aulize swali lake.

Na. 56

**Elimu ya Mabadiliko ya Tabianchi**

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI** aliuliza:-

Je, kwa nini Serikali haielimishi wananchi kujiepusha na madhara yatokanayo na athari za mabadiliko ya tabianchi hadi pale maafa yanapotokea?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji, Mbunge wa Mwera, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kwa kuelimisha wananchi kuhusu madhara yanayotokana na mabadiliko ya tabianchi ili waweze kujilinda na maafa yanayosababishwa na mabadiliko ya tabianchi. Baadhi ya hatua hizo ni pamoja na kutoa elimu kupitia njia mbalimbali hasa vyombo vya habari na mitandao ya kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu inayotolewa inalenga kukuza uelewa kwa makundi mbalimbali katika jamii hasa makundi ya wakulima, wafugaji na wavuvi kuhusu mbinu bora za kilimo, ufugaji na uvuvi endelevu zinazoweza kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi, lakini pia kujilinda na maafa yanayoweza kutokea kwa jamii. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zahor.

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; pamoja na kwamba Serikali imeendelea kutoa taaluma au elimu kwa wananchi mbalimbali kwa vyombo mbalimbali, je, Serikali imefanya tathmini kujua ni kiasi gani elimu hiyo inawafikia na inawasaidia wnanchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa sababu, Jimbo la Mwera ni jimbo la vijijini na athari kubwa inatokea kwenye mambo haya ya mazingira ambayo Mheshimiwa Waziri anasema wanatoa elimu. Je, ni lini sasa Mheshimiwa Waziri, *physically,* pamoja na

wataalam wake wanaweza kwenda kusaidia kutoa elimu wao wenyewe? Nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la kaka yangu, Mheshimiwa Zahor, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba kuweka *record* sawa; kaka yangu, Mheshimiwa Zahor, ni mzoefu sana, wakati anamsaidia Makamu wa Rais wakati ule alifanya kazi kubwa sana. Kwa hiyo, naomba kumpa maua yake kwa kazi kubwa aliyoifanya katika upande wa muungano na upande wa mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa tathmini, hivi karibuni tutatoa taarifa yetu ya mazingira ambapo, naamini utakapofika Mwezi Juni tutakuwa tumepata taarifa ambayo iko *very comprehensive*. Nina imani kwamba, baada ya taarifa hii tutaona tathmini ya hali ilivyo kwa maeneo hayo yote. Kwa hiyo, tusubiri mpaka Mwezi wa Sita, Siku ya *World Environment Day,* taarifa hii itatoka kwa lengo la kujua tathmini ya athari za mabadiliko ya tabianchi na athari za kimazingira kwa maeneo mbalimbali iko vipi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala zima la kutoa elimu; naomba nilichukue hili kwa sababu, nina dhamana ya Muungano. Mheshimiwa Mbunge atakumbuka huwa naenda katika majimbo yao kutembelea miradi ya Mfuko wa Jimbo na mambo mengine. Hili tunalichukua, tutaona namna bora zaidi kwa kushirikiana na wenzetu wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza, kule Zanzibar, kuona jinsi tutakavyofanya ili kuwafikia wananchi wa Mwera kwa ajili ya upatikanaji wa elimu. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Chaya, jiandae Mheshimiwa Asenga.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Katika Kata ya Sanza iliyoko Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni kuna Mto Sanza ambao mabadiliko ya tabianchi yamesababisha mto huo kuchepuka na kuathiri makazi na Kanisa la *Roman Catholic*. Je, ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba, madhara haya yanakabiliwa? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mbunge wa Manyoni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli, kwanza namshukuru Mheshimiwa Mbunge alikuja kunijulisha taarifa hii. Binafsi nasema kwamba, tunakiri tatizo hilo lipo, lakini kubwa zaidi sasa hivi tunaainisha maeneo yenye tatizo hilo kwa sababu yako mengi sana, tuna kule Manyoni, tuna Mpwapwa, tuna Mvomero, maeneo haya yamekithiri zaidi. Kwa hiyo, tutaangalia jinsi gani ya kufanya ili kushughulikia eneo hilo, lakini najua kweli ni tatizo kubwa, linaathiri hata lile jengo la kanisa, nalo liko hatarini  Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asenga.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. Hongera sana kwa Mheshimiwa Waziri, anafanya kazi kubwa ya kutunza mazingira ya nchi yetu. Sasa athari zimetokea na katika baadhi ya maeneo wananchi wamekumbwa na mafuriko makubwa ikiwemo Jimbo la Kilombero, Halmashauri ya Mji wa Ifakara. Hivi ninavyozungumza wananchi takriban 300 wako kambini katika shule. Je, Serikali na Ofisi ya Waziri kwa kushirikana wananisaidiaje kupata chakula cha dharura kwa wananchi wangu wa Jimbo la Kilombero?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la *Comrade*, Mheshimiwa Asenga, Mbunge wa Ifakara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuna maeneo sasa hivi yana athari kubwa sana, kuna eneo la Ifakara, Rufiji na maeneo mbalimbali. Kwa kweli, athari ya mafuriko imekuwa ni kubwa sana. Juzi nilikuwa naongea na moja ya balozi kwa ajili ya kuona jinsi wanavyoweza kusaidia na wameanza kutoa timu kupeleka katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu jambo hili ni jambo la kiutu zaidi, nawaomba wadau mbalimbali hasa wa kimaendeleo wabaini kwamba, watu sasa hivi wanaathirika, wawafikie ili kuwapa msaada kwa sababu kweli limekuwa ni tatizo kubwa na maeneo mbalimbali yanaathirika. Hoja ya Mheshimiwa Mbunge imechukuliwa na Serikali itaitafakari kwa upana zaidi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mchungahela.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Vikundi vingi vya mazingira vimekuwa vikikosa motisha na uwezo. Je, Serikali inachukua hatua zipi kuvijengea uwezo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la *Comrade,* Mheshimiwa Mchungahela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli, kuna vikundi vingi ambavyo vimejihamasisha zaidi kuhakikisha vinashughulika na shughuli za kimazingira, lakini wakati mwingine vinakuwa na changamoto ya bajeti. Nachukua fursa hii kuomba Mamlaka za Serikali za Mitaa, kupitia dirisha la utoaji wa fedha kwa ajili ya vikundi, ziangalie kama kuna vikundi vya kimazingira ambavyo vinaweza kupatiwa mtaji wa

uzalishaji wa miti waweze kufanya hivyo, kwa ajili ya kuvisaidia vikundi vyetu mbalimbali kuwa na nguvu na uwezo kwa ajili ya kushughulikia masuala ya kimazingira.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Twaha Mpembenwe. Mheshimiwa Twaha hayupo, kwa niaba.

**MHE. SUBIRA K. MGALU K.n.y. MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ngoja basi Mheshimiwa Subira. Mheshimiwa Subira.

Na. 57

**Huduma za Wakala wa Forodha Bandari ya Nyamisati**

**MHE. SUBIRA K. MGALU K.n.y. MHE. TWAHA A. MPEMBENWE** aliuliza:-

Je, ni upi mkakati wa Serikali wa kuweka huduma za Wakala wa Forodha katika Bandari ya Nyamisati?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Twaha Ally Mpembene, Mbunge wa Kibiti, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, maandalizi ya kutoa Huduma za Wakala wa Forodha katika Bandari ya Nyamisati yanaendelea ambapo Novemba, 2023, Mamlaka ya Mapato Tanzania ilifanya tathmini kujiridhisha na mawanda ya shughuli zinazofanyika katika eneo hilo. Matokeo ya tathmini hiyo yanaonesha kuwa, eneo hilo

lina uhitaji wa huduma za forodha. Hivyo, Serikali inatarajia kufungua ofisi za forodha katika Bandari ya Nyamisati mwaka 2024/2025. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mgalu.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza nampa pole Mheshimiwa Mbunge Twaha na wananchi wa Kibiti kwa mafuriko makubwa yanayoendelea kule, lakini pamoja na hayo, nina maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; kwa kuwa, jibu la msingi limeonyesha utayari wa Serikali kufungua Ofisi ya Forodha katika Bandari ya Nyamisati; na kwa kuwa, Bandari ya Nyamisati imeonesha ofisi katika Mamlaka ya Mapato *(TRA)*. Naomba kujua, je, Serikali ipo tayari mpaka Desemba, 2024 ofisi hiyo iwe imefunguliwa kwa umuhimu wake wa kuongeza mapato? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa, wafanyabiashara wa vyombo vya mashua kutoka Zanzibar wapo tayari kusafirisha bidhaa kwa kutumia Bandari ya Nyamisati kwa sababu ina miundombinu iliyo kamili. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yupo tayari kushirikiana na Mbunge Twaha pamoja na mimi Mbunge wa Mkoa kukutana na wafanyabiashara hao ili kuzungumza na kuwatia moyo katika maandalizi ya kutumia Bandari ya Nyamisati? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Subira, Balozi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iko tayari na ndiyo maana katika jibu la msingi tumesema Mwaka huu wa Fedha 2024/2025

forodha hiyo itafunguliwa. Kwa hiyo, Serikali iko tayari haitafika Disemba tutakuwa tumeanza zoezi hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili, Naibu Waziri yuko tayari kuambatana na Mheshimiwa Mbunge Twaha na Mheshimiwa Balozi wetu Bi. Subira kwenda kukaa na wafanyabiashara hao. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Afya. Mheshimiwa Tarimo.

Na. 58

**Mpango wa Kuirejesha *TFDA***

**MHE. PRISCUS J. TARIMO** aliuliza:-

Je, upi mpango wa kurejesha *TFDA* kwani imeacha masuala ya chakula na inakinzana na utaratibu wa usimamizi wa chakula na madawa duniani?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, Mbunge wa Moshi Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali katika kuimarisha mazingira ya biashara nchini ilifanya maamuzi kupitia Bunge lako Tukufu ya kuhamisha majukumu ya usimamizi na udhibiti wa ubora wa chakula na vipodozi kutoka iliyokuwa *TFDA* na kuyapeleka *TBS* ambako ndiko afua zote za usimamizi zinatekelezwa huko kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kurejesha usimamizi huo kwa *TMDA* bado linaendelea kujadiliwa ndani ya Serikali na mara

litakapokamilika mapendekezo ya utekelezaji yatawasilishwa Bungeni. Naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tarimo.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa kuwa, tayari imeshaonesha kwamba, *TBS* imeshindwa kushughulikia masuala ya chakula na kwa kuwa, Kamati mbalimbali za Bunge, Kamati ya Afya imetoa mapendekezo masuala haya ya chakula yapelekwe *TMDA,* lakini Kamati nyingine zimesema irejeshwe *TFDA* na kwa kuwa, *practice* duniani ni *Food and Drugs Authority*, ni kwa nini mchakato huo usifanyike kwa haraka zaidi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Mbunge wa Moshi kwa sababu, kwa muda mrefu huko nyuma, Moshi haikuwahi kupata Mbunge mzuri kama huyu anayejua Wanamoshi wanataka nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa swali lake ambalo kimsingi ni swali moja la mwisho, ni kwamba, kwa sababu hili jambo limepitishwa na Bunge letu Tukufu na Bunge ni *organ* kubwa muhimu sana, tunaomba kwa sababu Serikali inaendelea na huo mchakato, tuendelee kufuata taratibu zote ambazo zilifuatwa huko nyuma, halafu hili jambo litakuja Bungeni kama maelekezo ya Kamati yalivyoelekeza kwa Serikalini kwanza kukubaliana na kuweka mambo sawa kabla ya kulileta Bungeni kabla halijaiva vizuri. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Ujenzi. Mheshimiwa Noah Saputu, Mheshimiwa Festo Sanga, kwa niaba yake uliza swali namba 59.

Na. 59

**Kuzuia Magari ya Serikali Sehemu za Starehe**

**MHE. FESTO R. SANGA K.n.y. MHE. NOAH L. SAPUTU** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itazuia kupaki magari ya Serikali sehemu za starehe baada ya saa za kazi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, napenda kujibu swali la Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Waraka wa Rais Na. 1 wa Mwaka 1998 kuhusu Hatua za Kubana Matumizi ya Serikali, ilielekezwa kuwa Magari yote ya Serikali yanatakiwa kuwa yameegeshwa sehemu zilizotengwa kwa ajili hiyo ifikapo saa 12.00 jioni bila kukosa. Vinginevyo, kiwepo kibali rasmi kinachoruhusu Gari la Serikali kuwepo barabarani baada ya saa 12.00 jioni.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, Serikali kupitia Kanuni Na. 21 ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za Mwaka 2009, imezuia Watumishi wa Umma kutumia Magari ya Serikali kwa matumizi binafsi. Hivyo, mtumishi anayekwenda kinyume na maelekezo hayo anatakiwa kuchukuliwa hatua kali za kinidhamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa fursa hii naomba kuwakumbusha Maafisa Masuuli wote kusimamia maelekezo hayo. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Festo.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza, kwanza naishukuru Serikali kwa maelekezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; licha ya kwamba, Sheria na Kanuni zimekuwa zikizuia, kama ambavyo Mheshimiwa Naibu Waziri amesema, bado kwenye mitaa, baa na maeneo mengine Magari ya Serikali yamekuwa yakionekana majira ya usiku. Je, ni upi mkakati wa makusudi wa Serikali kuhakikisha unazuia kabisa uwepo wa magari katika maeneo hayo kwa sababu imegeuka kuwa kero kwa wananchi na pia inaonesha kwamba, ni matumizi mabaya ya fedha ya Serkali?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Mheshimiwa Waziri wa Fedha wakati anasoma bajeti alisema, Serikali ina mpango wa kuanza kupunguza kununua magari Serikalini na watumishi wa Serikali waweze kujinunulia magari kupitia mikopo. Je, ni hatua gani zimefikiwa hadi sasa, ili kupunguza matumizi ya Serikali, kama ambavyo wametuambia? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Sanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu ya msingi kwamba, tunawakumbusha na kuwasisitiza Maafisa Masuuli na waajiri wote kwa kuwa, Sheria, Kanuni na Taratibu zipo, ambazo zimeelekeza mtumishi yeyote ambaye anayetumia chombo cha umma na hasa magari, asiwe barabarani baada ya saa 12:00 jioni na asiwe kwenye maeneo ambayo si sahihi kwa muda ambao hauruhusiwi. Kwa hiyo, nakumbusha kwamba, Sheria zipo, kwa hiyo wanaohusika wachukue hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili alilosema, nadhani wakati Mheshimiwa Waziri wa Fedha atakapokuwa anawasilisha

bajeti atalifafanua vizuri, kitu gani na wapi Serikali imefanya na inategemea kufanya. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tarimba.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuwa, Serikali imeliambia Bunge lako Tukufu kwamba, Sheria na Kanuni za kukataza matumizi ya magari baada ya muda wa kazi zipo. Je, Serikali iko tayari kutoa maelekezo au kauli kwa wanaosimamia usalama wa barabarani kuyakamata magari ambayo yanaendelea kukaidi amri hii?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema ni kwamba, Sheria zipo na kila chombo kimepewa majukumu yake, ni nini kinatakiwa kifanye, nani anatakiwa alione gari liko wapi kwa wakati gani na kama halina kibali cha kuwepo mahali hapo kwa wakati huo afanye nini. Hivyo, bado nasisitiza kwamba, Serikali inatakiwa ichukue hatua. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi. Kuna magari mengi sana mabovu, hasa yale ya miradi, kwenye halmashauri zetu na kwenye ofisi za Serikali. Je, ni nini mkakati wa Serikali kupunguza magari haya mabovu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka lilete kama swali la msingi.

Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Uchukuzi, Mheshimiwa Maimuna Pathan.

Na. 60

**Serikali Kulipa Fidia Wananchi wa Nachingwea**

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN** aliuliza:-

Je, ni lini wananchi wa Nachingwea ambao mashamba yao yalitwaliwa na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege watalipwa fidia?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maimuna Ahmad Pathan, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kushughulikia na kufuatilia kwa ukaribu suala la ulipaji wa fidia kwa wananchi wanaopisha upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Nachingwea. Hatua ya awali ya kutambua wafidiwa na mali zao imekamilika na kuidhinishwa na Mthamini Mkuu wa Serikali. Aidha, maombi hayo yamewasilishwa Serikalini kwa ajili ya malipo. Pia Serikali itahakikisha kuwa wananchi wote wanaopisha maeneo yao kwa ajili ya ujenzi na upanuzi wa miradi mbalimbali wanalipwa fidia zao stahiki.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Pathan.

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; je, Serikali kwa kuchelewa kulipa pesa ya wananchi zaidi ya miaka mitano sasa, haioni kwamba imerudisha nyuma maendeleo ya wananchi hao kwa kukosa sehemu za kulima? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, naomba kauli thabiti ya Serikali, je, ni lini wananchi hawa wa Nachingwea wataipata pesa yao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba tuna viwanja takribani 15 nchi nzima ambavyo tunafanya uhakiki na hatua mbalimbali za utwaaji wa ardhi ili kuweza kufanya maendelezo makubwa ya viwanja vya ndege. Hilo moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ningependa kujibu maswali yake kwa umoja wake. Tunafahamu umuhimu mkubwa wa Uwanja wa Ndege wa Nachingwea, siyo tu kwa ajili ya korosho, madini ambayo yamegundulika na *LNG,* lakini pia kwa ajili ya mazao kama ufuta na kadhalika. Hivyo basi, Serikali kwa maana ya kutoa kauli thabiti, inaliarifu Bunge lako Tukufu kwamba tunao mpango wa kujenga uwanja huu na ndiyo maana sasa tulifanya uhakiki kwa wale wananchi 116. Awali ilikuwa tuwalipe shilingi bilioni 3.5, lakini baada ya kufanya uhakiki na ongezeko la gharama ya mazao, tukapata ni shilingi bilioni 3.4 – 3.5. Hii yote ni dhamira ya Serikali katika kuona kwamba wananchi hao wanakamilishiwa mradi wao. Hivyo basi, tunaendelea na taratibu mbalimbali za Serikalini, tukikamilisha tutaweza kuanza ujenzi huo. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Manyinyi.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Uwanja wa Ndege wa Musoma, watu wanadai fidia sasa ni zaidi ya miaka mitatu ambayo ni fedha isiyopungua bilioni 3.9. Hakuna biashara inayoendelea kwa kuwa wanategemea wapate fidia ili waendelee na maisha yao. Je, ni lini sasa hawa watu watalipwa fidia ili waweze kuendelea kuondoka pale? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu madai mbalimbali ya Uwanja wa Ndege wa Musoma na hivi juzi Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuwa hapo na alitoa maelekezo kwa sisi wasaidizi wake Serikalini tukamilishe haraka iwezekanavyo. Tupo kwenye hatua mbalimbali hususan za mwisho kwa wenzetu Wizara ya Fedha. Mara watakapokamilisha tutakwenda kulipa mara moja, kwa sababu tunafahamu umuhimu wa Uwanja wa Ndege wa Musoma kwa maana ya madini pamoja na vitu mbalimbali ambavyo viko pale. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mafuwe.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naishukuru Serikali kwa kutupa shilingi bilioni 11 kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi wale waliokuwa Uwanja wa Ndege wa *KIA* ili waweze kuondoka. Hata hivyo, kumejitokeza changamoto ndogondogo, baadhi ya wananchi kufanyiwa tathmini ndogo tofauti na hali halisi na baadhi yao kusahaulika. Changamoto hiyo Mheshimiwa Makamu wa Rais aliiagiza Wizara ya Uchukuzi iifanyie kazi. Je, ni lini sasa Serikali itamaliza changamoto hii ikiwa ni pamoja na kurudia tathmini kwa wale ambao walifanyiwa tathmini ambayo siyo sahihi? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tulifanya uhakiki kwa baadhi ya waliolalamika kwamba walipunjwa malipo yao katika Uwanja wa *KIA,* lakini kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge ameleta hoja hiyo, tuko tayari kama kuna malalamiko mengine, kuyapitia upya ili waweze kupata stahiki zao. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Wananchi wa Wilaya ya Kyerwa na Karagwe ambao kwa muda mrefu waliambiwa wasiendeleze maeneo ambayo yako karibu na barabara ambazo ni Barabara kutokea Omugakorongo

kwenda mpaka Murongo zikiathiri Kata za Kibale, Bugara na maeneo mengine. Je, ni lini sasa fidia hizo zitatoka ili wapishe hayo maeneo ya uendelezaji wa barabara kwa sababu wameshindwa kuendelea na maendeleo au kufanya chochote kwa sababu ni *issue* ya muda mrefu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye maelezo wakati namjibu mwenye swali la msingi, tupo kwenye hatua mbalimbali za utwaaji wa ardhi, tuna viwanja 15 nchini kote. Pamoja na hoja aliyoisema Mheshimiwa Mbunge, tunaichukua tuifanyie tathmini na tutaona namna bora ya kuonana naye ili kuweza kuzifanyia kazi hoja za wananchi hao.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Je, ni lini wananchi ambao wanapisha upanuzi wa Uwanja wa Ndege Manyara watalipwa fidia? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, hebu rudia tena swali lako.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini wananchi wanaopisha upanuzi wa Uwanja wa Manyara watalipwa fidia?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa hatua tuliyopo ni uandaaji wa taarifa ya uthamini, mara tutakapokamilisha, tutawalipa fidia.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kuna fidia ambayo inadaiwa Kipunguni, walipisha Uwanja wa Ndege wa Dar es Salaam. Hawa wananchi wanalalamika sana na tulishawahi kwenda pale kwa

Waziri wa Fedha, lakini bado fidia yao haijalipwa. Je, ni lini sasa watalipwa?

Waziri wa Fedha. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa. Ni kweli kama ulivyosema kuna fidia inadaiwa na wananchi walishapewa mwongozo huo na Serikali na ni kweli nilishafika pale. Kitu kilichofanyika ni kwamba…

**NAIBU SPIKA:** Tulikwenda wote mimi, wewe na Mheshimiwa Mbunge Bonnah pale.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tulifika na Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Segerea, Mheshimiwa Bonnah amekuwa akifuatilia ofisini mara kwa mara kuhusu jambo hili. Kilichotokea ni kwamba ilikuja kugundulika kuna baadhi ya maeneo ambayo wananchi walikuwa wamepewa maeneo mbadala, yalikuwemo kwenye sehemu ya madai na kuna baadhi ambao walikuwa wamehitaji fidia zaidi. Kwa hiyo kilichofanyika, tulipeleka timu iweze kuwianisha, iweze ku-*align* zile *numbers* na jambo hilo lilishafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunachofanya, tunatafuta fedha ndani ya kipindi hiki cha mwaka wa fedha unaoendelea ili tuweze kuanza kufanya malipo. Tutaanza na wale ambao madai yao yamehakikiwa na hayana vikwazo vyovyote…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ahsante…

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kulifuatilia kwa karibu sana jambo hili na sisi Serikali tutafanya hilo kwa ajili ya kuienzi kazi yake. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana na nampongeza Mheshimiwa Mbunge Bonnah kwa kazi na Wabunge wote wanaofuatilia mambo ya fidia.

Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Kigua.

Na. 61

**Kukamilisha Mradi wa Maji Kata ya Mabalanga – Kilindi**

**MHE. OMARI M. KIGUA** aliuliza:-

Je, lini Mkandarasi anayejenga Mradi wa Maji Kata ya Mabaranga - Kilindi atakamilisha kazi hiyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, Mbunge wa Jimbo la Kilindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na utekelezaji wa Mradi wa Maji Mabalanga uliopo Wilaya ya Kilindi Mkoani Tanga. Mradi huo unahusisha ujenzi wa tanki lenye ujazo wa lita 135,000, ujenzi wa tanki la kukusanyia maji *(sump well)* lenye ujazo wa lita 25,000, ujenzi wa vituo 12 vya kuchotea maji, ulazaji wa mabomba yenye umbali wa kilometa 6.62, ujenzi wa nyumba ya mitambo *(pump house),* ujenzi wa ofisi *CBWSO*, ukarabati wa machujio ya maji, ujenzi wa miundombinu ya kuvuna maji ya mvua pamoja na ufungaji wa pampu.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa mradi huo umefikia wastani wa asilimia 85 na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2024 na kunufaisha wananchi wapatao 6,021 waishio katika Kijiji cha Mabalanga. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kigua.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kwanza kuipongeza Wizara ya Maji kwa kazi nzuri sana kwa sababu kata hii ilikuwa ina changamoto kubwa sana ya maji. Sasa, nina swali moja tu la nyongeza. Je, Serikali iko tayari baada ya kukamilisha mradi huu kuhakikisha kwamba wananchi ambao wako pembezoni na kata hii pia wanapata maji? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, samahani, sijalisikia vizuri swali lake.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa rudia tena.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimetoa pongezi kwa Serikali, kuhakikisha kwamba wanafanya vizuri katika mradi huu katika Kata ya Mabalanga. Swali langu la nyongeza ni kwamba, Serikali iko tayari baada ya kukamilisha mradi huu kwenye Kata ya Mabalanga kuhakikisha kwamba vitongoji ambavyo viko pembezoni mwa kata hii pia vinapata maji?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Omari Kigua, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Chama Cha Mapinduzi inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imetoa takribani shilingi bilioni 39 katika kufanya miradi 13 katika Jimbo la Kilindi. Katika jimbo hili, miradi tisa inafanywa kwa Mfumo wa Wakandarasi na miradi minne wanafanya kwa Mfumo wa *Force Account*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaamini kwamba miradi hii 13 itakapokamilika, vijiji 78 vinaenda kunufaika na wakazi takribani 239,810 watanufaika na mradi huo. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge pindi miradi hii itakapokamilika Serikali itaenda kuanza

kupanua wigo wa upatikanaji wa maji vitongojini kulingana na upatikanaji wa fedha. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kakoso, jiandae Mheshimiwa Issaay.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji wa Kata ya Mishamo una zaidi ya miaka miwili haujakamilika. Je, ni lini mradi huo utaweza kukamilika katika kipindi hiki? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kakoso. kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhamira ya Serikali ya Chama Cha Mapinduzi kuhakikisha kwamba miradi yote ya maji inakamilika. Pia tunaendelea kuhakikisha kwamba tunakuwa na mawasiliano ya karibu sana na wenzetu wa Wizara ya Fedha ili kuhakikisha kwamba, wakandarasi ambao watakuwa wamewasilisha hati za madai, walipwe na kuendelea na miradi mingine ili Watanzania wapate huduma ya maji bila…

Mheshimiwa Naibu Spika, lini utakamilika? Itategemea sasa na namna gani wakandarasi wameji-*align* kuhakikisha kwamba wanakamilisha miradi yao na kuweza kuwasilisha kazi za baadaye…

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Issaay, jiandae Mheshimiwa Bushiri.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Tunaishukuru Serikali kwa kuchimba visima nane katika Jimbo la Mbulu Mjini na hadi sasa hakuna kisima kilicho tayari kwa ajili ya kujengewa miundombinu. Je, ni lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya kujenga miundombinu ya visima vyote nane katika Jimbo la Mbulu Mjini? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mbunge wa Mbulu Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iko kwenye mkakati wa kuhakikisha kwamba miundombinu ya maji inajengwa ili huduma ya maji iweze kutolewa. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge katika bajeti yetu ya mwaka huu, tutahakikisha tunazingatia hayo mahitaji ili wananchi wa Mbulu waweze kupata huduma ya maji safi na salama. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bushiri, jiandae Mheshimiwa Mnzava.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Je, ni lini Serikali itakamilisha Mradi wa Maji katika Kata ya Kimochi, Moshi Vijijini? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, jibu kwa kifupi sana. Muda wetu unakwenda.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nipokee changamoto hii kwanza nikaielewe kwa kina ili tuweze kuifanyia kazi kulingana na uhitaji wake. Nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mnzava, jiandae Mheshimiwa Massare.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni lini Serikali itakamilisha Mradi wa Maji wa Mwanga – Same – Korogwe ili kuzisaidia Kata za Mkomazi na Mkumbara ambazo ziko mwishoni mwa mradi huo? Nakushukuru *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ni lini?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mnzava, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi Mheshimiwa Waziri Jumaa Aweso alikuwepo Kilimanjaro na alikuwa kule kwa ajili ya kuhakikisha kwamba miradi ya maji iliyoko katika Mkoa wa Kilimanjaro pamoja na Tanga inakamilika kwa wakati. Nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwa niaba ya wananchi wake, miradi hii itakamilika ndani ya mwaka huu wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, miradi itakamilika. Mheshimiwa Massare.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, gari lililonunuliwa na Serikali na Mheshimiwa Rais kwa ajili ya kuchimba maji katika mikoa yote ikiwemo Mkoa wa Singida, magari hata hayatulii sehemu moja na usimamizi wake umekuwa haueleweki. Je, Serikali imejipangaje ili miradi ya maji katika vijiji na katika maeneo yetu iweze kufanyika vizuri?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Massare, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan Suluhu Hassan aliagiza magari ya kuchimbia visima na hii ilikuwa ni fursa kubwa sana kwa Watanzania. Kwa hiyo nitumie fursa hii kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, kuwaelekeza ma-*RM* wote nchini kuhakikisha kwamba haya magari hayakupelekwa kwa ajili ya kwenda ku-*park*, yamepelekwa kwa ajili ya kwenda kufanya kazi ili Watanzania wapate maji na nitafuatilia ili kuona utekelezaji unaendaje. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kasaka, jiandae Mheshimiwa Suma.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji wa Matwiga, awamu ya pili ambao ulianza toka 2012 unaenda kwa kusuasua sana. Je, ni lini Serikali itatoa fedha za kutosha ili Vijiji vya Mazimbo, Mtanila, Ifuma na Lupa viweze kupata maji haya? Nashukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Masache Kasaka, Mbunge wa Lupa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa mradi huu ulianza mwaka 2012, lakini unaenda kwa awamu. Awamu ya kwanza unahusisha vijiji viwili vya Matwiga pamoja na Isagawana na awamu hiyo ishakamilika tayari, wananchi wanapata maji. Awamu ya pili ambayo inahusisha vijiji sita, upo katika asilimia 90. Kwa hiyo namwomba Mheshimiwa Mbunge aendelee kuwa na subira, mradi huu utakamilika mwaka huu wa fedha na wananchi watapata maji.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Suma.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni lini ujenzi wa Tanki la Maji la Tukuyu Mjini Wilayani Rungwe utakamilika ukizingatia tanki lile ni la muhimu sana linahudumu Kata ya Bulyaga, Makandana, Bagamoyo, Tukuyu Mjini, Kawetele na Ibighi? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu ni mkubwa na ni wa muhimu sana kwa Watanzania. Nimwombe Mheshimiwa Mbunge

anipe nafasi, nikaufanyie kazi, lakini pia nitampa mrejesho kwamba mradi huu upo katika hatua gani na wapi umekwama na chanzo ni nini ili tuweze kuufanyia kazi kuhakikisha kwamba Watanzania wanapata maji. Nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Subira Mgalu.

Na. 62

**Mradi wa *Building a Better Tomorrow* Bonde la Mto Rufiji**

**MHE. SUBIRA K. MGALU** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha Mradi wa *Building a Better Tomorrow* katika Bonde la Mto Rufiji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Machi, 2024, jumla ya ekari 340,245.3 zimebainishwa na kupimwa afya ya udongo kwa ajili ya Programu ya *BBT* katika Mikoa ya Dodoma, Kigoma, Mbeya, Singida, Tanga, Njombe na Kagera. Kwa sasa maandalizi ya mashamba yameanza katika Mkoa wa Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara imepanga kuanza Mradi wa *BBT* kwa halmashauri 100 zitakazotenga maeneo yenye hekta 200 kwa kujenga miundombinu ya umwagiliaji na kutoa utaalam. Aidha, halmashauri zitakuwa na jukumu la kudahili vijana kutoka katika halmashauri husika ili waweze kunufaika na programu hiyo. Hivyo, namshauri Mheshimiwa Mbunge ahimize halmashauri yake itenge eneo litakalohitajika ili iwe miongoni mwa halmashauri 100 zitakazonufaika na mpango huo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mgalu.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, natoa pole kwa wananchi wenzangu wa Rufiji wakiwemo wanawake na watoto kwa janga kubwa la mafuriko linaloendelea kutokana na mvua nyingi. Pia nampa pole Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Rufiji, Mheshimiwa Mchengerwa, lakini niishukuru sana Serikali kwa kutukimbilia kwa haraka kupitia Kitengo cha Maafa kwa Wilaya za Rufiji na Kibiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya salamu hizo za pole, naomba sasa kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa kupitia ukurasa rasmi wa Mheshimiwa Waziri Bashe amefahamisha kwamba tarehe 20 Serikali itatangaza kazi ya ujenzi wa mabwawa ya umwagiliaji ya Ngorongo na Umwe; na kwa kuwa, mabwawa haya yanatarajia pia kushughulikia changamoto ya mafuriko; je, Serikali haioni sasa ipo haja ya Mradi huu wa *BBT* kwa Bonde la Rufiji hususan Wilaya ya Rufiji kwenda sambamba na ujenzi wa mabwawa haya ambayo yanatarajiwa kujengwa na Serikali? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa inapotokea mafuriko mashamba ya umwagiliaji yanapata changamoto kubwa ya kuharibiwa kwa mazao, kwa mfano Skimu ya Umwagiliaji ya Bagamoyo, inapotokea tatizo hilo wananchi hao wanaendelea kulipa tozo na ada mbalimbali kwenye Mfuko wa Umwagiliaji wa Taifa. Je, Serikali haioni ipo haja ya kuja na mwongozo kwamba, endapo kunatokea mafuriko na yanaharibu mashamba ya umwagiliaji na wananchi hawapati mazao, waweze kupewa nafuu katika tozo inayotakiwa kulipwa kwenye Mfuko wa Umwagiliaji wa Taifa kwa kuwa wamepata matatizo? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Wizara ya Kilimo kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji mwezi huu tutatangaza *tender* ya kujenga mabwawa makubwa mawili katika ile *downstream* ya Mwalimu Nyerere *Hydropower* hususan katika

eneo la Ngorongo pamoja na Mbatia Mtuli eneo la Umbwe kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri, huo ndiyo msimamo na haya ni maelekezo ya Mheshimiwa Rais ambayo aliyatoa wakati ametembelea katika Bwawa la Mwalimu Nyerere. Kwa hiyo, hilo ni kweli na linakwenda kutekelezeka kuhakikisha kwamba tunapunguza athari za mafuriko katika eneo la Bonde la Mto Rufiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili kuhusu mwongozo, nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, ushauri wake tumeupokea na tutaufanyia kazi kwa sababu jukumu la Serikali ni kusikiliza wananchi wake. Ahsante.*(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Salim Alaudin Hasham.

Na. 63

**Umiliki wa Msitu wa Hewa Ukaa Uliopo Kituti hadi Mgolo Ulanga**

**MHE. SALIM A. HASHAM** aliuliza: -

Je, lini Serikali itatoa majibu juu ya umiliki wa Msitu wa Hewa ya Ukaa uliopo Kituti hadi Mgolo?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 23 cha Sheria ya Misitu kimeweka utaratibu wa uanzishaji na usimamizi wa maeneo ya misitu kisheria. Kupitia Tangazo la Serikali Na. 783/2022, Wizara ilikamilisha taratibu za awali za kutoa notisi ya siku 90 za nia ya Serikali ya kuanzisha rasmi Msitu wa Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga. Kwa sasa Wizara inakamilisha taratibu za kisheria za kuanzisha msitu huo ambao utakuwa chini ya umiliki wa Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Salim.

**MHE. SALIM A. HASHAM:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naipongeza Serikali kwa hatua nzuri ambazo imezichukua, je, Serikali haioni tija kuharakisha jambo hili kwa sababu limekuwa ni jambo la muda mrefu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kutokana na Jimbo la Ulanga kuwa limezungukwa na msitu pamoja na hifadhi na tembo wamekuwa ni kero kubwa sana kwa wananchi wa Jimbo la Ulanga. Je, nini mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba inadhibiti tembo hao kwa sababu imekuwa ni kero kubwa sana kwa wananchi wa Jimbo la Ulanga? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaona nia, inaona haja ya kuharakisha jambo hili na ndiyo maana kazi kubwa imefanyika ya kuhakikisha mchakato wote umekwenda kama unavyotakiwa, sasa tuko katika hatua za mwisho za kukamilisha taratibu za kisheria. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge ndani ya mwaka huu wa fedha jambo hili litakamilika. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kendege.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kwamba biashara ya hewa ukaa ni biashara ambayo ni mpya kwa nchi yetu ya Tanzania, hivyo elimu inahitajika kutolewa ili maeneo mengi ikiwemo Halmashauri ya Kalambo iweze kufaidika. Je, ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba tunanufaika na biashara hii? Nakushuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba ipo haja ya elimu ya jambo hili kutolewa na ndiyo maana Ofisi ya Makamu wa Rais, eneo la Mazingira imekuwa ikiendelea kutoa elimu hii. Nimwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba

Wizara ya Maliasili kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira tutaendelea kufanya jambo hili ili uelewa uweze kusambaa kwa wananchi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Robert Chacha.

**MHE. ROBERT C. MABOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. Je, Serikali italipa lini kifuta jasho na kifuta machozi kwa wananchi wa Jimbo la Bunda Mjini?

**NAIBU SPIKA:** Hebu rudia tena swali lako.

**MHE. ROBERT C. MABOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali italipa lini kifuta jasho na kifuta machozi kwa wananchi wa Jimbo la Bunda Mjini? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa hebu rudia tena swali lako.

**MHE. ROBERT C. MABOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali italipa lini kifuta jasho na kifuta machozi kwa wananchi wa Jimbo la Bunda Mjini ambao mazao yao yameliwa?

**NAIBU SPIKA:** Sasa swali hilo liletwe kama swali la msingi.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya.

Na. 64

**Mafunzo ya Mgambo kuwa Sehemu ya JKT**

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kufanya mafunzo ya mgambo kuwa sehemu ya mafunzo kwa vijana wanaokosa nafasi ya kujiunga na JKT?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa *Engineer* Stella Martin Manyanya, Mbunge wa Nyasa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Akiba (Jeshi la Mgambo) lilianzishwa kwa Sheria ya Jeshi la Akiba Na.2 ya mwaka 1965 ili kuandaa nguvu ya akiba kwa ajili ya kusaidia Jeshi la Kudumu wakati wa vita, operesheni, majanga na kuuandaa umma wa Watanzania ili waweze kuelewa kuwa dhana ya ulinzi wa Taifa ni jukumu la kila Mtanzania. Vijana 600 kutoka kila Mkoa hupata mafunzo kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Kujenga Taifa lilianzishwa kupitia Sheria ya Jeshi la Kujenga Taifa Na.2, Sura ya 193 ya mwaka 1964 ambayo ilirejewa mwaka 2002 kwa malengo ya ulinzi wa Taifa, kujenga uzalendo na mshikamano, uzalishaji mali na kutoa elimu ya kujitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzishwa kwa vyombo hivyo kulilenga mahitaji tofauti. Kwa muktadha huo, hakuna mpango wa kuyafanya mafunzo ya Jeshi la Akiba kuwa sehemu ya mafunzo ya vijana wanaokosa nafasi za kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa. Aidha, vijana wenye sifa wanaruhusiwa kuomba kujiunga na mafunzo ya Jeshi la Akiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Manyanya.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hili Jeshi la Akiba (mgambo) limeonekana kuwa na hadhi tofauti kidogo ikilinganishwa na Jeshi la Kujenga Taifa na tumeshuhudia kwa siku za hivi karibuni kabla ya marekebisho kwamba hata ajira zikitangazwa zilikuwa zinalenga zaidi Jeshi la Kujenga Taifa katika baadhi ya maeneo. Je, Serikali haioni kwamba

iko haja sasa ya kuboresha haya mafunzo ya Jeshi la Mgambo ili kuwavutia vijana wengi zaidi waweze kwenda huko na kuwezesha uwiano na Jeshi la Kujenga Taifa ukizingatiwa kwamba Jeshi la Kujenga Taifa halina uwezo kwa sasa wa kuwachukua vijana wote wenye uhitaji wa kupitia huku. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze kwa kuendelea kutoa umuhimu kwa Jeshi la Akiba ambalo ni jeshi muhimu sana, kama nilivyotoa majibu katika swali la msingi majeshi haya mawili yameanzishwa kwa madhumuni tofauti, lakini ushauri alioutoa ni ushauri mzuri, ukizingatia sasa hivi tunajaribu kuangalia ni jinsi gani tunaweza tukawachukua vijana wote wanaostahili kwenda kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa. Kwa hiyo pamoja na kwamba mahitaji hayo ya majeshi haya ni tofauti, tutauangalia huo ushauri tuone kama unaweza kufanyiwa kazi namna gani.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Anna Richard Lupembe.

Na. 65

**Ujenzi wa Minara ya Mawasiliano Litapunga – Nsimbo**

**MHE. ANNA R. LUPEMBE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga minara ya Mawasiliano katika Kata ya Litapunga – Nsimbo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuendelea kuniruhusu kutimiza majukumu yangu. Pia nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuniamini na kunipa kazi na namuahidi kuendelea kujituma zaidi. Namshukuru zaidi pia Dkt. Tulia Ackson, Spika na Rais wa *IPU* pamoja na wewe Mheshimiwa Naibu Spika kwa kuendelea kutuongoza vizuri hata tunaweza kutimiza majukumu yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Juma Hamid Awesso, kwa kunipa ushirikiano zaidi ya miaka mitatu na kunifanya niweze kutimiza majukumu yangu. Mwisho si kwa umuhimu, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Nape Nnauye kwa kunipokea vizuri ndani ya Wizara pamoja na Katibu Mkuu na Menejimenti, nawaahidi kutoa ushirikiano wangu wa dhati ili kuweza kutimiza majukumu ya Wizara yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mbunge wa Nsimbo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF)* imeingia makubaliano na Shirika la Mawasiliano *(TTCL)* kwa ajili ya kupeleka huduma ya mawasiliano katika Kata ya Litapunga ambapo *TTCL* anajenga mnara katika Kijiji cha Kambuzi ‘A’ ambao utahudumia Vijiji vya Kambuzi ‘A’ na Kambuzi ‘B’. Utekelezaji wa mradi huu ni miezi 24 kuanzia tarehe 13 Mei, 2023 Mkataba uliposainiwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lupembe.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo mawili. Swali la kwanza; kwa kuwa, Kata hii ina vijiji 10 na hakuna mawasiliano kabisa na kwa

wakati huu mawasiliano ni biashara na katika shughuli mbalimbali watu wanawasiliana na sasa hivi mkataba umeenda kwenye vijiji viwili. Je, ni lini Serikali itapeleka mawasiliano katika vijiji nane vilivyobaki?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; kwa sababu mradi huu wa Vijiji viwili Kaguzi 'A' na Kaguzi 'B' umechukua muda mrefu, sasa hivi takribani tunaelekea mwaka mzima mradi ule haujakamilika kabisa wala haujajulikana utaanza lini. Je, Waziri yupo tayari kuambatana nami ili aende kuhakikisha na kuona uhalisia wa mradi huo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Anna Lupembe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Anna Lupembe kwa kufuatilia hili na niseme tu kama yeye alivyosema ni mradi ambao sasa hivi umeshaweza kutekelezwa ndani ya mwaka mmoja na mkataba uliosainiwa ni miezi 24. Kwa hiyo nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba, mradi huu utatimia ndani ya wakati na nipo tayari kuambatana naye baada ya Bunge hili kwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika vijiji hivi 10 mara baada ya mchakato kukamilika na niwasihi wenzetu wa mamlaka zinazoshughulikia vibali, kuhakikisha suala hili linapata utekelezaji wake kwa haraka ili huu mnara katika vijiji hivi kumi uweze kutekelezeka.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kipindi cha bajeti maswali ni saa moja na muda wetu umeshapita.

Waheshimiwa Wabunge, wageni waliopo Bungeni asubuhi hii ni waliokaa jukwaa la Spika ambao ni watumishi wawili kutoka Bunge la Uganda, Ndugu Kabanekera Ruth, Msaidizi wa Mkuu wa

Utawala na Ndugu Mirembe Lubega, Msaidizi Mkuu wa Utawala. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge ambao ni mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana, Waziri wa Katiba na Sheria ambaye ni Diwani wa Keko kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 14 wa Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa, Naibu Waziri wa Madini, Viongozi wa Jamii ya Kimasai kutoka Wilaya ya Simanjiro, Mkoa wa Manyara. Karibuni. *(Makofi)*

Masai ninyi si mnavaa nguo nyekundu, vipi tena leo? Haya karibuni. *(Makofi/Kicheko)*

Tunao wageni 21 wa Mheshimiwa Rehema Migilla ambao ni Makatibu wa CCM, Kata za Jimbo la Ulyankulu, Mkoa wa Tabora. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Dkt. Florence Samizi ambaye ni Msemaji wa Tawi la Simba *VIP* 'A', Jiji la Dar es Salaam. Karibu. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Timotheo Mnzava ambao ni rafiki zake kutoka Shirika la *PETpro* Tanzania linalosimamia na kutekeleza wajibu wa wazalishaji kuhakikisha ukusanyaji wa urejelezaji *(recycling)* wa vifungashio vyao baada ya matumizi. Karibuni. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Zuena Bushiri ndugu zake kutoka Moshi Mkoa wa Kilimanjaro wakiongozwa na mjukuu wake Ndugu Adriana Ally. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ambao ni:-

Tunao Viongozi 13 wa Menejimenti ya Shirika lisilo la Kiserikali la *Youth Integration and Environment Organization (YINEO)*

wakiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika hilo Ndugu Farijila Kunga. Karibuni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Katibu wa Bunge anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba leo tarehe 8 mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge saa 7.00 mchana kutakuwa na zoezi la ugawaji wa mchele. Mchele huo utagawiwa katika eneo la *basement* karibu na geti la Waziri Mkuu, tunashauri kila Mbunge achukue mwenyewe. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mnaona kwenye *order paper* yetu kuna uchaguzi wa Wenyeviti wa Bunge, kutokana na wachangiaji kuwa wengi tunaendelea na kuchangiaji leo, ratiba hii itaendelea kwa kipindi kinachokuja.

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaanza na Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda, wajiandae Mheshimiwa Manyinyi na Mheshimiwa Gambo.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nitumie nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kuendelea kutupa afya na uhai ili tuendelee kuwatumikia wananchi waliotuchagua.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama kuchangia hoja ya Ofisi ya Waziri Mkuu lakini kwanza ningependa kuchukua nafasi hii

kuipongeza sana Serikali hasa nikianza na kinara mwenyewe kiongozi wetu mkuu, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi nzuri inayoendelea kufanywa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuwatumikia wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe shukrani na sifa kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu mwenyewe kama Msimamizi wa Shughuli za Serikali, naamini wengi watakuwa mashahidi na watakubaliana na hoja yangu kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu ameendelea kuonesha uwezo mkubwa katika kufanya kazi yake. Kwa kweli naweza nikasema hata sisi wengine ambao tumekaa katika uongozi kwa muda, tunatamani tungekuwa na tabia na mwenendo unaofanana na Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya hilo napenda niwapongeze Mawaziri wanaofanya kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu, dada yangu Mheshimiwa Jenista Mhagama na Naibu Mawaziri wote kwa kazi kubwa wanayoifanya katika Ofisi ya Waziri Mkuu. Wakati nasimama hapa Watanzania wenzetu wakiwa wanakumbana na kadhia kubwa ya mafuriko, nami pia katika Jimbo langu la Kigoma Mjini katika Kata ya Katubuka yametokea mafuriko makubwa. Mafuriko hayo yamesababisha zaidi ya nyumba 80 kuwa hazikaliki na kufanya Makanisa mawili, kituo kimoja cha mafuta na barabara itokayo Mwanga kuelekea Uwanja wa Ndege wa Kigoma kufungwa na kutokutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili ni kubwa napenda niendelee kuwapa pole wananchi wangu na nitumie nafasi hii kuiomba Serikali wakati inatazama maeneo mengine itazame na eneo hili. Nimemsikia dada yangu Mheshimiwa Asia Halamga wakati anashukuru ameeleza kwamba kule Hanang wamempeleka mtu anaitwa Msangi kuendelea kuangalia hali ilivyo kule, naomba kama kuna Msangi mwingine amebaki wamlete pale Kigoma Katubuka ili aendelee na yeye kuona namna gani anashirikiana na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Mkoa ikiongozwa na Mkuu wa Mkoa, Kamishna Thobias Andengenye pamoja na Mkuu wetu wa Wilaya, Mheshimiwa Salum Kali na Kamati zao za Ulinzi na Usalama wanaendelea kufanya kazi kubwa, lakini wanahitaji msaada mkubwa wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Kitengo cha Maafa ili kabla mambo hayajawa makubwa, kuweza kunusuru hali hiyo ya Kata ya Katubuka katika Jimbo la Kigoma Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo napenda niliseme pamoja na kazi nzuri na kubwa inayoendelea kufanywa na Serikali, zipo changamoto ambazo ningependa Serikali izichukue na hasa Ofisi ya Waziri Mkuu katika suala la usimamizi. Moja ni jambo ambalo halitupi furaha sisi wawakilishi wa wananchi juu ya namna ambavyo Serikali inafanya kazi na sekta binafsi hapa nchini. Tatizo kubwa lililopo ni kwamba hii sekta binafsi inachelewa kukua na inarudishwa nyuma na Serikali yenyewe inapotoa kazi kwa sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na tatizo kubwa la ulipaji wa madeni ya kazi ambazo zinafanywa na wakandarasi na wazabuni wanaotoa huduma kwa Serikali. Jambo hili ni kubwa sana, wakati mwingine wanatoa huduma na kufanya kandarasi hizi za Serikali kwa kukopa kutoka benki. Benki zinaendelea kuwadai na riba zinaendelea ku-*accumulate,* lakini wakati huo huo Serikali haichukui hatua za kulipa kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ielewe sekta binafsi ndiyo *engine* ya uchumi wa Taifa letu. Wanapochelewa kuwalipa wanarudisha nyuma maendeleo ya sekta binafsi na pia ni maendeleo ya Watanzania na ifahamike kwamba mikataba ya wakandarasi wa ndani na wakandarasi wa nje ni tofauti. Wakandarasi wa nje wanapochelewa kulipwa wanawekewa riba ili kuilinda pesa yao iendelee kuwepo hapo, lakini wakandarasi wa ndani hawana hiyo riba. Kwa hiyo anafika mahali anacheleweshwa kulipwa mwaka mmoja, miaka miwili, miaka mitatu na pesa ni ile ile na ambayo yeye anaimaliza yote kwenye riba ya benki na wakati mwingine haitoshi, hivyo anaingia hasara. Wakandarasi wetu

wengine wamefika mahali wamekuwa maskini na wengine wamekufa hata kwa kihoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe Serikali jambo hili wasilifumbie macho, hatuwezi kupata baraka za kuendesha Serikali ambayo wananchi wake wananung'unika. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, yeye ni mtu makini, mwenye huruma na mfuatiliaji; asaidie kuhakikisha hawa wakandarasi na wazabuni wanalipwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo ni pale mahali ambapo Serikali imeamua kutwaa ardhi kwa maendeleo mbalimbali. Kwa mfano Mkoani kwangu Kigoma, Uwanja wa Ndege wa Kigoma unataka kupanuliwa; ni kazi nzuri na tunashukuru sana na hatua zinaendelea, lakini yapo maeneo ya wananchi ambayo wamechukua, tangu wayachukue wamewafanyia *valuation* tayari, ripoti imetoka wamesaini, wamekubali. Leo zaidi ya miezi sita wananchi wale wameambiwa wasiendeleze chochote, wasubiri kulipwa, lakini hawajalipwa mpaka leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa jambo hili ni baya sana. Watu wamekwishapanga mipango yao, mwananchi anajua natoka hapa, nahama, nisijenge choo na mvua zinaendelea kunyesha zinaharibu maeneo yao, lakini wanaona hata wakijenga wanatupa pesa kwa sababu tayari *valuation* ilishafanyika. Kwa hiyo ninachomwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu kupitia Ofisi yake wahakikishe maeneo ya wananchi wanayoyatwaa kwa shughuli za maendeleo wanalipa kwa wakati ili kuruhusu wananchi hao waendelee na shughuli zingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka nilizungumzie ni suala la mifumo. Bahati nzuri Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amelitolea maelekezo kutaka mifumo isomane. Moja ya jambo ambalo nataka kulizungumza kuhusu suala la mifumo ni suala la namna ambavyo Serikali wameamua kupeleka mifumo hii na kuwashirikisha wananchi katika mifumo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano mfumo kama TAUSI, ili mwananchi aweze kukata leseni ya biashara kwenye halmashauri lazima aingie kwenye mfumo huu. Wananchi wangapi ambao wana uhakika wameelimika kiasi cha kuutumia mfumo huu? Ni maeneo mangapi ya nchi yetu ambayo wanajua kuna *internet facility* ambapo wananchi wanaweza wakatumia mfumo huu? Halmashauri zetu nyingi tangu wameanzisha mfumo huu mapato ya leseni za biashara yameshuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sikatai mifumo, ninachosema tusiende *speed* katika jambo ambalo tunajua kabisa kwamba, hili jambo halijawafikia wananchi kwa kiasi kikubwa. Wa-*introduce* Mfumo wa *NeST* ili wakandarasi wote wanaotaka kuomba kazi waingie kwenye mfumo huu. Wakandarasi wengi wameshindwa kuomba kazi kwenye mfumo huu na hata mfumo wenyewe hauko *stable* kiasi hicho hata Maafisa wa Serikali waliowa-*train* wengine wamekwenda kuchukua mafunzo mwaka mzima, wenyewe wanataka wawa-*train* kwa siku tatu waendeshe mfumo huu. Wafanyakazi wengi wa Serikali wameshindwa kuendesha mfumo huu na hawana majibu ya mfumo huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachosema, tuna nia njema kabisa ya kutumia mifumo kuharakisha utekelezaji wa kazi za Serikali, lakini tusiende haraka kiasi hicho cha kuathiri shughuli za maendeleo. Sisi pale Kigoma Halmashauri yetu ya Manispaa ya Kigoma Ujiji ilikuwa imebuni mradi mzuri sana wa maendeleo, umekwama mpaka sasa mradi huo kuanza kwa watu kushindwa kuomba kupitia Mfumo wa *NeST*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais amekwishalisema jambo hili, lakini nimwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu kupitia…

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimpe taarifa mzungumzaji, anazungumza vizuri sana. Sasa hivi kupitia huo mfumo hata ukitaka kununua tairi la gari ya halmashauri mpaka uingie kwenye mfumo. Kwa hiyo tairi lile litanunuliwa na mtu wa Kigoma au gari lipo Liwale, lakini tairi mpaka lipitie kwenye *tender*, mtu wa Kigoma alete tairi Liwale. Huo mfumo haujakaa vizuri. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kilumbe.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na nimeipokea taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimalizie kwa kuzungumzia suala zima la mawasiliano ndani ya Serikali. Pamoja na kuanzishwa kwa mifumo hiyo, inaelekea bado kuna maeneo ambayo kuna mawasiliano duni na hili nilikuwa naomba katika usimamizi, Mheshimiwa Waziri Mkuu alichukue. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepitisha hapa katika Bunge hili bajeti, kodi inayoitwa *hotel levy* inayotozwa na halmashauri, 10% kwa kila mtu anayelala kwenye *guest house,* ikashuka kutoka 10% kuja asilimia tano, lakini mpaka leo ninavyokueleza bado zipo halmashauri zinatoza 10% na wanasema hawana mawasiliano yoyote, hawana mwongozo wowote na hawana waraka wowote… *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante muda wako umekwisha. Mheshimiwa Manyinyi Mathayo atafuatiwa na Mheshimiwa Gambo na Mheshimiwa Butondo ajiandae.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye hii

Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Naungana na wenzangu kwanza kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi ambayo ameendelea kuifanya katika nchi yetu. Nampongeza na Mheshimiwa Waziri Mkuu kama msaidizi wake wa karibu kwa namna wanavyoendelea kushughulikia changamoto za wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mambo na maendeleo mazuri yaliyopo, lakini zipo baadhi ya changamoto ambazo Serikali inahitaji izifanyie kazi tena kwa haraka. Kwanza naendelea kuipongeza sana Serikali kwa namna ilivyoendelea kuboresha elimu kwa kujenga vyumba vya madarasa vizuri pamoja na shule. Zipo shule nyingi ambazo Serikali imezijenga nzima nzima, kwa hiyo wananchi wetu wanaendelea kufaidika na wanaendelea kusomea mahali pazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio hayo kwenye upande wa elimu, wote tunakubaliana kwamba zipo shule ambazo Mheshimiwa Rais ametoa fedha, tumejenga vyumba vizuri vya madarasa. Mfano, unakuta darasa la tatu A ni chumba kizuri, kipya mpaka kina kila kitu, lakini kuna chumba kingine watoto wanakaa chini kwa maana kwamba, baadhi ya vyumba vimechakaa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hili tumekuwa tukilisema kila mara na kusema ukweli imekuwa ni kero kubwa. Kwa hiyo nimwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu aweze kuona ni kwa kiasi gani sasa vyumba vile vyote ambavyo vimechakaa vinaweza kujengwa vizuri. Hata yale maboma ambayo hayajakamilika, yakamilishwe ili watoto wote wajione katika *level* sawa, kuliko hii ambayo inaonekana, wengine wanasoma vizuri lakini wengine hawasomi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo suala la pili ambalo kusema ukweli ni changamoto bahati nzuri mwenzangu Mheshimiwa Kilumbe amelisema ni hili suala la wazabuni. Nikazie tu kwa kusema kwamba, wakati mwingine yawezekana Serikali huwa

inadhamiria kufilisi wananchi wake. Maana ukiangalia Serikali yoyote ile ina jukumu kubwa la kuwajengea watu wake uwezo ili waendelee kuwa na uwezo mzuri, waendelee kuwa matajiri ili wailipe Serikali kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye upande huo, upande wa wakandarasi na wazabuni yaani inaonesha dhahiri kwamba Serikali inawapa fedha, lakini baadaye inaamua ku-*drain* zile fedha. Mfano pale Musoma, wapo wazabuni ambao wame-*supply* vyakula mashuleni, karibu miaka 10 hawajalipwa. Sasa kama huyo mtu aliona hiyo ni biashara, akaenda benki, akakopa fedha, aka-*supply,* lakini miaka 10 hajalipwa, kinachofuatia ni benki kwenda kuuza nyumba yake na huyo mtu yuko hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kutokana na hali hiyo hata watu wengine wanafika mahali wanapoteza maisha. Sasa ndiyo maana nasema, kwa sababu Serikali inajua, basi maana yake ni kwamba imedhamiria hawa watu wafilisike. Kibaya zaidi, unakuta mwingine anadai miaka mitano, miaka kumi halafu anakosa mtaji anapewa mzabuni mwingine, anaanza ku-*supply* na hapo hapo anaanza kulipwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani hiyo siyo haki, Serikali inapaswa ilisimamie hilo na ione kwamba ni kwa kiasi gani itawasaidia watu wake kwa maana ya wakandarasi, lakini na hao wazabuni ambao wameendelea kusaidia watu wetu. Kwa hiyo nadhani katika hilo, Serikali ina kila sababu ya kulitafutia majibu na ione kwamba inamaliza hilo tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu ambalo na lenyewe nimeshindwa kuelewa ni hili la wafanyakazi kuhusiana na suala la kikotoo. Hili suala la kikotoo ni jambo ambalo liko wazi, siku za nyuma wastaafu walikuwa wanalipwa karibu ya nusu ya mafao yake halafu hiki kingine analipwa kidogo kidogo. Kwa sababu yule mtumishi siku ameajiriwa alikuwa anajua kabisa kwamba, baada ya muda fulani atastaafu, kwa hiyo tafsiri yake alikuwa anajiandaa, anajua

kwamba akistaafu atapata fedha yake *lump sum* ataendelea na maisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa leo unapomkata mpaka unamrudisha kwenye *one third* maana yake ni kwamba hizo zingine unasema utamlipa kila mwezi, mwishowe anapata *frustration* baada ya miaka mitano anapoteza maisha. Sasa naanza kujiuliza; hii najua ni Serikali ya wananchi na hao wananchi au hao watumishi wao mapenzi yao wanapenda walipwe ile *lump sum* ya kutosha ili maisha yake yaendelee. Sasa wewe Serikali inakuhusu nini mpaka useme mimi sikulipi hivi, badala yake naendelea kukulipa nusu nusu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe Mheshimiwa Jenista Mhagama kwamba, ni vizuri waone namna gani tunaweza kulimaliza hili.

**WABUNGE FULANI:** Siyo Mheshimiwa Jenista ni Mheshmwa Ndejembi.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Ohoo! Ni Mheshimiwa Ndejembi, mdogo wangu Mheshimiwa Ndejembi sasa ndiyo umeingia kwenye hii Wizara mpya, nikuombe kabisa na juzi hata nilisikia Mheshimiwa Rais anasema amekupeleka hapo ufanye mambo. Naamini kwamba kati ya jambo utakalolifanya na wananchi hasa watumishi Watanzania wakakuelewa, ni pale utakapowarudishia kile kikotoo chao cha zamani badala ya hiki cha sasa. Kwa hiyo nadhani hilo ni kati ya jambo ambalo ni suala la muhimu sana na Waziri alipe kipaumbele ili hiyo kero ya watumishi wa Tanzania iweze kwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuwa nimezungumza hilo lingine ni salamu tu za Mheshimiwa Waziri Mkuu. Bahati nzuri alikuja Musoma akafanya mkutano mzuri, akafanya ziara nzuri, wananchi wa Musoma wanaendelea kuwa na hamu naye hadi leo na wanamwomba arudi pale Musoma. Hata hivyo, kuna barua yao au kuna ombi lao, wale watumishi waliokuwa wa Kiwanda cha *Mutex*

ambacho kilikuwa kinafanya kazi, Serikali ikaamua tu kukisimamisha kwamba inatafuta mwekezaji mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuwa imekisimamisha wale watu wanadai mafao yao sasa kwa miaka mingi na hadi leo hawajapewa chochote. Matokeo yake wanaendelea kupoteza maisha kwa kuwa wanategemea kwamba watalipwa lakini hawajalipwa. Sasa kwa sababu walimpa barua yao Mheshimiwa Waziri Mkuu, wanaomba safari hii nikirudi, basi nirudi na barua yao ili niweze kuwapa majibu ya matumaini kama wanaweza kupata chochote kwa maana ya kiinua mgongo chao kwa muda wao walioitumikia Serikali hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ni suala la afya. Jana niliuliza swali la nyongeza kwamba, Sera ya Serikali ni kutoa huduma bure kwa watoto wa chini ya miaka mitano na akinamama wajawazito. Bahati nzuri Mheshimiwa Waziri Ummy akalijibu vizuri, akasema hivi "*anakubaliana kwamba ni changamoto na kwa sababu ni changamoto tusubiri ile Bima ya Afya.*" Sasa kwa sababu Serikali imekubali kwamba hili suala sasa la matibabu bure kwa wajawazito pamoja na watoto wa chini ya miaka mitano ni changamoto, basi ni vizuri Serikali kwanza itangaze dhahiri kwamba, kuanzia sasa watoto chini ya miaka mitano waendelee kulipa na wale wajawazito waendelee kulipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu hilo limekuwa ni tatizo. Ukienda kwenye zahanati au kituo afya unauliza wanakwambia wana dawa 98%, lakini wale wazazi wakienda kutibiwa bado wanaombwa fedha. Sasa ndiyo maana nasema kwamba kwa sababu limekuwa ni gumu kwa Serikali, basi iwatangazie wananchi ili waweze kukubaliana na hali halisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, hivi tunavyoelekea kwenye bima ya afya, ushauri wangu wa bure, tuondoe kabisa Serikali kwa maana ya kuwa na vituo vya afya pamoja na zahanati na kwa sababu tutatumia bima ya afya ni vizuri hivyo vituo vya afya, zahanati na hospitali tukavipa kwanza yale Mashirika ya Kidini ili

yaweze kuhudumia, lakini tofauti na hapo tuwape watu binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiendelea sisi kama Serikali kuendesha maana yake ni kwamba zile huduma zitaendelea kuwa za hovyo, ni kwamba *forgery* nyingi zitaendelea kufanyika kutokana na zile bima za afya, kwa hiyo nadhani haiwezi kusaidia. Kwa hiyo, ndiyo maana nasema ushauri wangu tuiondoe kabisa Serikali kwenye kuhudumia wananchi upande wa afya, maana imejaribu mara nyingi na mara nyingi imeendelea kushindwa, kwa hiyo, hilo ndilo ombi langu kubwa kwenye huo upande wa afya…

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mchango mzuri wa Mheshimiwa Mbunge, napenda nimpe taarifa kwamba, tunavyo vituo vya kutoa huduma za afya vinavyomilikiwa na Serikali ambavyo vinatoa huduma bora kuliko huko *private*. Hapa nataka kusema aende Muhimbili akaone mapinduzi makubwa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili chini ya Profesa Mohamed Janabi. Kwa hiyo, kubwa Serikali sasa hivi tunajikita katika kuimarisha usimamizi wa utoaji huduma za afya katika ngazi zote. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Halima, tuko Bungeni hapa, tuko Bungeni hapa, hatuko kwenye uwanja wa michezo, huwezi kuzungumza bila kupewa ruhusa.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, sawa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Manyinyi.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya Mheshimiwa Waziri siipokei kwa sababu gani? Ni hivi, leo hii pale Musoma, ukitembelea zahanati, ukitembelea vituo vya afya, mama mjazito akienda kujifungua pale ni pesa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Manyinyi, kengele ya pili imeshalia.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ndiyo maana tunasema kwamba…

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Manyinyi, kengele ya pili imeshapiga, ahsante.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie tu kwamba,endapo tunadhani kwamba bado Serikali tunao uwezo wa kuendesha, basi tutoe majibu kwamba…

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshindwa kusimamia hizo zahanati na vituo vya afya kuweza kutoa huduma nzuri…

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Manyinyi…

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naam.

**NAIBU SPIKA:** Una hoja mwandikie Mheshimiwa Waziri kwa sababu sasa unachukua muda wa mchangiaji mwingine.

Tunaendelea, Mheshimiwa Gambo, ajiandae Mheshimiwa Butondo.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kupata fursa ya kuchangia kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na nitajitahidi leo angalau kwa asilimia zisizopungua 90 nichangie kikotoo halafu kama muda utabaki, ndiyo nitaangalia masuala mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna bahati moja kubwa sana, Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan mara kadhaa alipokuwa anazungumza na jamii, amekuwa anaonyesha nia ya kutaka kikotoo kifanyiwe kazi kwa maslahi mapana ya wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunukuu tu wakati anazungumza na wafanyakazi ilikuwa ni Mei Mosi, 2022 hapa Dodoma. Alisema kwenye ukurasa wa 18: "Sambamba na suala la malipo ya mafao limetajwa pia suala la kupanda kikokotoo kitakachotoa faraja kwa wastaafu. Nashukuru Katibu Mkuu *TUCTA* wamekwenda mpaka kutaja kiwango. Tulikuwa kwa muda mrefu tukivutana kutoka 25 kwenda 50, lakini leo *TUCTA* wamesema tukutane katikati. Sasa Serikali tutakwenda kukaa katika utatu wetu au sisi na *TUCTA* kuangalia tunavyoweza kufanya, lakini wazo tulilokuja nalo siyo baya."

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo maana yake ni kwamba Mheshimiwa Rais yupo tayari kwenye suala hili. Pia Mheshimiwa Rais wakati anazungumza na Askari Polisi tarehe 23 Mwezi Septemba, 2023. Nanukuu alisema pia; "Kikokotoo tupo tunakifanyia kazi na kuona jinsi ambavyo tunaenda vizuri..."

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maneno haya inaonesha kabisa sisi tuliobaki tuna kazi kubwa ya kufanya kuhakikisha kwamba tunamsaidia Mheshimiwa Rais kwenye nia yake hii njema kwa wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nimeweza pia kupitia sheria na kanuni mbalimbali kama hii ya tarehe 20 Mei, 2022, Kanuni ya tarehe 27 Agosti, 2018, Sheria ya *SSRA* ya 2008, Kanuni ya *SSRA* ya tarehe 17 Agosti, 2018, Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya 2017 pamoja na Maoni ya Kambi ya Upinzani ya 2017. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kwa ujumla wake wenzetu ambao wanashughulikia masuala ya kikokotoo, kwanza kabisa kikokotoo cha kabla ya 2014 kilikuwa ni kikokotoo kizuri sana ambacho Watanzania wengi wanakitaka, kwa sababu kilikuwa chenyewe kimechukua asilimia 50. Kilikuwa kime-*assume* kwamba miaka ya kuishi baada ya kustaafu *(life expectancy)* itakuwa ni miaka kumi na tano na nusu. Pia kilikuwa kimechukua mshahara wa mwisho wa mfanyakazi ambao kwa kawaida ni mshahara mkubwa. Kikokotoo cha sasa kwanza kimepunguza. Ukiangalia *factor* inayotumika pale ya moja chini ya 540 chenyewe kimefanya moja chini ya 580, wakifahamu kwamba *denominator* ikiwa kubwa itakwenda kupunguza jawabu la kule mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia bado wamechukua *range* ya miaka 10, halafu wakasema wanatafuta miaka mitatu iliyo bora. Kwa hiyo, kama mshahara wako ni 2,500,000 na ulikuwa na mwingine 200,000 mwingine 500,000 lazima mshahara wako utapungua na utaathiri pia mafao yako. Pia wamepunguza miaka ya mtu kuishi kwamba, ukistaafu kwa sababu wanajua wanachowalipa ni kidogo, wameona hata ile miaka 15 na nusu hawawezi kufika, wameishusha sasa wameipeleka miaka 12 na nusu. Kitu ambacho nadhani siyo sawa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimechukua *sample* ya mishahara na nimefanya mahesabu. Kwa mfano, mfanyakazi ambaye anastaafu akiwa na wastani au *average* ya mshahara wa 800,000 kwa kikikotooo cha kabla ya mwezi Julai, 2014, wale waliokuwa mifuko ya *LAPF* na *PSPF* alikuwa anapata 57,866,666. Kwa kikokotoo cha sasa atapata 28,675,862. Tofauti yake ni 29,190,804. Kwa mwezi atakuwa anapata 400,001 kwa kikokotoo cha zamani na cha sasa atakuwa anapata 388,137. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu ambaye mshahara wake ni 1,500,000 kwa kikokotoo cha kabla ya Julai, 2014 alikuwa anapata 108,500,000. Kwa kikokotoo cha sasa anapata 53,767,101 ambayo tofauti yake ni 54,732,000. Kwa yule ambaye mshahara wake kama *level* ya Wakurugenzi 3,720,000. Kwa kikokotoo cha kabla ya Julai, 2014 angepata 269,080,000, lakini kwa kikokotoo cha sasa atapata 133,442,000 ambayo tofauti yake anakuwa amepunjwa 135,000,000. Mifano ipo mingi ila nitoe tu mifano ya kuanzia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa sasa hoja yangu ni nini? Katika hali ya kawaida kwanza yamefanyika makosa makubwa sana. Nafahamu sheria yoyote inavyotungwa huwa inaanzia pale ilipotungwa. Kwa hiyo, mfanyakazi yoyote ambaye sheria hii imemkuta kwa maoni yangu alitakiwa alipwe na sheria ya zamani. Maana yake ni kwamba, nimeajiriwa leo nafahamu kwamba nikistaafu nimeshakokotoa *formular* yangu ni hii, nitalipwa kiasi fulani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakuja hapa 2018 tunaweka mambo yetu, tunakwenda 2020 tumebadilisha kabisa kikokotoo chenyewe, tunakwenda kumuathiri kabisa hata mfanyakazi ambaye sheria iliyotungwa 2022, imemkuta, kitu ambacho nadhani siyo sawa. Kama kuna ulazima sana nadhani kikokotoo hiki kingeanza kwa wale waajiriwa wapya ambao wataajiriwa mara baada ya sheria kusainiwa, kwa sababu baada ya hapo miaka itakuwa mingi watakuwa na muda pia wa kuendelea kujadiliana na kushauriana huko mbele ya safari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini tumefika hapa? Tumefika hapa kwa sababu miongoni mwa waliosababisha changamoto hii kwa watumishi ni Serikali yenyewe. Tumesikia Ripoti za CAG mara nyingi hapa wametueleza namna ambavyo kumekuwa na madeni mengi ambayo Serikali ilitakiwa ilipe lakini imeshindwa kulipa. Tumeelezwa hapa tumekuwa na changamoto kubwa sana, tumekuwa na uwekezaji usio na tija na mifano ipo mingi ya miradi iliyowekwa lakini hamna tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeelezwa pia hapa kulikuwa na changamoto ya gharama kubwa za uendeshaji. Mifuko ilikuwa mitano, kila Mfuko una bodi yake na uendeshaji wake na ofisi yake. Kwa hiyo, unagundua kwamba, kuyumba kwa Mfuko sababu yake siyo tu kikokotoo. Sababu yake kubwa ni namna ambavyo tulikuwa tunaisimamia na kuiendesha Mifuko siku za nyuma. Sasa changamoto ninayoiona, badala ya Serikali itafute namna ya kurekebisha changamoto zilizopo, yenyewe inakwenda kumuadhibu mtumishi ambaye yeye ni *victim* wa haya ambayo yanafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba nishauri kwenye mambo manne. Jambo la kwanza, Serikali irejeshe fedha zote ambazo imezichukua kwenye Mifuko ili kuirudishia uhai Mifuko yetu ya Hifadhi za Jamii. Ushahidi ni kwamba *CAG* ametuambia mara nyingi namna ambavyo hela zimechukuliwa na Serikali kwenda kufanya shughuli tofauti na shughuli zinazohusiana na watumishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Serikali tutenge bajeti, kwa sababu ukifanya utafiti unaona kwamba pengine kwa mwaka tunalipa *approximately* 1.5 *trillion,* kwa wastani, ukikadiria, lakini unaambiwa kwamba, ili waweze kulipa inavyotakiwa inabidi pengine tuongeze kati ya bilioni 200 mpaka 300. Hili Bunge lako ndiyo kazi yake kupitisha hiyo hela ili kuleta ahueni kwa watumishi. Watuletee hapa kitakachopungua tuingize kwenye bajeti ili tukapeleke amani kwa watumishi na wafanyakazi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu wa tatu ni kwamba, kanuni mpya ya kikokotoo kama nilivyosema ni vizuri sasa isiwaadhibu wale ambao wameikuta hii sheria. Ni vizuri sasa kama inataka kuanza, basi ianze pale ilipotungwa ili watumishi wa kule nyuma wasipate changamoto kubwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la nne, katika ushauri wangu, ikikupendeza na Bunge lako Tukufu, tumeona Serikali wamehangaikia kwa muda mrefu sana suala hili, ni namna

ambavyo Mheshimiwa Rais ameonesha nia ya kutaka kulifanyia kazi jambo hili. Bunge lako Tukufu liunde Kamati Maalum, Kamati Ndogo kwa ajili ya kwenda kulifanyia kazi jambo hili ili hatimaye tuweze kumshauri Mheshimiwa Spika na Serikali kwa ujumla…

**NAIBU WAZIRI, OFISI WA WAZIRI MKUU, KAZI AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gambo kuna Taarifa.

**TAARIFA**

**NAIBU WAZIRI, OFISI WA WAZIRI MKUU, KAZI AJIRA VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na mchango mzuri wa Mheshimiwa Gambo katika suala la kikokotoo, si kweli kwamba Serikali inawapa mzigo au inawaumiza wananchi. Katika mchango wake ni vizuri pia akumbuke na aweze kuelezea, kama ameli-*study* vizuri jambo hili, kuhusiana na maslahi wanayopata wale *pre* 99 ambao wao katika mifuko ya awali walikuwa wanapewa mafao bila hata kuchangia shilingi moja kwenye Serikali na Serikali imekuwa ikilipia. Baada ya mabadiliko ya sheria hata wale ambao hawakuwahi kuchangia ilibidi Serikali ibebe mzigo huo kutengeneza nafuu kwa hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo natamani atoe ule usawa wa kutokuonea katika maelezo, tuangalie ni wangapi waliopata nafuu. Ukiangalia hata katika awamu ya awali, kuna zaidi ya 81% ya wachangiaji ambao wanaenda kupata nafuu kulingana na hali ilivyokuwa awali kwenye ile hali ya mifuko. Kwa hiyo katika maelezo yetu nadhani kwenye hatua ya baadaye tutaeleza, lakini nilitamani kuona badala ya kuipa mzigo Serikali aeleze uhalisia wa *pre* 99 jinsi hali ilivyokuwa na nafuu ambayo ilitolewa na Serikali katika *calculations.*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bulaya, Bunge linakwenda kwa utaratibu. Kama una hoja unaweza kuomba taarifa. Huruhusiwi kusema unachotaka kusema ndani ya Bunge. Hii ni mara ya pili sasa unakataa maelekezo ya kiti. Nakwambia wewe, Kanuni ya 84 inaeleza vizuri sana na wewe bado mdogo, unaweza ukapotea. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Gambo malizia.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niwe wazi taarifa yake siipokei. Mheshimiwa Naibu Waziri ni miongoni mwa watu ambao mimi nawaheshimu sana. Najua ni Mbunge mwenzangu, tunatetea hapa wananchi, nimshauri tu kwamba kwa sababu wananchi wanafahamu kwamba kikokotoo hiki hakitugusi sisi kama Wabunge, kwa hiyo nimwombe tuungane kukisemea ili tuweze kuwapa *support* ya pamoja wananchi wenzetu. *(Makofi)*

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuna taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gambo, muda wako umekwisha kaa.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Butondo, jiandae Mheshimiwa Emmanuel Shangai. *(Makofi)*

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika hoja ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kadri mjadala unavyoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri, lakini bajeti ambayo ina matumaini makubwa. Hotuba hii ni hotuba ambayo itakuwa imebeba mambo makubwa na maono makubwa kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Ndejembi, Naibu Mawaziri, Mheshimiwa Katambi pamoja na Mheshimiwa Ummy kwa namna ambavyo wanasaidiana kwa karibu na kushirikiana kwa ajili ya kuhakikisha kwamba, Ofisi ya Waziri Mkuu inatekeleza majukumu yake sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kuanza kumpongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu kwa namna ambavyo anashirikiana vizuri sana na Mheshimiwa Waziri Mkuu katika kuona kwamba shughuli za kimaendeleo, azma na matarajio ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano na wananchi na shughuli za nchi zinakwenda vizuri na kwa ushirikiano mzuri, wote kwa pamoja katika Ofisi ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nichukue nafasi hii kumpongeza kwa namna ya pekee Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa namna ambavyo amekuwa akitekeleza majukumu yake kila siku. Tumeshuhudia ziara zake nyingi za kikazi katika mikoa mbalimbali, lakini kwa wazi kabisa kwa sababu fedha nyingi zimeenda katika halmashauri zetu. Tumekuwa tukishuhudia kwa namna gani ambavyo wamekuwa wakifuatilia suala zima la ukusanyaji wa mapato na matumizi ya fedha za umma. Sote tunajua kwamba katika ngazi za halmashauri ndiko shughuli nyingi zinakofanyika katika sekta zote na ndiko kwenye maeneo ambayo yamekuwa na mianya mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu amekuwa hasiti na amekuwa akichukua hatua kali dhidi ya watumishi ambao wamekuwa wakikiuka taratibu za usimamizi wa fedha na hata ukusanyaji wa fedha za umma. Kwa hiyo tunampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Sisi kama Wabunge tunaendelea kusimama naye na tuna imani naye kubwa sana. Tunamwombea kwa Mwenyezi Mungu amwezeshe ili aendelee kutekeleza majukumu yake sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kumpongeza sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo ameendelea kuleta fedha nyingi katika ngazi za halmashauri kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo katika Sekta za Maji, Afya, Barabara, Miundombinu na mambo mengine mengi. Kwa kweli tumeshuhudia mafanikio makubwa sana katika kipindi kifupi cha miaka mitatu ambapo Serikali hii ya Chama Cha Mapinduzi imekuwa ikifanya kazi kubwa na hasa kwa maendeleo ya wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sote kila Mbunge hapa akisimama anaweza kashuhudia mambo mbalimbali ambayo yamefanyika katika Jimbo lake. Kwa hili tunaomba tumpongeze sana na tumtakie afya njema Mheshimiwa Rais wetu na tutaendelea kumwakilisha, tuna imani kubwa naye na wananchi wetu wana imani kubwa sana na yeye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo jitihada kubwa sana zinazoendelea bila kusimama. Kwa mfano, miradi mikubwa ya kimkakati, Miradi ya *SGR,* Mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere na Daraja la Busisi. Miradi mingi ya kimkakati inakwenda sawasawa, lakini bila kusahau jitihada kubwa anazozifanya katika Sekta ya Umeme (Nishati), kwamba umeme unasambaa vijijini kwa kasi kubwa na jitihada kubwa tunazishuhudia katika Uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita. Kwa hiyo tumpongeze sana Mheshimiwa Rais na kwa kweli tuna imani kwamba baada ya muda mfupi maendeleo yatakayokuwepo katika nchi yetu, yatakuwa ni ya kuigwa kwa Nchi za Afrika, lakini hata katika dunia yetu hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nijielekeze katika eneo la barabara. Sote tunatambua kuna mvua kubwa hapa zimekuwa zinaendelea kunyesha, hizi mvua za *El-Nino*. Uharibifu mkubwa wa barabara umeendelea kuonekana katika maeneo mbalimbali na Waheshimiwa Wabunge wengi hapa wamelalamika. Nitumie fursa hii kuzungumza kwamba, hata katika Wilaya ya Kishapu kuna changamoto kubwa sana ya uharibifu wa barabara. Hii ni kutokana na mvua kubwa hizi ambazo zinaendelea kunyesha ambayo

imesababisha makalavati na madaraja mengi hata barabara kuondolewa kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ninavyozungumza tathmini iliyofanyika muda mfupi ni zaidi ya kilomita 53, zimeharibiwa kabisa katika Wilaya yangu ya Kishapu na hasa katika kata mbalimbali. Hii imepelekea kuandika ombi maalum kwa watu wa *TARURA* watusaidie walau hata bilioni 2.5 kwa ajili ya kuhakikisha tunarudishia miundombinu, kwa sababu zaidi ya kata sita sasa hazina mawasiliano kabisa. Tunaishauri Serikali ifanye jitihada kubwa za kuhakikisha kwamba inarudishia miundombinu hii ili jitihada za kimaendeleo ambazo zinafanywa na wananchi katika kusafirisha mazao na kusafiri wao wenyewe na shughuli ziweze kuendelea sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie upande wa barabara na hasa *TANROADS*. Ipo Barabara ya Kishapu ambayo inatoka Kolandoto inakuja Kishapu kwenda kwa Mwangongo ambapo ni Wilaya ya Maswa, kilomita 63. Barabara hii kwa kipindi kirefu imekuwa ikipangwa katika mpango wa bajeti takribani miaka zaidi ya nane au saba. Sasa ni kitu ambacho hakipendezi hata kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunafahamu Ilani yetu ya Chama Cha Mapinduzi ni mkataba baina ya wananchi na Serikali. Sasa tunayo Ilani yetu ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2015 – 2020, hii Barabara ilikuwemo, ni moja kati ya barabara ambayo haikutekelezwa katika miaka mitano ile. Tumekuja 2020 – 2025, leo tunakwenda mwaka wa nne barabara hii haijatekelezwa japokuwa imo katika mpango wa bajeti mpaka hivi tunavyozungumza. Hili halileti afya kabisa hata kidogo. Tunafanya mambo mengi makubwa lakini katika eneo hili Wanakishapu bado tunakwazwa na eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua Serikali ya CCM ni Serikali Sikivu. Serikali ya CCM inautumia vizuri mkataba baina ya Serikali yake na wananchi na hasa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi.

Kuna wajibu wa Serikali yetu kuhakikisha inatekeleza ujenzi wa barabara hii katika kiwango cha lami. Barabara hii inatumika katika kusafirisha mazao na barabara hii ndiyo inatumika kuwasafirisha wananchi kwenda makao makuu ambapo ni mkoani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ilani tumebainisha kwamba kuna haja ya kuunganisha wilaya na Makao Makuu ya Wilaya na Mawa. Nataka nitoe taarifa, kwa kweli sitasita kushika shilingi katika bajeti ya Wizara hii ambayo inahusiana na ujenzi kuhusiana hili la kutokutekeleza ujenzi wa barabara hii, vinginevyo nipate maelezo ya kina kwa namna gani Serikali imejipanga kulitekeleza hili. Haya ni mambo ambayo yanatakiwa yazingatiwe na pengine tutakwenda kupunguza adha kubwa sana kwa Wananchi wetu wa Kishapu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia jambo lingine nataka nisisitize ni barabara hii inayokwenda kuunganisha Singida, Manyara, Arusha na Simiyu. Kwa hiyo, hii ni *trunk road*. Sasa kwa nini *trunk roads* tunachelewa kuziweka katika utekelezaji? Tunajua kimsingi ndiyo zinakwenda kuharakisha mnyororo mzima wa kiuchumi na maendeleo ya nchi yetu. Ni lazima tuhakikishe kwamba, hili jambo lazima linasimamiwa na linatekelezwa kwa wakati *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka nizungumzie ni kuhusiana na Mpigachapa wa Serikali. Hivi karibuni Serikali imetoa fedha nyingi sana kwa ajili ya kuhakikisha kwamba uchapishaji na udurufu wa nyaraka mbalimbali unaendelea vizuri. Sasa, tumetoa fedha nyingi, lakini kwa bahati mbaya Mpigachapa Mkuu wa Serikali katika eneo hili naona uzingatiaji haupo. Tunajua tuna taasisi za umma nyingi, halmashauri na taasisi nyingine zote, tulishaelekeza kwamba ni lazima wahakikishe wanaitumia vizuri Ofisi ya Mpigachapa Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshuhudia nyaraka nyingi zimekuwa zikizurura mitaani, lakini hata uchapishaji unakiuka taratibu, umekuwa haufuati taratibu. Serikali inaendelea kukosa mapato kwa sababu eneo hili la Mpiga Chapa wa Serikali tuna

matumaini makubwa kwamba, linaendelea kupata mapato makubwa ambayo yangesaidia kukusanya mapato na idara hii ingeweza kujiendesha. Mpaka sasa halmashauri zinaendelea kuchapisha nyaraka zake katika taasisi binafsi, wanaendelea kuchapisha mitaani na tumeshuhudia nyaraka nyingi zikiwa zinatoka nje, zinatapakaa huku na kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba sana kwa Mama Mheshimiwa Jenista Mhagama kwamba, hili jambo lisimamiwe kwa ukaribu, kwa maana ya halmashauri na taasisi zingine zote za umma, zielekezwe kwa ukali na kwa maelekezo ya aina yake kwamba, wakachape nyaraka zao zote kwa Mpiga Chapa wa Serikali. Hii itasaidia sana kuongeza mapato na pengine kudhibiti usiri wa mambo mbalimbali ya Serikali kutoka nje pasipokuwa na utaratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka kuzungumzia ni upande wa jitihada kubwa zinazofanyika katika eneo la Kamishna Jenerali wa Dawa za Kulevya. Jitihada kubwa sana anaifanya, Serikali tumeshuhudia...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Butondo, kengele ya pili.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Emmanuel Shangai, ajiandae Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay.

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu inayohusu bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025. Awali ya yote naipongeza Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuwaletea wananchi maendeleo. Pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na timu yake yote

kwa kuendelea kusimamia Ofisi ya Waziri Mkuu na hatimaye Watanzania kupata maendeleo pamoja na huduma zinazotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nichangie kwenye Jimbo langu la Ngorongoro, tumepata maendeleo katika nyanja mbalimbali. Tumejengewa shule za sekondari; Shule ya Sekondari Ololosokwan, Oldonyosambu, Masusu na Shule ya Msingi Loswashi iliyopo Kata ya Soitsambu. Haya ni maendeleo makubwa kwa manufaa ya Wananchi wa Wilaya ya Ngorongoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika hizi shule, kwa jiografia ya Wilaya ya Ngorongoro wanafunzi hawataweza kunufaika na masomo kwa sababu katika eneo letu kuna wanyama wengi, lakini hatujajenga mabweni na hakuna nyumba za walimu. Kwa hiyo, naiomba Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Wizara zingine zinazohusika waweze kutenga bajeti kwa ajili ya kujenga mabweni pamoja na nyumba za walimu ili sasa wanafunzi waweze kunufaika na huduma nzuri inayotolewa na Serikali yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu ukiangalia Shule ya Sekondari Ololosokwan kutoka Makao Makuu ya Kata, ipo zaidi ya kilometa 10. Kwa hiyo, wanafunzi hawawezi kutembea, labda tukiamua ziwe shule za kutwa, hivyo hivyo Oldonyosambu. Pia kuna shule zingine zimejengwa na wananchi, Shule ya Sekondari Rela iliyopo Kata ya Digodigo na Shule ya Sekondari Jema. Kwa hiyo, naiomba Serikali iweze kututengea bajeti kwa ajili ya wanafunzi hao kuweza kupata huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine, ningependa leo wakati wa kuhitimisha bajeti hii Ofisi ya Waziri Mkuu ingetwambia au ingeniambia au ingewapa wananchi wa Wilaya ya Ngorongoro majibu, kwa wananchi wa Tarafa ya Ngorongoro zaidi ya 108,000 waliobaki baada ya wale wengine 7,000 kuhama kwenda Kijiji cha Msomera. Kutoka mwaka 2022 wananchi hawa wamekuwa *locked down* kwa suala la maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo la Tarafa ya Ngorongoro, kuna shule 27 za msingi, lakini hakuna hata shule moja ambayo sasa hivi wanaruhusiwa angalau hata kujenga au kukarabati choo. Naweza ku-*share* picha za vyoo vya wanafunzi, kila sehemu, wanafunzi pamoja na walimu wanaenda kujisaidia porini, kwa nini tunafanya hili? Kila mwananchi ana haki ya kupata huduma ndani ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, zoezi la kuhama kwa Tarafa ya Ngorongoro ni la hiari. Mheshimiwa Waziri Mkuu alienda kuzungumza na wananchi tarehe 14 Februari, 2022 na alisema ni zoezi la hiari, iweje sasa wananchi tuwawekee vikwazo vya kimaendeleo? Hata huduma za afya zimekuwa hafifu sana. Isitoshe, Shule ya Msingi Endulen ambayo kuna wanafunzi wa bweni, sasa hivi watoto wanaenda kuchota maji mtoni kwa sababu wamesitishiwa huduma ya maji na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, watoto wadogo wa kike na wa kiume wanaenda kuchota maji mtoni kwa sababu wamekatiwa huduma ya maji. Kwa nini tunawawekea wananchi vikwazo? Kama suala ni la hiari kwa nini tuweke vikwazo? Kwa nini tusiwape wananchi huduma ili yule anayeona kwamba maisha ya nje ni mazuri kuliko ya Ngorongoro aende kule kwa hiari lakini siyo kwa kuwawekea vikwazo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba wakati wa kuhitimisha Bajeti hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu na suala hili lenyewe lipo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu atwambie, hawa wananchi ana mpango nao gani? Kwa sababu haiwezekani wananchi wapo miaka mitatu hawapati huduma, huduma za afya zenyewe zimekuwa hafifu. Kwa nini tuwafanyie hivi wananchi? Wamewakosea nini hawa wananchi? Wananchi hawa wapo ndani ya eneo la Hifadhi ya Ngorongoro kwa mujibu wa Sheria ya Mwaka 1959 na sheria hiyo bado inafanya kazi mpaka sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tuna mpango wa kupunguza...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shangai, dakika moja.

Waheshimiwa Wabunge nawaomba, hii ni hoja ya Waziri Mkuu. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge, ili Waziri Mkuu aweze kujibu hizi hoja, mwacheni apokee michango ya Wabunge. *(Makofi)*

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana...

**NAIBU SPIKA:** Msiende kukaa kwenye kiti na kuzungumza na Waziri Mkuu, mnamwondoa kwenye *focus* ya ku-*concentrate* na michango ya Wabunge. Mheshimiwa Shangai endelea. *(Makofi)*

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kwa hiyo, napenda baadaye wakati wanakuja kuhitimisha hoja hii waniambie wana mpango gani na wananchi wanaoishi Tarafa ya Ngorongoro, wananchi zaidi ya 100,000? Isitoshe kwenye geti la Ngorongoro sasa hivi mwananchi akija kufanya huduma zake Karatu ili arudi anazuiliwa asirudi nyumbani. Anaambiwa alete Kitambulisho cha Mpiga Kura, wengine ndiyo wamefikisha miaka 18, hawana hivyo vitambulisho. Anaambiwa nenda polisi, leta *loss report* na mwananchi hana fedha za kulala Karatu. Kwa nini tunawafanyia hivi?

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine wanaofanya biashara ya mifugo tunawazuia wasifanye. Sasa hivi akitoka Mang'ola akitaka kwenda Mnada wa Endulen wanawazuia, wanataka wabebe ng'ombe kwa kutumia lori na hakuna barabara ya kupitisha. Sasa, kwa nini tunawafanyia hivi wananchi wetu? Wananchi hawa siyo wakimbizi, ni wananchi ambao walikuwepo. Umefika wakati ni bora wawaambie hawatakiwi kuwepo katika eneo la Tarafa ya Ngorongoro badala ya kuwapa mateso.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine, leo kulikuwa na mradi wa elimu ambao wanafunzi walikuwa wanasomeshwa vyuo vikuu, vyuo vya kati pamoja na shule za sekondari. Wanafunzi 154 ambao walipitishwa na Baraza la Wafugaji wa vyuo vya kati na vyuo vikuu

wamesitishiwa ufadhili. Watoto wa kike wanaenda kujiuza kwa ajili ya kupata chochote, kwa nini tunawafanyia haya hawa watoto wetu? Mheshimiwa Waziri Mkuu, najua ndiye alikuja kuomba kura Ngorongoro mwaka 2020, aliwahakikishia hawa wananchi kwamba watapewa huduma na watasaidiwa kama wananchi wengine wa Tanzania. Kwa nini sasa tunawafanyia hivyo? Nataka leo Waziri Mkuu akija hapa, kama kuna Mbunge amewahi kushika shilingi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, leo mimi nitashika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Rais anawaapisha viongozi pamoja na Wakuu wa Mikoa alisisitiza kwamba kila kiongozi ni lazima atende haki kwa wananchi katika maeneo wanayowahudumia, lakini pia kuondoa migogoro katika maeneo yale. Kinachoshangaza, sisi Wilaya ya Ngorongoro kwa wiki tano sasa kumekuwa na migogoro inayosababishwa na Mkuu wa Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, amefika wilayani kwetu amewakuta wananchi wana utaratibu wao wa kujiokotea na kupata mapato yao kwenye vibanda vilivyopo pembeni mwa barabara, amewaagiza wananchi kuvunja vibanda vyao, akinamama ntile wamevunjiwa vibanda, akinamama wana mikopo kwenye *VICOBA*, wengine wanayo kwenye benki, lakini mpaka leo wananchi hao wanalia kwa sababu hawana chochote, wamefilisika, hawana chochote kwa ajili ya kuhudumia familia zao. Kwa nini haya yanatokea? Mtu ukimuuliza anasema mimi sikutumwa kufanya siasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine, mnada wa juzi Ijumaa wananchi wamegoma kupeleka mifugo kwa sababu wamefika wanataka ku-*forge* mapato ya halmashauri, wamepandisha ushuru kwa mbuzi kutoka shilingi 2,500 mpaka shilingi 8,000 na Baraza la Madiwani halijui, Mwenyekiti wa Halmashauri hajui, Mkurugenzi hajui na wanatumia wanajeshi kukusanya ushuru. Kwa nini hili linatokea Ngorongoro tu? Kwa nini wananchi wanafanyiwa haya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mwananchi ana haki ya kulipa ushuru kwa maendeleo ya nchi lakini Mheshimiwa Rais alikataza kukusanya ushuru au kodi kwa kutumia mitutu ya bunduki. Mpaka

maeneo mengine sasa hivi kumetulia na Serikali inakusanya mapato, kwa nini *DC* huyu aendelee kutumia mabavu na kuwaumiza wananchi? Nimshauri Mheshimiwa Waziri Mkuu, wananchi waruhusiwe kufanya biashara zao kwa uhuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano kutoka mnadani, Mheshimiwa Waziri Mkuu anajua, Uwanja wa Waziri Mkuu Loliondo, wananchi wanatoka kule chini unapoingilia Loliondo ndiyo kuna mnada wa mifugo na wananchi wanatakiwa kuwa na biashara ya mifugo pale pamoja na bidhaa zingine, lakini amefika ametenganisha minada yote miwili...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Shangai, kengele ya pili hiyo.

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba wananchi waruhusiwe wafanye biashara kwa uhuru waache bugudha. Nashukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, unaweza kumwandikia barua.

Tunaendelea, Mheshimiwa Zacharia, ajiandae Mheshimiwa Kyombo.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema aliyetujalia wakati huu na nafasi hii kwa rehema zake zote. Pia, nachukua nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais na Serikali nzima kwa kazi kubwa inayofanyika nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nachukua nafasi hii kumshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Wizara zote, idara zote zilizoko chini yake na Kamati zetu nne za Bunge kwa taarifa yao waliyoiwasilisha hivi punde. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza nachukua nafasi hii kuishukuru Ofisi ya Waziri Mkuu na Idara zilizo chini yake kwa ujenzi wa Mahakama kule Mbulu na Jengo la *PCCB*, miradi ambayo tumeiweka kwenye mpango wa bajeti na hivi sasa utekelezaji wake unaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kuzungumzia suala hili la utoaji wa fedha, mtiririko wetu wa fedha siyo mzuri. Nimeipitia Taarifa ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kitengo cha Vijana tulitarajia kupeleka shilingi bilioni tatu lakini hatujapeleka hata shilingi kwenye eneo hilo la maendeleo ya vijana, hasa makundi ya walemavu na eneo la ujenzi au ukarabati na ujenzi wa vituo vya mafunzo kwa maendeleo ya vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tuendelee kuishauri Serikali, tunapitisha hizi bajeti hapa ndani, lakini baadaye tunakwenda kuwaambia wananchi kwamba katika mwaka huu wa fedha tumepitisha au tumepata mpango wa kufanya mambo kadhaa. Pale ambapo fedha zinakosekana tunapata wakati mgumu sana. Fedha hizi za maendeleo zinakuwa na athari kubwa kwa sisi viongozi, hasa Wabunge kwa sababu tunapofanya vikao tunarudisha mrejesho wa bajeti kwa wananchi tunaowaongoza na fedha zinapokosekana na hasahasa zile fedha za miradi, hali inakuwa mbaya sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali ijitahidi sana kupeleka fedha kwa yale maeneo ambayo tumeshaomba fedha, tumepitisha kwenye bajeti na lengo letu ni kwenda kutoa huduma kwa wananchi. Utoaji huu wa fedha unaathiri sana Sekta za Barabara, Maji, Elimu na Afya. Asubuhi niliuliza swali la maji lakini nilijibiwa kwa namna ambayo sikuridhika kidogo kwa sababu, majibu yale ya kuomba tupate fedha za miradi na tutekeleze miradi, kwa mfano, unapochimba visima miaka mitatu au miaka miwili, hujajenga matenki, hujajenga mabomba, hujapeleka huduma kwa wananchi, lazima wananchi wanasubiri kwa hamu kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii imetuathiri sana na hasahasa Wizara ya Ujenzi, tunaomba Mheshimiwa Mwigulu atusikilize sana. Wizara ya Ujenzi tulianza kujenga barabara kule Mbulu kwenda Haydom, kwa maana ya Mbulu – Garbabi kilometa 25. Sasa hivi katika kilometa 25, ndani ya miaka miwili hatuna hata kilometa moja iliyowekwa lami. Kwa hali kama hii tunakwenda wapi? Barabara ya kilometa 25 kama itachukua miaka mitano, je, Barabara ya Karatu – Mbulu – Haydom na hatimaye Sibiti, itachukua miaka mingapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali, nia yetu hapa ni kwamba tupeleke huduma kwa wananchi, mkandarasi yule ameshaondoka. Wizara ya Ujenzi na Wizara ya Fedha wakae chini wamrudishe yule mkandarasi amalize kilometa 25 ya Mbulu – Garbabi. Mkataba tuliousaini mwaka jana mwezi Juni wa Karatu – Mbulu - Haydom kupitia *EPC+ Finance*, waanze mara moja kabla ya Kura ya Bajeti ya Bunge hili. Vinginevyo hatutaelewana kwa sababu tayari wananchi walipokea kwa hamu kubwa, kwa bashasha na furaha tele wakitegemea ile barabara inajengwa. Sasa hivi kila saa wanatuuliza hiyo barabara itaanza lini kujengwa, hakuna hata kinachoeleweka. Miradi ile tuliyosaini Jakaya Kikwete ya barabara kama saba, hakuna hata barabara moja iliyoanza mpaka leo na hali hii ni mbaya kwa sababu tumeahidi, tukasaini tena hadharani, lakini mpaka sasa hivi hakuna utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimelizungumza eneo hili kwa sababu changamoto kubwa ukiulizwa ni fedha na kama tuna bajeti ya shilingi trilioni 43 halafu hatujatekeleza pengine kama kwa 70% au 80%, mwisho wa siku kwa wananchi tunaonekana tunajifurahisha na kupanga bajeti kubwa ya nchi, lakini mafanikio ni machache.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kwamba, angalau kwenye vipaumbele tuone. Hata kazi zianze kwa awamu, hata kama hatutaweza kilometa 389, basi tuanze hata sehemu inayowezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee na eneo lingine la pensheni kwa wastaafu...

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa kuna taarifa.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kumpongeza mchangiaji kwa hoja nzuri anazozitoa, lakini napenda kumpa taarifa kwa kumhakikishia kwamba, barabara hizo ambazo tulizisaini, hatujasaini na kuziacha na kazi hiyo itaanza mara moja. Kuna masuala ya kitaalam yalikuwa yanaendelea baada ya wakandarasi kupewa mradi. Kuna masuala ya ku-*design* pamoja na *mobilization* kulingana na ukubwa wa miradi ambayo inatekelezwa kwa sababu ni miradi mikubwa mno. Kwa hiyo, hivi tunavyoongea sasa hivi tuko hatua za mwisho kuwapatia malipo ya awali na kazi itakwenda kuanza mara moja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Zacharia.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampenda sana Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, Mheshimiwa Waziri ni rafiki yangu sana. Kwa kweli Juni mwaka jana, kesho ni Juni mwaka huu. Garbabi ni miaka miwili, Labay - Haydom ni miaka miwili. Hii kwa dalili ya wazi kwa wananchi, hawatakuwa na imani kabisa kwetu sisi wawakilishi wa wananchi kwa kadri ambavyo tunatendewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, amezungumza hivi punde; Juni tunapiga kura, isiwe ajabu kusema hapana kwenye kura hizi kwa sababu tunaingia kwenye ajali za kisiasa. Mimi siipokei taarifa yake kwa kweli, nitaipokea siku ya kupiga kura kwenye bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee na eneo la wastaafu, katika hili nitazungumzia maeneo mawili. Moja, ni pensheni ya kila mwezi, pensheni ya kila mwezi kwa wastaafu wetu hasa wale wenye mishahara midogo, imekuwa ndogo sana kiasi kwamba hata hawawezi kupata bima ya afya, yaani kiasi kwamba hali yao ya afya inadorora. Fedha tunazowalipa kwa mwezi ni ndogo, Serikali itazame upya viwango tunavyolipa. Serikali iongeze angalau kwa sehemu na wao waweze kumudu maisha yao na kuweza kuhudumiwa na Taifa hili kwa kadri hali ya maisha yao inavyozidi kuwa mbaya na kadri umri unavyokwenda wanapata majanga mengi, majanga ya afya na majanga ya kupoteza nguvu kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la kikokotoo; nampongeza sana Mheshimiwa Gambo na Wabunge wengine waliochangia naungana nao. Serikali yetu iwe Sikivu, waje na hoja. Mheshimiwa Waziri Mkuu tunampenda sana, tunamwamini sana, ofisi yake ilitazame upya. Tunampenda Mheshimiwa Rais, hayuko huko na hata Mheshimiwa Waziri Mkuu ni msikivu sana. Suala hili twendeni kwa wafanyakazi tuwasikilize, wafanyakazi wanasononeka, kila unayekutana naye salamu atakayokuanzishia ni hiyo ya kikokotoo. Kwa kuwa Serikali ni sikivu, sisi Bunge ni sikivu, tusichongeane mpaka kufikia hali ya watumishi wetu kutokuwa na imani nasi na sisi kutokuwa na sura nzuri kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili linazungumzika, Mheshimiwa Waziri Mkuu ni kiongozi wetu tunampenda sana, tunamheshimu na anatujali, anatutembelea kwenye majimbo. Watumishi wote kuanzia sisi mpaka wale watumishi wengine wote wako chini ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, tulitazame jambo hili upya kama Serikali, tuwe na nia ya staha, tuanzishe *forum* ya kuzungumza na vyama vyao na sisi tuje tuzungumzie jambo hili. Kama tukienda kwenye kijiji hakuna mzee wa miaka 70, wazee wote wa miaka 70 au 80 wamesharudisha namba, sisi huko tunapokwenda tunaenda na lawama kwa sababu wao wanalalamika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli Wabunge tukianza kufikiri jambo hili ni la watu wa upinzani siyo kweli, jambo hili ni letu, tulilipitisha sisi wenyewe hapa tukiwa ni Bunge lenye Wabunge wengi wa CCM. Jambo hili linatuhitaji tulirudie upya, tujadili jambo hili upya na lije mbele yetu kwa nia ya kukaa meza moja na watumishi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo nataka kulizungumzia ni kwamba, wakati fulani tunapokwenda kujadili hoja ya vijana tuweke vipaumbele kwenye viashiria tulivyopitisha kwenye bajeti. Vijana wengi wanasubiri hali ya mazingira yao kuwa nzuri ili kuweza kumudu kuishi duniani kwa sababu ajira sasa hivi imekuwa ngumu. Fursa hizi za fedha za Ofisi ya Waziri Mkuu tuziongeze na fedha za miradi ya vijana tuziongeze. Tuone jinsi ya kuwatafutia vijana wale madirisha ambayo baadaye wataona Serikali imewajali. Changamoto ya ukosefu wa ajira ni dunia nzima wala siyo Tanzania na kwa sababu hiyo, basi kila nchi inapambana na hali yake kuona kwamba watumishi wake na vijana wake wanapataje ajira au namna ya wao kujiajiri na kufanya kazi. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Issaay kengele ya pili hiyo.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, ajiandae Mheshimiwa Asya Sharif Omar.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa nafasi ya kuchangia bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwanza kabisa nimshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan na tunaona pongezi hizi zinakwenda kwa sababu taarifa iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, inaonesha dhahiri

kwamba Mheshimiwa Rais wetu amedhamiria na ni mbeba maono wa nchi yetu na anamaanisha anachokisema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mahususi nimpongeze sana Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wetu ambaye amekuwa ni mchapakazi, lakini pia ni mfuatiliaji katika kila kona na tunaona taarifa yake imesheheni utumishi uliotukuka na chini yake kwa kweli kuna wasaidizi wake bila kuwataja hao nitakuwa sijamtendea haki Mheshimiwa Jenista Mhagama, kazi ni nzuri sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu, ameongezewa jembe lingine ndugu yetu Mheshimiwa Deogratius Ndejembi, tunaamini katika kumsaidia Mheshimiwa Waziri Mkuu, atafanya kazi vizuri. Pia Manaibu Waziri, dada yetu Mheshimiwa Nderiananga na ndugu yangu Mheshimiwa Patrobass Katambi na Makatibu Wakuu wote, kazi nzuri inafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaangalia katika eneo la utawala wa sheria, ambalo katika taarifa ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, limeelezwa kuanzia ukurasa wa 24. Tunaona Serikali imeboresha kabisa Mahakama zetu, tumejengewa vituo jumuishi vya kisheria, vituo jumuishi vya haki, lakini tunaona Mahakama za Rufaa za Mikoa, Mahakama za Wilaya na Mwanzo zinaendelea kuboreshwa. Pia tunaona *Mobile Courts* zipo katika maeneo ambayo hayafikiki kirahisi na hii yote ni maazimio ya Mheshimiwa Rais, kuhakikisha wananchi wetu wanapata haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la utawala wa sheria tunaona Serikali inaendelea kuboresha mifumo ya Mahakama, tunaona sasa hivi tunatumia akili mnemba kuhakikisha kwamba kesi zinazoendeshwa Mahakamani, hukumu zinavyotolewa zinatolewa kwa wakati kwa kuwa katika mfumo huo, mara baada ya kusikiliza kesi, taarifa inatolewa pale pale na mwananchi anapata haki yake ya kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo hili nishauri zile taasisi zote ambazo zinaendana na utendaji kazi wa Mahakama, nikimaanisha Ofisi ya Mashtaka ya Taifa na Ofisi ya Wakili Mkuu wa

Serikali, basi na zenyewe pamoja na kwamba zinaendelea kufanya kazi nzuri, ziendelee kuboreshewa bajeti zake, ziendelee kuwezeshwa ili kuweza kuboresha miundombinu ya TEHAMA. Pia ziweze kufungua na kuanzisha ofisi katika maeneo ambapo hawajafika, lakini ziendelee kuongezewa watumishi ili ziweze kufanya kazi vizuri. Naamini katika muunganiko huo, basi mtiririko wote wa kisheria na haki za wananchi utakuwa umekamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala langu la pili nitaenda kwenye Sekta ya Uzalishaji, ambalo katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ameielezea kuanzia ukurasa wa 26 na kuendelea. Niipongeze Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwawezesha wakulima kupata mbegu bora, mbolea, zana bora za kilimo na za kisasa na upatikanaji wa masoko ya ndani na nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Mkoa wa Kagera nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipoishukuru Serikali na utendaji kazi wa Mheshimiwa Waziri Mkuu, ambapo walifuta tozo zile ambazo zilikuwa ni kero kwenye zao la kahawa. Leo wananchi wetu wanaweza kuuza mazao ya kahawa kwa ushindani na kupata bei ambayo ina nafuu kwa mkulima. Katika suala hili tunapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la sekta ya uzalishaji, naomba niishauri Serikali. Ni miaka takribani 10 sasa toka wananchi wa Mkoa wa Kagera waanze kulima zao la *vanila*. Zao hili limesaidia hasa katika kuongeza thamani ya mashamba yetu ya ndizi ambapo migomba ilikumbwa na ugonjwa mnyauko, lakini baada ya kuingiza zao la *vanila,* ukichanganya na zao la Kahawa tumeanza kupata angalau kipato na kumwinua mwananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nisikitike kusema kwamba Serikali imekuwa kimya katika eneo hili na ukiangalia katika miaka iliyopita zao hili lilianza likiwa na bei nzuri kwa kilo ya *vanila*. Tulianza kuuza kwa shilingi 120,000 mpaka shilingi 200,000, ikashuka ikaja shilingi 30,000 ikashuka mpaka shilingi 15,000, leo tunavyoongelea zao la vanila ni shilingi 2,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, naangalia hapa kwa nini Serikali imekaa kimya katika eneo hili, lakini katika eneo hili natambua uwezo wa Mheshimiwa Waziri wetu wa Kilimo, Mheshimiwa Bashe, *comrade* wakati yupo *backbencher* tulimtambua kama *champion* wa kilimo. Ni kweli akaenda akawa Naibu Waziri na akawa Waziri na mpaka leo anafanya kazi vizuri, lakini kwenye zao letu la *vanila* bado Mheshimiwa Waziri amekaa kimya. Kwa imani tuliyonayo naamini ukimya wake atakuja na mkakati wa kishindo kwa zao hili la *vanila*. Mheshimiwa Waziri Mkuu, kama Mtendaji Mkuu wa Serikali, lakini pia mlezi wa Mkoa wa Kagera. Kama ni mlezi, tunatamani aje na neno ambalo atasema juu ya *vanila* za Mkoa wa Kagera. Tunapotaka kujikwamua kiuchumi ni kwa sababu *GDP* ya Mkoa wa Kagera tunasema imeshuka na Kagera ni ya mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo wakati wananchi wanaleta zao ambalo linaweza kuwainua kiuchumi, lakini Serikali inakaa kimya. Siamini katika Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambayo imefanya mambo mengi, mazito na mazuri kwa Wanakagera, leo katika suala hili naamini Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, haiwezi kula ng'ombe mzima ikashindwa mkia. Kwa hiyo, niombe sana kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika eneo hili kama Wanakagera wanataka kuona mkakati mahususi ambao una-*reflection* katika bajeti, ni zao letu la *vanila* katika maeneo manne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kwanza, zao hilo litambulike; suala la pili, kutafuta soko la uhakika la ndani na nje; suala la tatu, kuliwekea zao hilo mkakati na mfumo maalum wa kuwa na Bodi kama mazao mengine na hii inawezekana; lakini suala la nne, tupate elimu ya jinsi gani ya kukausha zao hilo ili unapofika wakati wa kuvuna, mkulima asivune hilo zao na kuliuza hapo hapo, akiogopa zao hilo lisioze bali aweze kulitunza na kuliuza pale ambapo bei itakuwa nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, niupongeze uongozi wa Mkoa wa Kagera chini ya Mheshimiwa Hajati Fatuma Mwasa na Mheshimiwa Mkuu wetu wa Wilaya Kanali Hamisi Maiga lakini na Mkurugenzi wetu wa Halmashauri *Advocate* Paul Wanga na wasaidizi wake,

pamoja nami kama mwakilishi wa wananchi na Waheshimiwa Madiwani, tumekuwa tukishirikiana bega kwa bega na wakulima, lakini inafika sehemu sasa tunazidiwa na tunaanza kukata tamaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, siamini kama Serikali inaweza ikashindwa kuleta mkakati wa zao la *vanila* ambalo linainua uchumi wa Wanakagera, linainua uchumi wa Wanamisenyi na katika kata zote zao linastawi vizuri, *research* tumeshafanya imeshatosha. Kwa hiyo niombe sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, wakati anakuja kuhitimisha hapa atuambie Wanakagera zao letu la *vanila* wanaliimarisha vipi katika haya maeneo manne niliyotaja ya masoko, ya mfumo wa kuweka Bodi, ya teknolojia lakini pia tulitambue na kuhakikisha kwamba zao hilo sasa linakuwa mkombozi kwa Wanakagera.

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo wanunuzi wachache wachache ambao wananunua mazao hayo, lakini inaonekana wameelemewa kwa sababu nao katika soko la dunia, wapo kama Tanzania, hawaoni kama kule nje tuna soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la tatu, nitaongelea kwenye maliasili, ambalo imeelezewa vizuri katika ukurasa wa 34 wa taarifa ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nipongeze juhudi za Mheshimiwa Rais, ambaye yeye kwa utashi wake na uzalendo wa nchi yetu kupitia *Royal Tour* na kupitia *Amazing Tanzania* alileta matokeo chanya katika Sekta ya Utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaona leo katika taarifa ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, leo watalii wameongezeka kutoka milioni 1.4 mpaka milioni 1.8, ambalo ni ongezeko la asilimia 8.4. Ni suala la kushukuru na kupongeza Serikali yetu, lakini tunaona mapato yanayotokana na maliasili na utalii yameongezeka kutoka bilioni 2.5 *USD* kwenda bilioni 3.37, ongezeko la 33.3%. Wakati Mheshimiwa Rais anarekodi hii rekodi ya *Royal Tour* alikuwa katika mbuga ambazo zina *risk* kubwa, lakini kwa sababu ya uzalendo na upendo kwa nchi yake aliona afanye hiyo kazi yeye mwenyewe ili iweze kuleta *impact*

ambayo leo tunaiona. Tumpongeze Mheshimiwa Rais kwa uzalendo na utashi na maono yake kuyasimamia kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaona wanyama wameongezeka, wamezaliana kwa sababu ya usimamizi mzuri na ndiyo maana tunaendelea kupata watalii na mapato. Katika eneo hili, niombe pamoja na uzalishaji mwingi na mapenzi mema ya nchi yetu kwa wananchi, tunaona ongezeko la wanyama sasa, wanatoka katika mbuga wanakuja katika makazi ya wananchi. Leo katika Wilaya ya Missenyi tuna uvamizi mkubwa wa tembo katika maeneo ya Missenyi *Ranch* pamoja na wananchi wa Mabale wote na hata kilimo kimesimama.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiangalia wanaharibu mali za wananchi, hawawezi kuvuna mazao, lakini pia wananchi wanajeruhiwa, pia tunaona miundombinu yote inayojengwa kwa mfano katika *Ranch* za Missenyi na Mabale masharti ya Wizara ya Mifugo inataka uendeleze kitalu chako, ujenge miundombinu, uweke mabwawa ya maji, ujenge nyumba, lakini sasa tembo akija anaharibu vyote, huku unasimamiwa kwamba hujatekeleza masharti ya upangaji, lakini huku tembo bado wanaendelea kukaa katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru juhudi za Mheshimiwa Angellah Kairuki, ameshatuita, naomba sasa mkakati uje kwenye *reflection* ya bajeti…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kyombo kengele ya pili hiyo, ahsante.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asya Sharifu Omar, wajiandae Mheshimiwa Esther Matiko na Mheshimiwa Mariam Nyoka.

**MHE. ASYA SHARIF OMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi asubuhi hii ya leo ya kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema mpaka nikaweza kusimama katika Bunge letu hili Tukufu ili kuchangia. Nianze kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa juhudi zake mbalimbali anazozifanya katika kulitumikia Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna asiyeona, hakuna asiyejua namna mama anavyoupiga mwingi katika kulitumikia Taifa letu. Nikwambie kwamba sisi majeshi ya Mama Samia tutaendelea kuona jitihada zake, lakini tutaendelea kukijenga Chama chetu Cha Mapinduzi ambacho kinaongozwa na Jemedari wetu, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa. Pia niwapongeze Naibu Waziri Mkuu Mheshimiwa Biteko na dada yangu Mheshimiwa Jenista Mhagama. Nitakuwa mwizi wa fadhila kama sikumpongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Spika wetu Mama Tulia, kwa kweli Spika wetu anatulea vizuri, anatujenga vizuri hadi leo tumeweza kusimama kwa sababu anatuvumilia na anatuongoza, tusingeweza kusimama leo kuchangia hoja hii bila malezi yake Mama Tulia. Nimwambie Mama Tulia, ana vijana wazuri, lakini ana wanawake ambao wanajiamini, ambao wamelelewa na wamefunzika. Tutaendelea kusemea Serikali yetu inayoongozwa na Mama Samia kwa yale mazuri, sababu tunazo, vigezo vipo na uwezo upo kwa nchi inayoongozwa na Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nianze kuchangia hoja yangu kwa kuzungumzia suala la ukatili wa kijinsia ambao unawagusa jinsia zote, wakiwemo watoto wa kike na kiume lakini pia sisi wanawake, lakini vikongwe vilivyokuwa havina hatia. Tumeguswa sana na jambo hili. Kwa hiyo nimeona nilichangie hili kutokana na wimbi kubwa la ukatili unaoendelea siku hadi siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu Serikali yetu namna inavyoendelea kupambana na haipendezwi na vitendo hivi vinavyofanywa na wachache ambao wanajifanya wamejizima *data*, jambo hili halikubaliki, kwa sababu Taifa limekuwa likiongeza nguvu kubwa kuwekeza katika suala la afya ya watoto hawa, suala la uchumi na suala la kuhakikisha wasome lakini waweze kuimarika. Sasa kama wanajitokeza wachache wanaojizima *data* na kuwafanyia ulawiti watoto, haiwezekani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na wimbi la watoto ambao wapo shuleni na nje ya shule wanafanyiwa ulawiti pasipo na hatia yoyote, watoto hawa wamekosa raha na baadhi ya walimu wanahusika, jambo hili halileti afya. Tunafahamu ipo sheria ambayo inawabana, lakini imeonekana imezoeleka. Kwa hiyo sasa, niiombe Serikali ione haja ya kuibadilisha sheria hii na kuwekea adhabu ya kuwahasi hawa wote ambao wanafanya vitendo hivi kwa makusudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, matukio haya ni mengi sana na kwa kweli Watanzania yanatuumiza tukiwemo wanawake, tunashuhudia vitoto vichanga vinatiwa kwenye maji, vinabakwa na vinachinjwa, hatujui kwa nini. Tunakwenda wapi? Jamani tumuogopeni Mwenyezi Mungu. Watoto leo wamekuwa hawana haki ya kucheza, hawana haki ya kusoma, hawana uhuru wa aina yoyote wakati Taifa hili linategemea hawa watoto baadaye ndiyo waje wawe viongozi wa nchi hii. Sasa ikiwa leo kuna wachache ambao wanajizima *data*, wanawaharibu na kuwafanyia ukatili watoto wetu, huu ni unyama wa kiasi gani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema haya kwa machungu makubwa kama mwanamke, kama mama, kama mzazi, inauma, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anapambana usiku na mchana, tukijipima sisi na yeye, bora sisi tunapumzika, tunakaa kuliko yeye anavyohangaika kututafutia maisha bora, inakuwaje wanatokea watu wachache wanatuvuruga akili zetu kwa kuwaharibu hawa watoto. Niiombe sana Serikali, sheria ifanyiwe mabadiliko ili vitendo hivi vikome. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo haya ni mengi na ni makubwa yanayohusiana na udhalilishaji wa kijinsia, wanawake, watoto wa kike na kiume, nimeshayaeleza hapo juu. Naamini Serikali yangu Tukufu na kwa kuwa ni Serikali Sikivu, itayafanyia kazi ili kuweka dira ambayo italeta manufaa kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niondoke kwenye udhalilishaji niingie kidogo kwenye suala la maji, kwa sababu suala la maji linatugusa na ni suala la kila siku. Katika suala hili la maji nizungumzie Sera ya Maji. Hii lengo lake ikifika 2025, mijini ifikie 95%, lakini vijijini 85%. Suala hili ni kubwa na tunaipongeza sana Wizara hii ya Maji inayosimamiwa na kaka yetu Mheshimiwa Jumaa Aweso, jitihada za Serikali tunaziona, lakini bado kuna maboresho kidogo yanatakiwa yafanyiwe kazi kwa faida ya kuleta manufaa ya upatikanaji wa maji kwa wananchi wa Tanzania kwa sababu ni kitu tunachokitegemea kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo yenyewe ambayo tunatarajia yaweze kuleta ufanisi ni kwamba, pale inapotekelezwa miradi ya maji kwenye maeneo husika, washirikishwe wahusika ambao ni wananchi wa pale. Jambo hili litaleta afya, kwa sababu inapokwenda miradi kama wanajamii hawashirikishwi inaleta manung'uniko na tija ya Serikali itakuwa haipatikani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndoto ya Mama Samia ni kubwa katika kumtua mama ndoo kichwani. Tuseme ukweli, tunamshukuru sana Mama Samia, ameweza kututua ndoo kichwani wanawake, lakini ametoa fursa ya kujinyanyua kiuchumi kwa sababu wanawake tulikuwa tunapoteza muda mwingi kwenda kuchota maji, lakini leo tunakwenda kilomita kidogo tunapata maji, tunakwenda kufanya shughuli za kimaendeleo, tukishirikiana na wenza wetu. Namwambia Mama Samia, ahsante, chukua maua yako. Tutaendelea kumuunga mkono, Mama Samia anatosha, vigezo anavyo na kimojawapo ni hicho cha kutuondoa wanawake katika vita ya maji na kutuwezesha kuwa na uchumi mzuri, tunataka nini Watanzania? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maji ndiyo kila kitu, lakini Serikali inapopeleka miradi katika maeneo ya wananchi, kuna vyanzo vya maji ambavyo vingine havizingatii kuweka maeneo ya malisho kwa wafugaji, jambo linalopelekea vyanzo hivyo kuharibiwa wakati Serikali tayari imeshawekeza pesa nyingi pale. Sasa ikiwa maji yatachafuliwa, wananchi watapata afya isiyokuwa bora. Sasa, niiombe sana Wizara ya Maji, wakati wanaweka vyanzo vya maji, basi yatengwe maeneo maalum ya malisho ya wale wafugaji ili kusiwe na manung'uniko, wakaiona Serikali yao ni mbaya wakati Serikali inayoongozwa na Mama Samia ni nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, niseme naunga mkono hoja na nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Esther Matiko, halafu wajiandae Mheshimiwa Mariam Nyoka na Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq. *(Makofi)*

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia fursa nami niweze kuchangia kwenye bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa maeneo mawili, kwanza ni kwa kudumisha demokrasia na kuimarisha demokrasia nchini. Sasa hivi tunaona hata sisi wapinzani tunafanya mikutano ya ndani, tunafanya mikutano ya hadhara, tunafanya maandamano kwa amani ukilinganisha na miaka iliyopita ambapo tulikuwa hatuwezi kufanya mikutano ya ndani, hatuwezi kuandamana, sana sana tunaishia gerezani, nami mwenyewe nimeshawahi kuwa mhanga kwa hili. Pia kuna uhuru wa Mtanzania kutoa maoni yake na kuweza hata kuweza kui-*criticize the government* lakini pia uhuru wa vyombo vya habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ninampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuimarisha diplomasia ya uchumi na mahusiano baina ya Mataifa mbalimbali duniani. Hii imeongeza idadi ya wawekezaji nchini, na pia mahusiano haya chanya yameweza kudhihiri. Kwa mfano, tulipokuwa tunafanya uchaguzi na Mheshimiwa Spika wetu alikuwa anagombea Urais wa Umoja wa Mabunge ya Dunia, kwa

kweli tulikuwa tunapata ushirikiano mzuri sana kwa Mataifa mbalimbali na ndiyo maana hata tukaweza kuibuka. Hii yote imechagizwa na jinsi mama anavyoji-*position* na Mataifa haya ukilinganisha na huko nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mazuri haya yote na dhamira ya dhati ya mama ambayo tunaiona katika kuhakikisha anakuwa na utawala bora, lakini kuna changamoto nyingi ambazo zinafanyika ambazo zinatokana na watendaji ambao wapo katika Serikali na wasaidizi wa mama, na ninaenda kuainisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, alikuwa na ziara Mkoa wa Mara kuanzia tarehe 24 mpaka tarehe 29, alishuhudia kero mbalimbali, lakini kwa masikitiko, baadhi ya hizo kero zimeendelea hata baada ya ziara yake. Nitazungumzia madhila ambayo tunayapata wananchi ambao tunazunguka Mbuga ya Serengeti. Wananchi wanaozunguka Mbuga ya Serengeti wanapatwa na madhila mbalimbali ikiwemo ya mauji, kulemazwa, kutaifishiwa mifugo yao, mifugo yao kupigwa risasi na vitu vingine vingi, wanawake wanabakwa wakienda kukusanya kuni kwenye hifadhi na mambo mengine mengi, mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeandaa nakala ya *evidence* kwa ambayo nitayaongelea hapa na nitayaweka hapo Mezani. Kulikuwa na matukio mbalimbali; tukio la kwanza ambalo nitarejea kwa machache yake tu ni ambalo limetokea *recently* baada ya kuondoka Mheshimiwa Waziri Mkuu. Tarehe 11 Machi kule Serengeti Kitongoji ya Jerumani, Kijiji cha Machochwe, Askari watano wa *SENAPA* walikwenda nyumbani kwa ndugu yetu Julius Nyaisuka Muhono mwenye miaka 21 tu, saa 3.30 asubuhi wakafika pale na kumtuhumu kwamba alikuwa anaenda kuchunga hifadhini, wakataka kuswaga ng'ombe. Hili limekuwa likiendelea miaka yote, ninalizungumzia hapa. Wanaenda wanaswaga ng'ombe kutoka maeneo fulani wanapeleka hifadhini. Yule kija alivyo-*resist* wakampiga risasi na kumpakia na kuondoka naye.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasemekana wananchi waka-*riot* na alifika pale Afisa Tarafa na akampigia simu *DC* na wengine wakafika eneo la tukio, wakakiri kuona damu, maganda ya risasi, matairi ya gari, miwani ya wale askari na wananchi, wakawatambua hao Maaskari. Huyu kijana mpaka tunavyoongea hajapatikana akiwa hai wala akiwa amekufa ili wamrudishe tuweze kumhifadhi kwa mila na desturi za Wakurya. Hilo limetokea tarehe 21 Machi mwaka huu 2024. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tukio lingine ambalo lilitokea Agosti mwaka 2023, kijana Julius Mwita Mmali wa Kijiji cha Kenyamsabo kule Gorong'a Tarime Vijijini akiwa anachunga, alikamatwa, wananchi wakashuhudia amekamatwa na gari la wahifadhi wakaondoka naye. Mama yake Maseke akafuatilia kwenye Kambi hii ya Kenyanganga akaambiwa kama unamtaka kijana wako toa fedha. Akasema ana shilingi 400,000/= wakamwambia ondoka, tupo na kijana wako. Walivyofuatilia mara ya pili, *documentary* ipo mnaweza mkafuatilia katika kufanya uchunguzi, walifuatilia mara ya pili wakasema hawana huyo kijana, hawajamwona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka tunavyoongea leo, hatujui huyu Julius yupo wapi? Kaacha mke, ndio wameoana tu, wana mwaka. Huyu ndio kijana pekee kwenye familia, ndio alikuwa kijana tegemezi. Haya yanaondoa na ku-*tarnish the government*. Tunataka uhai wa watu wanaoishi…

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hizi mbuga, huwezi ukathamini mbuga *vis-a-vis* uhai wa binadamu ambao wanazunguka hizi mbuga. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Matiko, kuna Taarifa.

**TAARIFA**

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimpe Taarifa mchangiaji kwamba jambo hili analolizungumza kuhusu mwananchi kupigwa risasi na kwamba inasadikika ni Askari wetu wa Wanyamapori ndio walifanya tukio hili, Wizara imefanya kazi kubwa kufuatilia jambo hili. Timu imekwenda uwandani kufuatilia jambo hili na timu hii ilikuwa ni huru, inayohusisha vyombo mbalimbali, *independent institutions* zilihusika kwenye kufanya uchunguzi wa jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nini kilichobainika? Kilichobainika ni kwamba, hakuna ushahidi wa wazi kwamba jambo hili lilihusisha Askari wetu. Damu iliyoonekana kwenye eneo la tukio ilipelekwa maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali. Matokeo yake yanasema hakuna ushahidi wa moja kwa moja kwamba damu hii ni ya binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, linapokuja suala la maisha ya Watanzania, Serikali hii ipo makini kweli kweli kwenye kushughulikia jambo hilo. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu linapokuja jambo la uhai Watanzania tuwe makini kwenye kutoa taarifa zake. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimeipa muda Serikali kutoa maelezo vizuri ili wananchi waelewe taarifa ambazo zinaletwa Bungeni zisiharibu jina la Serikali bila sababu yoyote. Mheshimiwa Matiko, unapokuwa unatoa taarifa kama, hizi wewe ni mzoefu, uwe na uthibitisho, uwe na vigezo ambavyo kauli zako zisije zikaleta sintofahamu, hasa wewe mwenyewe ukaingia kwenye matatizo na wananchi wako katika maeneo yako. Nakurudishia dakika moja yako.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** *(Hapa alizungumza bila kutumia kipaza sauti)*.

**NAIBU SPIKA:** Unabishana na kiti sasa? *(Kicheko)*

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunaongea kwa nia njema kabisa kuhakikisha Serikali inasimamia uhai wa Watanzania. Ninachokiongea, kuna *series* za *events* za mauji kwenye hifadhi na hili likiwepo, na *evidence* zipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tukio lingine pia lilitokea, nimeelezea la huyu Muhono, nimeelezea la Julius na ninaelezea na vijana wengine wawili walikamatwa tarehe 20 Disemba, 2023 na Askari hawa hawa wa hifadhi wakawa-*torture* wakawa wamewapeleka mahali kuna mto, inasemekana ndiyo wanapoulia watu wetu. Wakataka kuwapiga risasi na hili nimeshamweleza Katibu Mkuu wa Wizara na Waziri husika. Wanataka kuwapiga risasi, hao maaskari *game* walikuwa na watoto. Watoto, malaika ndio wamewaokoa wale vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kijana yupo tayari kuongea na Serikali, wafanye *parade* wawatambue hao Askari, waite familia zao watoto, walikaririwa watoto wetu. Wanasema hilo eneo, wanawapiga risasi wanaanguka na kuna mamba wanakula hao binadamu. Ukiona kwenye hilo eneo kuna nguo nyingi. Waziri anajua, Katibu Mkuu wa Wizara anajua nimewapelekea. Sasa hivi ni miezi mitatu *no action*, *nothing*! Hatuwezi kukubali hii laana, mbuga kugeuka kuwa laana badala ya kuwa neema kwenye nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimetaja matukio matatu, kule nina orodha ya watu waliouawa, mathalan sitawataja majina lakini watu waliouwa katika Kata ya Tuhanje na Gorong'a kwa muda mfupi ni watu 11. Kata ya Nyanungu watu sita wameuawa, majina yapo hapa mmeyafanyia kazi? Hatujarudishiwa ndugu zetu, we *need them;* tunahitaji kuwazika. Hata kama wameingia hifadhini, mmewaua kama majambazi, *bring them* tuwazike kwa mila za Wakurya, ni ndugu zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, waliopigwa risasi wakalemazwa na hifadhi, *evidence* zipo ni wengi tumesema. Mwaka 2013 nilikuwa Mbunge hapa, ilitokea dhuluma hii hii tukalalamika, kulikuwa na Operesheni Tokomeza, ikaundwa Kamati Teule ya Bunge ikaenda ikagundua madudu na zaidi ya Mawaziri watano waliwajibika. Tunaongea siyo kisiasa, tunaongea *bitterly*. Mama ana dhamira ya dhati, *our people* wanauawa. Msiweke huu utani kwa maisha ya watu. Ni Tanzania pekee mwanadamu anafariki watu wana-*take easy,* wanafanya siasa. *This happens only in Tanzania*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni mwanamke, mniulie mwanangu, ninalia kila siku; Mama atafanya *Royal Tour,* atafanya *The Amazing Tanzania,* lakini nikilia laana inaenda. *We will never grow* katika utalii. Tu-*solve* haya mambo *once and for all.* Tutoe elimu wananchi wasiingie kwenye hifadhi. Tufanye mpango katika ardhi, tutoe *priority* kwenye mbunga ili sasa wananchi wasivamie hifadhi. Pangeni Tanzania, tuna eneo kubwa sana. *Why don't you act? Give the priority*, pangeni ardhi watu wasiuawe. Hii haikubaliki kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu mtu unaongea, kuna mtu analeta mzaha… *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Kengele ya pili hiyo. Mheshimiwa Nyoka atafuatiwa na Mheshimiwa Toufiq. *(Makofi)*

**MHE. MARIAM M. NYOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia bajeti ya Waziri Mkuu. Awali ya yote, naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa namna anavyoipambania nchi yake, na anavyotupambania wananchi wa Tanzania. Miradi ni mingi mikoa yote, wilaya zote, kata zote na vijiji vyote vya Tanzania vina miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na wasaidizi wake

wote kwa namna wanavyoshirikiana wakati wa maandalizi ya bajeti pamoja na utekelezaji wa shughuli zote za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie kwenye maeneo matatu. Eneo la kwanza ni mikopo kwa vijana. Tumeona Fungu Na. 65 limetengewa fedha kiasi cha shilingi bilioni moja kwa mwaka 2023/2024, hata hivyo mikopo ile bado haijapelekwa. Kiasi cha mikopo hiyo kwanza ni kidogo ukilinganisha na mikoa yote ya Tanzania kwamba ipate mkopo wa shilingi bilioni moja kwa vijana wote, hii siyo sawa. Pamoja na changamoto ya kiasi hiki kuwa kidogo, uelewa wa vijana wetu kule vijijini juu ya mikopo hii, ni mdogo. Tunawaomba wataalamu wetu waende vijijini wakatoe elimu ya mkopo huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utolewaji wa mkopo huu umekuwa sijui wa namna gani? Ukienda *field* kule kwenye vijiji, vijana wetu wanauliza, hiyo mikopo ya vijana ni vijana gani wanapatiwa mikopo hii? Au ni vijana wa maeneo gani? Mashrti yake ni yapi katika utolewaji wa mikopo hii? Nawaomba wataalamu wetu washuke chini waende wakaandae makundi kwa vijana, wawahamasishe ili nao waweze kunufaika na mikopo hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye eneo lingine la Vitambulisho vya Taifa *(NIDA)*, kutokana na Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 tumeona kundi kubwa la vijana limeongezeka, lakini vijana hawa hawana Vitambulisho vya *NIDA*. Nawaomba wataalamu wa *NIDA* waende vijijini wakawasajili vijana hawa, kwa kuwa mara ya mwisho kwenda vijijini ilikuwa ni mwaka 2016. Hata walivyoenda kwenye vijiji hivyo, wamewasajili lakini changamoto kubwa ni katika upelekaji wa vitambulisho hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vitambulisho hivi wengi wao wamepata namba tu, mpaka leo wanatumia namba kwa muda wa miaka sita mpaka saba. Hata vitambulisho vilivyopelekwa kwenye yale maeneo vitambulisho hivi, vimechanganywa changanywa badala ya vitambulisho kwenda kwenye Kata *A* vimepelekwa

kwenye Kata *B*, inakuwa ngumu vitambulisho hivi vya Taifa kuwafikia walengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, changamoto nyingine ni ucheleweshaji wa vitambulisho hivi. Naiomba Serikali iandae utaratibu mzuri wa kuwafikia wananchi kule vijijini. Wataalamu wetu hao wasikae ofisini, wasikae Makao Makuu, waende vijijini wakawafikie wananchi kwa ajili ya zoezi zima la usajili wa Vitambulisho vya Taifa. Kwa kufanya hivyo, tutakuwa tumetimiza malengo ya Serikali ya kufikia wananchi wetu wenye umri zaidi ya miaka 18 kupata Vitambulisho vya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya eneo hilo, naomba niende kwenye eneo la barabara. Mkoa wa Ruvuma ni kati ya mikoa yenye changamoto kubwa ya barabara mijini na vijijini. Leo naomba niongelee eneo la *by pass* ya barabara inayotoka Mletele inapita Msamala inaenda Mkuzo - Mwengemshindo hadi Namanditi. Upatikanaji wa barabara hii utasaidia kutatua changamoto ya malori yanayopita katikati ya Mji wa Songea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeongea mara kadhaa juu ya barabara hii, wananchi wa Songea wana changamoto kubwa ya malori yanayopita pale katikati ya mji, kama malori ya makaa ya mawe. Suala hili siyo la leo, ni la tangu wakati wa Hayati Dkt. Benjamini William Mkapa, Rais wetu aliyepita. Tathmini yake ya kwanza ilifanyika mwaka 2015. Mpaka hivi ninavyoongea, tathmini tatu zimefanyika juu ya barabara ile, lakini majibu ya Serikali yamekuwa mchakato unaendelea, pia barabara hii imeunganishwa na Barabara ya Lutukila, siyo kweli. Kwani barabara hii ikitengenezwa, wananchi wale wakafurahia na Serikali yao si itakuwa inafurahi wananchi wao tukiwaondolea kero hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali iliangalie hili suala kwa ukaribu. Pamoja na suala hilo, pia kuna ulipaji wa fidia kwa wananchi wanaokaa maeneo hayo. *TARURA* mwaka 2023 imewaahidi wananchi wanaokaa maeneo haya waende ofisini. Hiyo ilikuwa mwezi wa Kumi wakalipwe fidia, lakini hawajalipwa

mpaka sasa hivi. Waliahidiwa tena waende mwezi Januari mwaka huu 2024, wameenda ofisini wanaambiwa bado. Serikali iwe wazi kwa wananchi wale, kama hakuna fidia tuwaambie na kama kuna fidia tuwaambie. Kama hakuna fidia kabisa tuwaache waendelee kufanya shughuli zao za maendeleo, tusiweke kigugumizi kwenye suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali, kati ya mambo yote muhimu inayoyafanya, tuuangalie Mkoa wa Ruvuma kwenye hii changamoto kubwa inayopatikana pale, juu ya suala zima la barabara ya *by pass* inayotoka Mletele kuelekea Namanditi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, pia naipongeza Serikali katika maeneo mbalimbali, sekta mbalimbali kwa Mkoa wa Ruvuma zimekuwa zikinufaika na miradi mingi ya Mheshimiwa Mama Samia. Tumeona mambo mengi yanayofanyika mkoani kwetu, wilayani kwetu, hakuna mtu atakayebeza juu ya hilo na hakuna mtu atakayeambiwa tazama, kila mtu anajionea mwenyewe kwa macho yake, anasikia mwenyewe kwa masikio yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sina mengi lakini nilikuwa naiomba Serikali iende kuboresha maeneo haya muhimu matatu ambayo nimeyataja ambayo ni eneo la Vitambulisho vya *NIDA,* eneo la barabara yetu *by pass* kutoka Mletele kwenda Namanditi na mwisho ni eneo la mikopo kwa vijana. Vijana wetu hawa tunaomba wafikiwe na hii mikopo. Tunaomba wakanufaike badala ya kundi la watu wachache wananufaika na mikopo hii. Wananchi wetu, wale vijana wetu hawafahamu hii, wanafahamu zaidi ile ya asilimia 10 tu ya halmashauri. Kwa hiyo, naomba Serikali ifanye utaratibu mzuri, ifanye maandalizi mazuri, namna ya kuwafikia vijana wetu wa nchi nzima ili nao waweze kunufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo naomba kuunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Fatma Toufiq, atafuatiwa na Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani na Mheshimiwa Flatei ajiandae.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuchangia hoja. Nachukua fursa hii kwanza kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema nami niweze kuchangia hoja hii ya hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge kwa mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami pia naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wote ambao wameshachangia kwa kuendelea kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa maono yake ya kuhakikisha kwamba Watanzania tunapata maendeleo endelevu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri. Pia nampongeza Naibu Waziri Mkuu, Mawaziri wote katika Wizara hii, Naibu Mawaziri na Watendaji wote kwa hotuba ambayo imeandaliwa kwa umahiri mkubwa sana, nawapa pongezi nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijielekeze katika maeneo matatu. Nitajielekeza katika miradi ya kielelezo kwa mwaka 2023/2024 ambayo ipo ukurasa wa 11 hadi ukurasa wa 16, sambamba na hilo, nitazungumzia kuhusu masuala ya kazi na wafanyakazi, ambayo katika hotuba hii ipo ukurasa wa 74 hadi ukurasa wa 83, na hali kadhalika nitazungumzia kuhusu uratibu wa maafa ambayo ipo ukurasa wa 92 hadi ukurasa wa 94.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa miradi ya kielelezo ambayo ipo miradi minane, nitazungumzia ule mradi wa uwekezaji wa kiwanda cha Mkulazi ambacho ni kiwanda cha sukari. Kiwanda hiki kimewekezwa kwa pesa ya ndani kwa asilimia 100. Naomba niipongeze sana Serikali kwa kuweza kuwekeza katika

kiwanda hiki. Pia ujenzi wa kiwanda hiki umeshafikia asilimia 99, hii ni hatua kubwa sana. Halikadhalika uzalishaji katika kiwanda hiki umeweza kuanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaamini kwamba iwapo kiwanda hiki uzalishaji wake utafikia ile *full swing* ambayo ni tani 50,000 kwa mwaka, itasaidia kupunguza ile nakisi ya sukari ambayo imekuwa ikitokea mara kwa mara nchini, lakini ninaamini kabisa kwamba kama mradi huu utatekelezwa vizuri, maana yake uzalishaji unaweza ukazidi na hatimaye unaweza ukakidhi kuweza kupata sukari katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo, natambua kwamba katika kipindi cha mwaka uliopita, hadi mwaka huu, kumekuwa na mvua za *El-Nino*, na miongoni mwa maeneo ambayo yameathirika sana ni pamoja na viwanda vya sukari ikiwemo kiwanda cha Mkulazi kwa sababu miwa ile imekuwa ikiathiriwa sana na maji au kuna uharibifu uliotokea au pengine uvunaji umekuwa una matatizo sana. Sasa je, Serikali haioni kwamba umefikia wakati wa kuangalia namna bora kwamba pengine kama imebainika kuna majanga kama hizo mvua za *El-Nino* ambazo zinaweza zikaleta athari, yale matenki ambayo yapo pale, ule mchuzi unaozalishwa kwa kukamua ile miwa uweze kupatikana kwa wingi zaidi ili kusudi mchuzi ule uweze kuhifadhiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, kuna ile *syrup* ambayo mwisho wa siku ikiwa *processed* inakuja kuwa sukari, ingewekwa mle kwa muda mrefu mahali ambapo haitaharibika ili kusudi kuwe kuna hifadhi ya kutosha pindi inapotokea madhara kama haya, sukari iweze kuzalishwa kwa wingi. Ninaamini jambo hili linaweza kupatikana. Natambua kwamba tahadhari zimekuwa zikichukuliwa, lakini basi ichukuliwe tahadhari ya mapema zaidi na kuona kama majanga mengine yanaweza yakatokea *in the future,* basi matenki haya yaweze kuwepo ya kutosha ili kusudi ile miwa iweze kuvunwa kwa wakati, halafu mchuzi wake ule uweze kuhifadhiwa na hatimaye kutengenezwa sukari.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nilitamani kulizungumzia ni kuhusiana na masuala ya wafayakazi ambayo ipo ukurasa wa 74 hadi ukurasa wa 83. Naendelea kuipongeza sana Serikali kwa kuratibu uzalishaji wa fursa za ajira ili Watanzania hasa vijana ambao ni kundi kubwa sana, ambao wamekuwa na tatizo kubwa sana la ajira, waweze kusaidiwa. Sina shaka Serikali imekuwa ikijitahidi sana na imekuwa na *programs* mbalimbali za kuhakikisha kwamba vijana wanapata ajira, wanaajiriwa au wanaweza wakajiajiri wenyewe na hasa zile ajira ambazo zina staha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie zaidi kwenye lile *program* ya kukuza ujuzi. Natambua kwamba Serikali imekuwa na juhudi nyingi sana za kuhakikisha kwamba vijana wanapata mafunzo ya ujuzi katika fani mbalimbali. Bahati nzuri Kamati yetu ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii imeweza kutembelea vituo mbalimbali ambapo Serikali imekuwa ikitekeleza miradi hii ya kukuza ujuzi kwa ajili ya vijana. Tumeona na kwa kweli tunaipongeza sana Serikali. Vijana wenye ulemavu wamekuwa wakipata stadi za ujuzi kama ufundi cherehani, ufundi magari, ufundi uashi, ufundi bomba na mengineyo mengi. Kwa hiyo, hii ya ujuzi ina maana kwamba mwisho wa siku vijana hawa wote wenye ulemavu na ambao wapo kawaida wataweza kujiajiri wao wenyewe na hatimaye waweze kujikwamua katika suala zima la maisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, ni kwamba kuwa na hivi vituo na hizi *programs* ni jambo moja, nilikuwa ninaomba niishauri Serikali ione umuhimu wa kutenga bajeti ili vijana hawa wanapokuwa wamefuzu mafunzo yale ya kukuza ujuzi, iweze kutengwa bajeti maalum ili baadhi yao ambao watakuwa wana uhitaji wa vifaa au vitendeakazi, waweze kupatiwa ili waweze kwenda kufanya kazi. Inawezekana kabisa kuna mwingine ni fundi cherehani lakini hana uwezo wa kununua ile cherehani. Pengine huyu ni fundi uashi lakini hana uwezo wa kununua vile vifaa vya uashi au ni seremala au ni fundi bomba. Kwa hiyo, kama itawezekana Serikali ione sasa pia inatenga bajeti kidogo ili kusudi wale watakaomaliza waweze kupata vifaa au vitendea kazi na waweze kujiajiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo jingine ambalo napenda kulizungumzia kuhusiana na hili suala la ajira, kwanza naipongeza sana Serikali kwa kuunganisha Watanzania na ajira za nje ya nchi. Sambamba na hilo nawapongeza Watanzania wote ambao wanafanya kazi nje ya nchi. Vilevile naipongeza Serikali kwamba hivi karibuni iliingia mkataba na nchi za Saudia pamoja na Falme za Kiarabu ili Watanzania waende wakafanye kazi kule. Nawapa pongezi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuishauri Serikali kwamba ni budi ikafanya *shopping* katika zile nchi nyingine ambazo bado zina upungufu sana wa ajira ili kusudi Watanzania pia waende katika nchi nyingine ikiwemo pengine Canada, Switzerland na nchi nyinginezo ambazo pia kuna nafasi za ajira ili kusudi vijana wengi zaidi waweze kufanya kazi nchi za nje au huko ughaibuni. Tunaamini kabisa kwamba wakienda kule nchi yetu inaweza ikapata faida kubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba niishauri Serikali iweke mfumo maalam wa kuwabaini wafanyakazi wote wa nje ili kuweza kusimamia ukusanyaji mapato kupitia ujira wao. Kuna baadhi ya nchi ambazo zimefanikiwa au zimekuwa zikiongeza pato la ndani kwa kupata pesa kutokana na wale wafanyakazi wao ambao wanafanya kazi nchi za nje kwa sababu nao wana mfumo maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikitaja nchi chache miongoni mwa nchi hizo ni pamoja na Egypt ambayo imeweza kupata dola bilioni 24.5, lakini pia wenzetu Nigeria wameweza kupata dola bilioni 20.5, Morocco wameweza kupata dola bilioni 12.1, Ghana wameweza kupata dola bilioni 4.9, Kenya pia wenzetu nchi jirani wameweza kupata dola bilioni 4.2. Ninaamini kabisa na kwetu Tanzania inawezekana, lakini ni budi tukaweka mifumo mizuri ili kuwabaini watu hawa, na mwisho wa siku waweze kuipatia kipato nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo nilikuwa naishauri Serikali iweze kutuma wataalam waende katika hizi nchi ambazo

zimefanikiwa kuwapeleka watu wao kule nje ya nchi ili kusudi waweze ku…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Fatma, kengele ya ili imelia.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa nafasi hii ya kuchangia katika Wizara hii muhimu sana. Kuna msemo unaosema; "*progress is a double edge sword*" au maendeleo ni upanga wenye makali kuwili, ikiwa na maana kwamba kwa namna yoyote tunayopata maendeleo kuna hasara fulani fulani zinazotokana na maendeleo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii tunazungumzia nchi yetu ina utaratibu wa elimu bure na kwa hiyo, naipongeza sana Serikali yangu ya Chama Cha Mapinduzi. Pia siyo elimu bure tu, ni ya lazima, na mikopo inatolewa mpaka kwa elimu ya juu. Katika vita hiyo ya kuondokana na adui ujinga, tumejikuta tumekuwa na vijana wengi zaidi ambao wana elimu, lakini hawana ajira na hiyo sasa imekuwa ni changamoto namba moja kwa vijana wetu wa Kitanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa sababu imekuwa inaonesha utashi wa moja kwa moja kupambana na changamoto hii. Tumeona ajira zinatafutwa mpaka nchi za nje, vijana wetu wanapewa. Pia tumeona Mheshimiwa Rais anapiga kelele kuhakikisha kwamba asilimia kumi za vijana zinarudishwa tena kwa utaratibu ulio bora. Hii yote ni kumkomboa kijana wa kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili nina machache ya kushauri. Moja, pamoja na kwamba tunapigia kelele zaidi asilimia

kumi ambazo kaka yangu Mheshimiwa Deo, wewe ni kijana mwenzetu, tunaamini maelekezo aliyoyatoa Mheshimiwa Rais mkiwa mnaapishwa, mtakwenda kuyatekeleza tena kwa mwaka huu wa fedha, katika bajeti hii. Naomba mhakikishe asilimia kumi za vijana zinarudi kwa sababu muda huu wa karibu mwaka mmoja ambao asilimia kumi hizi hazikutolewa, tumeona *gap* kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana tumepata changamoto kubwa sana ya kupata mitaji, na takwimu zilizotolewa na Serikali zinaonesha kila mwaka kwamba zaidi ya vijana milioni 16 na kuendelea wana-*approach financial institutions* kwa ajili ya kupata fedha, lakini hawapewi kutokana na upungufu mwingi waliyonao ikiwepo kutokuwa na dhamana. Fedha hizi zilikuwa zinatusaidia sana, tunaomba mzirudishe ili ziendelee kutusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nilikuwa nashauri kitu kimoja. Bunge hili katika utashi huu huu wa kumkomboa kijana wa Kitanzania, mwaka 2023 tulipitisha Sheria ya Manunuzi. Katika sheria hii tuliandika kwamba 30% ya fedha zote za manunuzi ziende kwa makundi maalum, 10% kwa vijana, 10% kwa wanawake, asilimia tano kwa wazee na asilimia tano kwa watu wanaoishi na ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu zinazokusanywa na *PPRA* zinaonesha Halmashauri zetu hazifuati utaratibu huu. Mheshimiwa Deo wewe ni kijana mwenzetu nenda katusaidie. Leo hii tunavyozungumza 65% mpaka 70% ya bajeti nzima tunayopitisha katika Bunge hili ni fedha zinazokwenda kwenye manunuzi. Mwaka wa fedha uliopita tulipitisha bajeti ya shilingi trilioni 44, mwaka huu tunazungumzia shilingi trilioni 49. Kama 65% mpaka 70% ya fedha hizi zinakwenda kwenye manunuzi na 10% ya fedha hizi, zinatakiwa ziende kwa vijana kwa namna ya kuwapa kazi na *tender*. Ninaamini tatizo la vijana kukosa ajira changamoto hiyo inaenda kwisha tukihakikisha fedha hizi zinakwenda zinapotakiwa. Tunaomba sana Serikali iliangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niliwahi kushauri katika Bunge hili Tukufu kwamba kulikuwa na *program* ya *NSSF* kwa vijana. Nikiwa

Mjumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria, tuliona kwamba *NSSF* ina utaratibu wa kuwa inakusanya fedha kiasi kwa vijana au kwa watu na baada ya muda fulani watu hawa wanakuwa *viable* kupewa mikopo ya vifaa mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilishauri kwenye Bunge hili kwamba *program* hii iwe *tailored* kupelekwa kwa vijana wa vyuo vikuu. Namshukuru sana Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Mheshimiwa Jenista, alipokea wazo hili na akasema wanakwenda kulifanyia kazi ili vijana wa vyuo na vyuo vikuu wakiwa wanajiwekea akiba ndogo ndogo kupitia fedha zao za kujikimu na mikopo wanayopewa na Serikali *by the end of three to four years* mtu huyu awe na zaidi ya fedha inayomwezesha kupata pikipiki, au vifaa vya kufyatulia tofali, au kupata mashine mbalimbali ambazo zitamfanya kijana anapotoka chuoni aweze kwenda kujiajiri moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wazo hili lilipokelewa, utafiti ukafanyika, ikaonekana linawezekana, lakini mpaka sasa utekelezaji wake haujaeleweka. Vijana wa vyuo wanauliza, kwa sababu wanataka kuingia kwenye mpango huu ili wakimaliza watoke vyuoni waingie mtaani wakiwa wanajua wanakwenda kufanya nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tuna Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ulio chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Nchi hii inaongoza kwa mipango. Katika Mpango wa Miaka wa Miaka Mitano tuliopitisha ndani ya Bunge hili tukiwa tunaanza mwaka wa kwanza, tulipisha kwamba mfuko huu kwa miaka yote mitano utapewa kiasi cha shilingi bilioni tano, lakini mpaka leo tunapozungumza, mfuko huu umepewa shilingi bilioni moja tu, kwa maana ya kwamba katika miaka yote mitatu ni mwaka mmoja tu ambao ni 2023 ndiyo fedha ziliingizwa. Jambo la kusikitisha zaidi, mwaka huu badala ya kuendelea kutenga shilingi bilioni moja moja, wamepunguza mpaka shilingi milioni 600. Hii yote inakwenda kinyume na utashi tunaouona wa Serikali kusaidia vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi yanayotolewa katika mfuko huu ya vijana kuhitaji mikopo ni mingi, lakini badala ya kutafuta vyanzo vingine kuongeza fedha katika mfuko huu kufidia fedha ambazo zimekuwa hazitolewi kwa miaka mingine, badala yake wanapunguza zaidi fedha hizi. Katika hili naomba Mheshimiwa Waziri anapokuja kutujibu atusaidie kupata *justification* ya upunguzaji wa fedha hizi, na ni kwa nini zisiongezwe na zile ambazo hazikutolewa kwa miaka mingine iliyopita, kwa nini zisitolewe ili vijana waweze kunufaika? Pia ili kuweza kusaidia kuzalisha ajira nyingi zaidi kwa vijana, *attention* kubwa zaidi iwekwe kwenye kuanzisha viwanda, kusaidia vijana kuanzisha viwanda ili wajiajiri na kuajiri wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ilani yetu imesema kwamba nchi yetu itahakikisha kwa miaka hii mitano, inaanzisha viwanda vingi zaidi. Leo hii tunaongelea mapinduzi katika sekta ya kilimo, hizo zote ni malighafi, zinakwenda kuchakatwa wapi? Huku ndiko tunapotakiwa pia kuzalisha ajira nyingi kwa vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati huo huo namwomba Mheshimiwa Waziri Deo, vijana wengi wanaofanya kazi kwenye viwanda vya wawekezaji wetu wa nje wanalalamika, *treatment* yao siyo nzuri. Naomba sana, Maafisa wetu wawe wanatembelea mara kwa mara kuhakikisha Watanzania hawa vijana wanaofanya kazi kwenye hivi viwanda wanakuwa *treated* kama ambavyo sheria zetu zinataka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ambao utakuwa ni wa mwisho ni kwenye suala zima la vijana kujitolea. Nimewahi kuomba hapa zaidi ya mara moja au mbili, kwamba Serikali ituletee sera ya kutoa kipaumbele kwa vijana wanaojitolea katika ajira. Tunavyozungumza hapa, mpaka sasa sera hiyo haijaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwa Serikali, tulikuwa na utaratibu miaka ya nyumba ambapo kulikuwa na uwazi na utayari wa Serikali katika taasisi zake na Halmashauri na Bodi zake nyingine kupokea vijana wanaojitolea na kuwa-*mentor* wakiwa wanasubiri kupata ajira. Utaratibu huu kwa sasa siyo *formal,* naiomba Serikali ije

na sera ambayo itaruhusu na ikiwezekana kulazimisha taasisi mbalimbali za Serikali kuwapokea vijana wanaojitolea ili waweze kupata uzoefu, lakini pia katika kujitolea huko wanachangia katika pato la Taifa. Pia kijana akiruhusiwa kujitolea katika sekta hizi za Serikali, siyo wote wanaoishia kusubiri ajira za Serikali, kuna mwingine kupitia kufanya kazi humo, anaamua kupata uelekeo mwingine kwa fursa hiyo aliyoipata.

Mheshimiwa Naibu Spika, wahenga walisema "mtembea bure sio sawa na mkaa bure." Leo hii kijana anayehitimu, anayekaa nyumbani ni tofauti na yule ambaye tukimruhusu aende akajitolee kwenye taasisi zetu za Serikali. Utakuta kijana anaomba kujitolea tu kwenye Halmashauri, lakini anabembeleza utadhania anaomba kulipwa, wakati anaomba kujitolea na halipwi, atakuwa anajigharamia mwenyewe. Anachotaka ni kupata uzoefu tu. Tuombe Serikali ije na sera ambayo italazimisha vijana kukubaliwa kujitolea kwenye sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliwahi kuliulizia nikaambiwa kwamba changamoto ni kwamba vijana wanaonekana watavujisha siri. Nadhani ni jukumu la Serikali kuhakikisha kwamba inatunza taarifa zake ili ambaye hatakiwi kuziona asizione, lakini tusizuie au kutumia kigezo hiki kukatalia vijana kujitolea katika taasisi zetu ili wapate uzoefu unaostahili. Pia nadhani ni wakati sahihi sasa wa Serikali kuja na sera ambayo itatuonesha namna gani vijana wanaojitolea watapewa kipaumbele pale ambapo ajira zitatangazwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Flatei, atafuatiwa na Mheshimiwa Jonas William Mbunda na Mheshimiwa Kakunda ajiandae.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi. Kwanza, nianze kwa kumshukuru sana Mungu kwa afya. Pia

namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kazi njema anayoifanya hasa katika majimbo yetu na miradi ya maendeleo ambayo kimsingi tumeshuhudia katika maeneo yetu ya majimbo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kweli anafanya kazi nzuri ambayo Wabunge na wananchi wanaiona. Mheshimiwa Waziri Mkuu, hongera sana. Biblia inasema; "Moyo usio na shukurani hukausha mema mengi." Pia nawashukuru Waheshimiwa Mawaziri wanne, maana yake Naibu wawili na Mawaziri wawili ambao mnamsaidia Mheshimiwa Waziri Mkuu katika utendaji wa Wizara yetu hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nina machache, nataka niende haraka kidogo kwa sababu najua muda ni mfupi. Mheshimiwa Waziri Mkuu, kule kwangu kuna shida kubwa hasa ya umeme, *REA* haikufanya vizuri kule kwetu. Jimboni kwangu kuna vijiji 76; kati ya vijiji hivyo, vijiji 19 havijawaka umeme mpaka ninavyoongea sasa. Najua Mheshimiwa Waziri amesema sana katika hotuba yake kuwa wamefika asilimia 96, lakini Tanzania tuna majimbo 254. Ukigawa hiyo idadi ya vijiji, unaweza kukuta kila jimbo lina kijiji kimoja, lakini mimi kwangu viko 19 ambavyo havijawaka. Naomba tu kwa kweli, najua Mheshimiwa anafanya kazi kubwa, basi iwekwe nguvu kidogo kwa yule mkandarasi amalize vile vijiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua kuna mradi unaokuja unaoitwa Ujazilizi, basi tusipoteze hiyo nafasi ya Ujazilizi, lakini pia kuna kilometa mbili katika maeneo hayo. Kwa hiyo, ombi langu ni kwamba wananchi wa Jimbo la Mbulu Vijijini wakumbukwe katika hali hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, liko jambo hapa la miradi viporo. Mheshimiwa Waziri Mkuu ameisema katika hotuba yake, lakini naomba pia mtusaidie Hospitali yetu ya Wilaya haijakamilika. Tatizo dogo tu limetokea, ni katika ule mtiririko wa kupelekewa fedha, basi imerukwa shilingi milioni 800. Kwa hiyo, naomba tu katika ule mtiririko wa fedha, basi irudiwe pale, tupate ile fedha ili Hospitali yetu ya Wilaya iweze kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika maeneo ya utawala, Mheshimiwa Waziri Mkuu, ukiangalia sensa iliyopita ya mwaka 2012, tulikuwa Watanzania kama milioni 40 na kitu, leo tuko milioni 61. Sasa maeneo ya utawala kwa kweli kule yamekuwa makubwa, hasa kwenye Jimbo la Mbulu Vijiji na maeneo mengi. Vijiji na kata zinahitaji kugawanywa kutokana na wingi wa watu. Kutokana na sera ambayo tumeiweka sisi kama Serikali ya *D by D*, ugatuaji wa madaraka kwa kupeleka madaraka kule vijijini kutokana na vijiji kuwa vikubwa sana. Vitongoji vingine ni vikubwa, vina shule za msingi mbili na vina ofisi zao. Sasa wanachohitaji tu ni kupewa hadhi ya kuwa kijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna vijiji vyangu vya Haydom, Haydarer, Dongobesh, Maretadu, Imboru, Sidgi, Mangisa na vijiji vingine ambavyo vinataka kugawanywa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, najua Mheshimiwa Waziri Mkuu amefika mwenyewe ametembelea pale, tunamshukuru...

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba wachangiaji waelekeze hoja kwenye Kiti. Hii kuwatajataja Mawaziri na kumtaja Mheshimiwa Waziri Mkuu, anamtoa kwenye reli. Ana *document* pale anasoma, lakini kila saa anasikia Waziri Mkuu, Waziri Mkuu, yeye anatakiwa aongee na kiti. Naomba ungewaelekeza wachangiaji namna hiyo. *(Makofi/Vicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Flatei.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, namheshimu sana ndugu yangu, lakini naomba niiache, niendelee na mchango wangu. Naona ananipotezea muda. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tena Mheshimiwa Waziri Mkuu, hii hotuba tunayoichangia ni ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na bajeti hii ndiyo ya kwake. Kwa hiyo, naomba uniruhusu niendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunazo barabara ambazo kimsingi zimeshasainiwa. Kwa mfano, barabara ambazo zimetajwa katika hotuba yake na barabara ya *EPC+F*. Ukiangalia Wizara ya Ujenzi inapewa fedha na mpaka Desemba wamepewa 64%. Ukiangalia kwenye *folder* la maendeleo tuliyotengea shilingi bilioni 482.2, ukiangalia mpaka sasa hivi wamepewa shilingi bilioni 280.2. Ukiangalia, ni wazi kwamba kutokana na fedha zilizotolewa, siyo rahisi miradi yote ikatekelezwa. Ukiangalia sasa hivi, wakandarasi wengi wako *site* na hawana namna yoyote kwa sababu hawajapewa fedha na hawajalipwa. Ushauri wangu ni kwamba, ni vyema tukatenga bajeti kubwa ambayo itasaidia wakandarasi hawa kulipwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia sasa hivi Wizara ya Ujenzi, maeneo mengi bado hayajapewa pesa na wakandarasi wako *site*. Mimi ombi langu, ikija wakati wa bajeti hii tuone namna ya kufanya. Serikali iongeze bajeti na sisi Wabunge hebu tuisaidie Wizara ya Ujenzi kwa sababu kila Mbunge humu analalamika kwa habari ya barabara na hali ya barabara siyo nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia hata fedha za dharura zimetengwa kidogo sana. Kutokana na bajeti hapa, nimeangalia kwenye bajeti hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu hasa kwenye upande wa maafa, hali siyo njema. Ukiangalia pale Hanang tulipeleka fedha nyingi na tunashukuru sana Watanzania wengi waliweza kuchangia, lakini sisi kama Serikali tungetenga bajeti kubwa hapa ingekuwa rahisi kusaidia Wizara ya Ujenzi na tukawasaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye *EPC+F,* tunashukuru sasa tumesaini barabara nyingi na juzi pia tumesaini kilometa saba. Sasa kwenye maeneo yetu kuna kilometa 53 sasa hivi. Ombi langu ni kwamba, fedha zipelekwe ili wakandarasi waliopo *site* waendelee. Vinginevyo, maana yake ni kwamba tutakuwa tumesaini hii

mikataba lakini baadaye barabara zitakuwa hazijengwi na wananchi baadaye watatupa maswali mengi ya kujibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama umesaini barabara na muda unazidi kwenda, maana yake nini? Maana yake ni kwamba wananchi watajua hii tumeshawadanganya, lakini ili tusionekane waongo, ni vizuri zaidi tukapeleka fedha, wakandarasi wakaendelea. Maana yake, ukiangalia kitaalam hapa, kama barabara imesainiwa mwaka 2023 na tunaendelea kukaa hivi tu, maana yake ni kwamba gharama itapanda na kama barabara ilikuwa inaisha kwa shilingi bilioni 300 ni wazi kwamba itakwenda kuwa shilingi bilioni 400, na kwa mujibu wa sheria, itabidi tuwalipe wakandarasi wale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ombi langu, Serikali ipeleke fedha na Mheshimiwa Waziri wa Fedha apeleke pia fedha ili barabara zianze kujengwa na wananchi waone kwamba barabara zao na ahadi iliyotolewa na ilani, izidi kutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nieleze suala lingine hasa hili la ujenzi wa barabara. Nawashukuru sana, tumesaini barabara hizi, ni mwanzo mzuri sana na tumefunga ndoa. Sasa ombi langu, ndoa iwe na watoto basi. Maana yake leo tunaposaini, maana yake ni kweli kabisa wananchi wanaona tumesaini, lakini kusaini ni jambo moja na kujengewa barabara au kupelekewa fedha ni jambo lingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo naomba tena kwenye Hotuba ya Waziri Mkuu, kwa kweli sasa fedha zipelekwe ili barabara zianze kujengwa. Mwishoni hapo hatutaelewana kwa sababu wananchi wanatusubiria. Umebaki muda mfupi sasa, leo ni mwaka 2024 ambapo tunaenda kupitisha bajeti nyingine. Umebaki muda mfupi sana, miezi kama miwili hii ambayo itatusaidia kuona kwamba tunakwenda kwenye bajeti nyingine ya mwaka 2024 kwenda 2025, ombi langu ni fedha zipelekwe ili walau barabara hizi ziweze kujengwa. Naamini Mheshimiwa Waziri Mkuu ni mtu wa kazi na anachapa kazi kweli kweli. Anao Mawaziri wanne wanamsaidia,

mimi naamini kwa michango hii tunayotoa sisi wawakilishi wa wananchi, mtaiangalia na mtaifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kuhusu mikopo kwa vijana. Najua mko Mawaziri vijana mnaomsaidia Mheshimiwa Waziri Mkuu. Uko ndugu yangu Mheshimiwa Ndejembi, Mheshimiwa Ummy na Mheshimiwa Katambi uko hapo. Hebu saidieni vijana katika nchi hii, mikopo hii inatakiwa na vijana. Tumeshapata maswali mengi kule. Najua utaratibu haukuwa mzuri, basi wekeni utaratibu wa kibenki vizuri kabisa vijana wapate mikopo. Nina uhakika vijana wakipata mikopo, watakushukuru, nao wataweza kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wewe unajua wazi kabisa vijana walioko mtaani sasa hivi ni wengi, wanahitaji hiyo mikopo na wanaisubiri kwa hali na mali. Sisi katika mikutano yetu ukifika tu unaulizwa Mheshimiwa Mbunge, mikopo inaanza lini na inakuwaje? Kwa sababu imesimama. Kwa muda mfupi huu ambao imesimama, msije mkaondoa ile *percent* yao. Ijumlishwe kutokana na *percent*, kutokana na mwezi na mwezi, tuendelee kutoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na ahsante sana, na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jonas Mbunda, ajiandae Mheshimwa Kakunda na Mheshimiwa Esther Malleko.

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Awali ya yote, naomba nichukue nafasi hii nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi ya uhai na nimepata muda wa kuchangia hotuba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nichukue nafasi hii nimshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi anavyosimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali pamoja na shughuli mbalimbali za

maendeleo. Pia, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa pamoja na Naibu Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko kwa kusimamia vizuri shughuli za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa jinsi anavyotuongoza na kusimamia shughuli mbalimbali za Serikali. Namshukuru na kumpongeza pia ndugu yangu, rafiki yangu Mheshimiwa Deo Ndejembi kwa jinsi anavyoisaidia Serikali katika kutekeleza majukumu mbalimbali. Vilevile nawapongeza Waheshimiwa Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu kwa kumsidia Mheshimiwa Waziri Mkuu katika kutekeleza majukumu yake mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirudie kumpongeza sana na kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutekeleza miradi mbalimbali katika maeneo yetu ya majimbo kwa nchi nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuanzia, nikifuatilia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, inaonesha kabisa makusanyo ya Serikali hadi Januari, 2024 tulifikia 95.9%. Ni makusanyo mazuri na ninaomba Serikali iendelee kusimamia na kuimarisha mifumo mbalimbali ya ukusanyaji wa mapato kupitia *TRA* na kupitia Serikali zetu za mitaa. Naomba Serikali kwenye suala hili la mapato iendelee kupanua wigo wa vyanzo mbalimbali vya mapato ili tuweze kuongeza mapato yetu, yaweze kutusaidia katika miradi mbalimbali ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwenye suala la miundombinu ya barabara. Mwanzo kabisa katika Jimbo langu nilikuwa napata shilingi milioni 280, lakini sasa hivi Serikali imeongeza wigo, tumepewa shilingi bilioni 2.8 ambayo imetusaidia sana kutengeneza barabara katika maeneo mbalimbali ya Jimbo la

Mbinga Mjini. Serikali pamoja na kuongeza wigo wa bajeti hii ya barabara, lakini kulikuwa na changamoto kubwa sana hasa kipindi cha mvua katika sehemu mbalimbali za barabara katika Jimbo la Mbinga Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na changamoto kubwa sana ya Barabara ya Mbinga – Mpepai – Mtua. Kama unavyofahamu eneo la Mbinga, sehemu kubwa ni miinuko ya milima. Sehemu hiyo ilikuwa imeharibika sana na wananchi wa kutoka eneo la Mpepai walishindwa kusafirisha mazao na hata kusafiri katika hali ya kawaida kuja eneo la Mbinga kwa ajili ya kumaliza shughuli zao mbalimbali za kijamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kulikuwa na changamoto ya barabara ya kutoka Mbinga – Kikolo hadi Kihungu ambapo maeneo haya yote yana jiografia sawa. Pia, kulikuwa na changamoto ya Barabara ya Mbinga – Kitanda hadi Masumeni. Kwa hiyo, naomba Serikali itakapoangalia uwezekano wa kutekeleza kwenye majukumu ya dharura, iangalie maeneo hayo matatu, barabara hizo tatu zikamilike ili ziwasaidie wananchi kusafirisha mazao na mambo mengine mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mbinga Mjini ni Jimbo ambalo nalo limepewa fursa katika Mradi wa *TACTIC*. Kwa hiyo, naiomba Serikali itusaidie, kwani wananchi wanausubiri huu mradi kwa hamu sana. Mradi huu utasaidia kutengeneza barabara za pale Mbinga Mjini pamoja na miradi mingine ambayo itaisaidia halmashauri kuongeza mapato mbalimbali. Kwa hiyo, naiomba Serikali isimamie na itekeleze mapema mradi huu wa *TACTIC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, naipongeza Serikali kwa kutekeleza miradi mbalimbali ya maji katika Jimbo la Mbinga Mjini. Pamoja na utekelezaji wa miradi hiyo, lakini bado kuna miradi ambayo haijakamilika. Kwa hiyo, naiomba Serikali itenge fedha kwa ajili ya kukamilisha miradi hiyo ya maji ili kuwasaidia wananchi waweze kupata maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali kwa upande wa elimu, kwanza kwa kuendelea kutoa elimu bila malipo, na pia kwa kujenga miundombinu mbalimbali katika shule zetu za msingi na sekondari. Katika Jimbo langu Serikali imejenga shule mbili mpya za msingi na shule mbili mpya za Serikali. Pili, imejenga majengo mengi katika shule mbalimbali ili kuhakikisha kwamba wanafunzi wetu wanapata elimu katika mazingira mazuri. Pia, Serikali inaendelea kutoa mikopo ya elimu ya kati pamoja na elimu ya juu. Naipongeza sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuimarisha miundombinu kwenye shule zetu za msingi na sekondari, wananchi wameanza kujenga maboma kwa kutumia nguvu zao. Kwa hiyo, naiomba Serikali itenge fedha kwa ajili ya kukamilisha maboma ili kuunga mkono nguvu za wananchi na kuhakikisha kwamba tunaendelea kuwapa wananchi moyo wa kujitolea katika maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali kwa upande wa nishati, imejitahidi kupeleka umeme kupitia *REA* katika maeneo mbalimbali ya vijiji vyetu, lakini kwenye eneo langu la Mbinga Mjini bado kuna vijiji ambavyo havijapelekewa umeme. Kuna Kijiji cha Ruvuma Chini, Kijiji cha Ruhangai, Kijiji cha Mtua, Kijiji cha Kikolo, Kijiji cha Luhehe na Kijiji cha Iringa. Baadhi ya maeneo hayo, Serikali tayari imeanza kupeleka nguzo. Tunategemea baada ya mvua kufika mwisho, Serikali itakamilisha miradi hiyo na itaendelea kupeleka maeneo mbalimbali. Naomba kushauri kwamba mara baada ya ukamilishaji wa upelekaji wa miradi ya umeme kwenye vijiji, naomba Serikali ianze kupeleka umeme kwenye vitongoji kwa sababu wananchi hawa wana mahitaji makubwa sana ya umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye upande wa afya naomba nipongeze Serikali kwa kupeleka fedha kwenye maeneo mbalimbali ya zahanati, ujenzi wa vituo vya afya pamoja na hospitali. Upande wa Jimbo la Mbinga Mjini, tulipata shilingi milioni 500 ya kujenga Kituo cha Afya katika Kata ya Mbangamao

ambacho kimekamilika. Pia tulipata shilingi milioni 250 kujenga Kituo cha Afya Kata ya Muyangayanga. Naiomba Serikali ituletee shilingi milioni 250 zilizobaki ili kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Afya katika Kata ya Muyangayanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali vilevile kwani tulipewa shilingi milioni 900 kwa ajili ya kukarabati hospitali kongwe. Kazi hiyo imeanza na wananchi wale wamefurahi sana, lakini naomba tuongezewe fedha ili tuweze kukamilisha ukarabati na ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Mbinga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa kilimo, naipongeza sana Serikali kwa kuendelea kutoa ruzuku ya pembejeo kwenye mazao yetu, lakini bado kuna haja ya kuendelea kuangalia tozo mbalimbali katika zao la kahawa ili zipunguzwe. Pia, kuendelea kuhakikisha kwamba masoko ya uhakika yanapatikana katika mazao haya ya kahawa pamoja na mahindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na wachangiaji waliopita kusema kwamba, katika maeneo yetu bado kuna changamoto na wananchi wanalalamika sana hasa wale wastaafu kwenye suala la kikokotoo. Naomba niishauri Serikali kwamba kwenye eneo hili, ikae na vyama mbalimbali vya wafanyakazi ili kufikia muafaka na kuweka msingi bora na mzuri ambao utakubalika na hao wastaafu katika eneo kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo niliyochangia, naunga mkono hoja. Nakushukuru sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kakunda.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa nafasi hii. Nianze kwa kutoa pongezi nyingi kwa Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya hasa kwenye majimbo yetu. Kwa kweli tumeshuhudia ubora mkubwa sana kwenye sekta za elimu, afya, maji, mawasiliano, umeme na sekta nyingine nyingi za kijamii na

kiuchumi. Kwa hiyo, kwa kweli ni lazima tumpe maua yake Mheshimiwa Rais, anafanya kazi kubwa sana katika kuliongoza Baraza la Mawaziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii nitazungumzia maeneo muhimu kama matatu tu hivi, ambayo yanagusa wananchi wa Jimbo langu. Mradi wa kwanza ambao nitauzungumzia, ambao bado una changamoto kubwa sana kwetu ni mradi wa utekelezaji wa barabara, ambayo ni barabara kuu inayotoka Mwanza – Shinyanga – Nzega – Tabora – Ipole – Ruangwa – Makongolosi – Mbeya – Tunduma. Hii ni barabara kuu namba nane, wahandisi waliita *T8 (Trunk Road No. 8)* katika nchi hii, na ilipitishwa tangu mwaka 1980, na ilianza kujengwa tangu mwaka 1984 pale Mwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka leo hii nasimama hapa Bungeni, barabara hii haijakamilika kujengwa tangu mwaka 1984 mpaka leo, na kipande ambacho hakijajengwa ni vipande viwili vikubwa; kipande cha kwanza ni kutoka Ipole mpaka Rungwa kilometa 172 na kipande cha pili ni kutoka Rungwa kwenda Makongorosi, zaidi kilometa 200.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ina vipande viwili vikubwa; kipande cha kwanza kutoka Ipole mpaka Mpanda kimekamilika, naipongeza Serikali kwa hatua hiyo; kipande cha pili *T*23 kutoka Rungwa kwenda Mkiwa kupitia Itigi nacho hakijakamilika. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, alipokuwa Singida alitoa agizo kwa Wizara ya Ujenzi kwamba wafanye mbinu zozote, mikakati yoyote iwayo ili waweze kuijenga barabara hii na ikamilike kwa ukamilifu wake, kwa maana ya barabara hii ya *Trunk Road Number 08* pamoja na vipande vyake viwili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma sana Ilani zetu za Uchaguzi za Chama cha Mapinduzi, tangu mwaka 2000 barabara hii imetajwa itajengwa kwa kiwango cha lami, Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2000, Chama cha Mapinduzi kilisema kwamba Serikali itatenga fedha za ndani kwa ajili ya kujenga barabara za lami ili

kuunganisha makao makuu ya mikoa yote nchini ifikapo mwaka 2010. Hii tunaizungumzia ni ya tangu mwaka 2000, lakini, mpaka leo hii, hapa ninapozungumza Makao Makuu ya Mkoa wa Tabora na Makao Makuu ya Mkoa wa Mbeya haijaungwanishwa. Kwa hiyo, hii Ilani ya Uchaguzi wa mwaka 2000 haijatekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005 ilitaja pia, Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2010 ilitaja pia, Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2015 ikataja tena, Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2020 ikataja tena, lakini mpaka leo hii nasimama hapa Bungeni utekelezaji bado haujakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutojengwa kwa barabara hii kumeleta hasara nyingi katika nchi. Nitataja hasara chache hapa. Moja, ni kufungwa kwa Kiwanda cha Nguo cha Mbeya *(Mbeya Textile)* ambacho kilikuwa kinapata pamba kupata maeneo ya Mbeya, Chunya, lakini baada ya Serikali kupiga marufuku ukulima wa pamba katika Mkoa wa Mbeya kwa sababu ya wadudu wekundu kiwanda kikakosa pamba, na barabara ya kutoka Tabora mpaka Mbeya ikawa haipo kuweza kuhudumia kiwanda kile. Kwa hiyo, kiwanda kimefungwa kwa sababu barabara hii haijajengwa. Hii ni hasara kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, usafirishaji wa mazao ya biashara na mazao ya chakula baina ya maeneo haya nao umeathirika vibaya kwa sababu barabara hii haijajengwa. Usafiri na usafirishaji wa bidhaa umekuwa wa gharama kubwa kwa sababu barabara hii haijajengwa na wakati wa mvua inakuwa inakatikakatika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano mwaka huu, barabara hii katika eneo la Ipemba - Mpazi ilikatika vipande vinne, maeneo manne yalikatika kabisa, na kwa hiyo, hakukuwa na usafiri kati ya Kata ya Kitunda na Makao Makuu ya Wilaya ya Sikonge. Kwa hiyo, kati ya Mbeya na Tabora mawasiliano yalikatika na kwa sababu hiyo ikabidi mtu kama anasafiri kutoka Mbeya kuja Tabora lazima apite Katavi. Kutokana na hilo, gharama za usafiri kutoka Mbeya

mpaka Tabora zilipanda kutoka shilingi 40,000 mpaka shilingi 70,000. Kutoka Kitunda kuja Sikonge ni shilingi 10,000 lakini gharama za usafiri zilipanda kutoka shilingi 10,000 mpaka shilingi 30,000. Ni adha kubwa sana kwa wananchi wa Sikonge, Tabora na Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Serikali itekeleze maelekezo ya Mheshimiwa Rais kama ambavyo alikuwa ameyatoa hadharani kwenye mkutano wa pale Singida.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ni kengele ya kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 22 Oktoba, 2008 Rais Kikwete alitembelea barabara hii, alitaka kwenda Kitunda akakwama njiani kwenye tope kwa sababu ya barabara hii kutojengwa. Akaagiza kwamba anataka barabara hii ipitike muda wote wa mwaka. Ndipo mwaka 2010 alipotembelea Sikonge kwa mara ya pili akapita kwenye barabara hiyo ambayo ilijengwa kwa kiwango cha kupitika kwa mwaka, lakini mwaka huu imerudi kuharibika tena vibaya sana. Ninaomba sana Wizara ya Ujenzi itakapoleta bajeti yake, isisahau kabisa barabara hii kwa sababu ya umuhimu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo naomba wasisahau, ni kwamba barabara nyingi sana za vijijini katika Jimbo la Sikonge zimeathirika vibaya sana kwa mvua za mwaka huu. Nilikuwa naomba mpango maalum wa matengenezo ya barabara za vijijini uweze kutekelezwa na Serikali kabla ya Bunge hili la Bajeti halijaisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu ambalo napenda kuzungumzia, sisi tuna mradi wa kilimo cha umwagilia pale Sikonge katika Bwawa la Uluwa. Bwawa hili la Uluwa lilichimbwa kama utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashamba uliokuwa unatekelezwa mwaka 1975 baada ya Azimio la Iringa la Halmashauri Kuu ya Taifa ya *TANU*, ambalo lilisitiza kaulimbiu ya siasa ni kilimo. Mpango huu ulianza kutumika mwaka

1975, bwawa likachimbwa na lilizinduliwa na Mwalimu Nyerere mwaka 1977.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya uzinduzi wake, Mwalimu Nyerere siku ile aliagiza kwamba sasa Wizara ya Kilimo itekeleze ujenzi wa miundombinu ili wananchi waanze kunufaika na kilimo cha umwagiliaji. Kwa bahati mbaya sana mwaka 1978 tukaingia kwenye vita na nchi ya Uganda. Kwa hiyo fedha nyingi zikaelekezwa kwenye vita, mradi huu hatukuupata. Mradi huu ulianza kutekelezwa mwaka 2006/2007 kwa Serikali kutoa zaidi ya shilingi bilioni 379. baada ya mradi kuanza, ulipoonekana kwamba unachota kama hekta 500 kutoka kwenye eneo la hifadhi ambalo ni hifadhi ya Halmashauri, watu wa maliasili wakauzuia huu mradi. Serikali imeingia gharama, lakini watu wa maliasili wameuzuia huu mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Mawaziri kama watano hivi ambao tumewapeleka pale, akiwemo Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, Mheshimiwa Profesa Maghembe, Mheshimiwa Dkt. Ramo Makani pamoja na Mheshimiwa Maige. Wote walipotembelea pale wakauliza kwamba sasa kuna shida gani? Kuna tatizo gani Serikali imeshindwa kwa miaka yote kuwaruhusu wananchi watumie hekta 500 tu waweze kufanya kilimo ambacho kinampa heshima Mwalimu Nyerere?

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba sana kupitia Bunge lako hili Tukufu, Serikali hasa Wizara mbili; Wizara ya Kilimo na Wizara ya Maliasili, wakae pamoja, waje Sikonge, waturuhusu tuweze kutumia huu mradi kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wetu. Ilikuwa ni hayo tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ya Waziri Mkuu. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo wa Kiti.

## MWONGOZO WA SPIKA

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa *Chief Whip*, Mwongozo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na natumia Kanuni ya Mwongozo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa Bungeni leo, wakati wanachangia Mheshimiwa Esther Matiko ameeleza mambo mazito. Masuala haya aliyoyaeleza yanahusu uhai wa Watanzania. Katika maelezo yake wakati akiendelea alisema pia kwamba ni kama Mheshimiwa Naibu Waziri alikuwa anafanya mzaha katika jambo hilo. Kama Serikali, wote tunafahamu kwamba Serikali ya Awamu ya Sita tangu imeingia madarakani suala la haki jinai, ili kuhakikisha Watanzania wanakuwa salama, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amelipa kipaumbele kikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tukiacha tu jambo hili likaisha hivi lilivyo, nadhani kwa kazi nzuri inayofanywa na Serikali, haitakuwa ni jambo jema. Wakati Serikali ikitoa maelezo kupitia Mheshimiwa Naibu Waziri, imeeleza kwamba taarifa hizi zimefika Serikalini na Mheshimiwa Mbunge amesema. Tunachofahamu ndani ya Serikali ni kwamba, suala hili limeanza kufanyiwa kazi kwa kiasi kikubwa na kiasi cha kutosha ili kuhakikisha uhai wa Watanzania unalindwa kwa gharama kubwa sana na Serikali ya Awamu ya Sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba mwongozo wako, ili Serikali isiunganishwe katika mtazamo wa kutokujali uhai wa Watanzania; na kwa kuwa, Mheshimiwa Mbunge ameingia hapa akiwa na *document* ambazo anasema ni za ushahidi ambazo sisi ndani ya Serikali hatuna, na sisi ndani ya Serikali jambo hili tulishaanza kulichukulia kwa uzito kupitia Wizara ya Kisekta, na Mheshimiwa Mbunge ametuambia kwamba alishaleta jambo hilo ndani ya Serikali na Serikali inaendelea nalo; naomba kama Kiti chako kitaridhia na kanuni zinaruhusu, basi kabla hatujaingizwa

katika mtazamo huo wa kutokutenda haki na kujali uhai wa watu, tupatiwe hizo taarifa ili ziwe ni sehemu ya shughuli inayoendelea ndani ya Serikali ya kulifanyia jambo hili utaratibu wa kiutafiti, ili kuwa na mwisho mzuri utakaosaidia kukomesha jambo hilo kama itaonekana lipo. Hivyo basi, Bunge hili liwe limemtendea haki Mbunge na pia liwe limeitendea haki pia Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Mwongozo wako. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa *Chief Whip*, ahsante. Ni kweli Mheshimiwa Rais aliunda Tume ya Haki Jinai na Tume hii ilipewa muda, wakaomba waongezewe na Rais akakubali kutokana na uzito wa changamoto ambazo zipo. Tume hii imeshawasilisha taarifa yake kwa Mheshimiwa Rais, na changamoto hizi zinaanza kufanyiwa kazi.

Pamoja na hayo, Mheshimiwa Matiko amewasilisha Mezani kwangu nyaraka za uthibitisho za ushahidi ambao anao. Serikali mtakabidhiwa nyaraka hizi ili mzifanyie kazi. Mtakapokuja kutoa maelezo yenu muwe na majibu ya kuwa mmefanyia kazi vipi na kueleza umma ukweli ulivyo, kama unavyofahamu kwamba Mheshimiwa Rais yuko tayari kumchukulia hatua mtu yeyote ayatakayebainika amekiuka taratibu za haki za watu kwenye Taifa letu. *(Makofi)*

Madhumuni ya kuweka tume hii ni kubainisha changamoto na vilevile kuwachukulia hatua watu ambao wanaharibu jina la Rais na jina la Serikali kwa masilahi yao kama hizo tuhuma zitakuwa ni za ukweli. Kwa hiyo, nakala zimekuja mbili, moja itakabidhiwa Serikali na moja itabaki katika Ofisi ya Spika kwa kazi za Kibunge. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, jioni tutaanza na Mheshimiwa Esther Malleko, Mheshimiwa Nicodemas Maganga na Mheshimiwa Hassan Mtenga.

Sasa nampisha Mheshimiwa Spika kwa kazi nyingine ya ziada kuja kumalizia mpaka hapo saa saba. *(Makofi)*

*Hapa Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alikalia Kiti*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimempokea hapa Mheshimiwa Naibu Spika kwa ajili ya kazi moja ambayo ipo kwenye Orodha ya Shughuli za Leo. Nitaifanya hiyo kazi moja halafu tutasitisha shughuli za Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, kama inavyoonekana kwenye orodha ya shughuli leo kuna shughuli ya Uchaguzi wa Wenyeviti wa Bunge. Kanuni ya Saba ya Kanuni za Bunge imeelezea uwepo wa wenyeviti watatu wa Bunge ambao huongoza vikao kwa utaratibu na maelekezo ya Spika au Naibu Spika na Kanuni za Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 13(2) imeelezea nyakati mbalimbali ambapo uchaguzi unaweza kufanyika, mojawapo ikiwa ni mara baada ya Kiti cha Mwenyekiti wa Bunge kuwa wazi kwa sababu yoyote isiyohusiana na Bunge kuvunjwa. Mtakumbuka kuwa tarehe 30 Agosti, 2023 katika mabadiliko ya Baraza la Mawaziri, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alimteua aliyekuwa Mwenyekiti wa Bunge, Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile kuwa Naibu Waziri wa Uchukuzi. Vilevile, tarehe 31 Machi, 2024 Mheshimiwa Rais alimteua aliyekuwa Mwenyekiti wa Bunge, Mheshimiwa Daniel Baran Sillo kuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Kwa muktadha huo nafasi mbili za wenyeviti wa Bunge zipo wazi.

Waheshimiwa Wabunge, kutokana na nafasi mbili za wenyeviti kuwa wazi na msingi wa masharti ya Kanuni ya 13 na taratibu zetu, siku ya Ijumaa tarehe 5 Aprili, 2024 Kamati ya Uongozi ilikutana na kwa kauli moja ilipendekeza majina mawili ya Wabunge wenzetu yawasilishwe Bungeni ili wathibitishwe kuwa Wenyeviti wa Bunge. Majina yaliyopendekezwa ni Mheshimiwa, Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mwenyekiti wa Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria na

Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mwenyekiti wa Kamati ya Biashara, Kilimo na Mifugo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia napenda kuwakumbusha kuwa Bunge letu lilishaweka utaratibu kwamba katika chaguzi zinazofanyika hapa Bungeni, iwapo idadi ya wagombea inalingana na nafasi zilizopo na vigezo vinavyohitajika vimetimizwa, basi wagombea hao wanapita bila kupingwa. *(Makofi)*

Utaratibu kama huu ulitumika kwenye uchaguzi wa Wenyeviti Wabunge katika Bunge la Kumi, Bunge la Kumi na Moja, na Bunge hili la Kumi na Mbili linaloendelea ambapo Kamati ya Uongozi ilipendekeza majina yanayolingana na nafasi zinazogombewa na baadaye majina hayo yalithibitishwa na Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa nafasi zilizopo wazi ni mbili, na kwa kuwa, Kamati ya Uongozi imependekeza majina mawili, Bunge hili katika kikao cha leo tarehe 08 AprilI, 2024 linaombwa kuwathibitisha Wabunge hawa kuwa Wenyeviti wa Bunge ili kupata uamuzi wa Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ili tuwe tumefanya maamuzi, inabidi niwahoji kuhusu kuwathibitisha Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria na Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo waweze kuwa Wenyeviti wa Bunge.

*(Hoja ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge. Baada ya kuwahoji, sasa hayo ndiyo maamuzi ya Bunge, leo tumewachagua ndugu zetu hawa wawili, Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama na Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika kuwa Wenyeviti wa Bunge. Mimi na Mheshimiwa Naibu Spika tunawakaribisha kwenye safu ya Uongozi wa Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu hao ambao tumewachagua wapo humu ndani, basi mruhusu angalau wawashukuru kwa kura mlizowapa leo kila mmoja kwa dakika moja tafadhali. Tutaanza na Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama.

**MHE. DKT. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kutoa shukurani zangu za dhati kabisa kwako Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson; Naibu Spika, Mheshimiwa Azzan Zungu; Kamati ya Uongozi kwa maana ya Wenyeviti wote wa Kamati za Kudumu za Bunge; Makamu Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge; na kwa namna ya pekee sana kwa Waheshimiwa Wabunge wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa imani ambayo wamekuwa nayo kwangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitoe ahadi kwamba nitajitahidi kwa kadri nitakavyojaaliwa na Mwenyezi Mungu kutekeleza jukumu hili muhimu sana kwa heshima ya Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa heshima ya Taifa letu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema kusimama hapa mbele ya Bunge lako Tukufu kuweza kusema machache.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nitoe shukrani zangu za dhati kwako, kwa Naibu Spika na Kamati nzima ya Uongozi wa Bunge letu kwa kulipitisha jina langu kwenye kikao chetu ili niweze kuletwa hapa ndani na kupigiwa kura au kukubaliwa kuwa Mwenyekiti wa Bunge siku hii ya leo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa miongozo mbalimbali pamoja na Naibu Spika, ambayo mmekuwa mkinipa, hata nikaweza kuonekana kwamba naweza nikafanya kazi kubwa zaidi ya hiyo ambayo nilikuwa nikiifanya. Kwa namna ya pekee,

nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wa Bunge hili kwa namna ambavyo wameonesha hapa kwamba wana imani kubwa nami katika kushika nafasi hii ya kuliongoza Bunge katika kumsaidia Spika na Naibu Spika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitoe ahadi kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwamba nitaifanya kazi hii kwa weledi na kwa uadilifu mkubwa nikizingatia kanuni, taratibu na sheria zote ambazo zinatawala uendeshaji wa Bunge hili na nikizingatia Kanuni ambazo hazijaandikwa za kuwa *fair*. Baada ya kusema hayo nawashukuru tena, naomba Mwenyezi Mungu anisaidie. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunawatakiwa la heri katika nafasi hizo ambazo Waheshimiwa Wabunge wamewaamini kwazo.

Waheshimiwa Wabunge, yako matangazo mawili hapa. Kwanza tangazo la wageni. Wageni wangu saba ambao wanatoka Kampuni ya Bima ya *UAP Insurance Tanzania*, ambao wapo viwanja vya Bunge kwa ajili ya kutoa elimu ya Bima kwa Waheshimiwa Wabunge na Watumishi wa Ofisi wa Bunge, wako pamoja nasi hapa Bungeni. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, maonesho ya Kampuni hii yako nyuma ya Ukumbi wa Msekwa, lile eneo la wazi. Kwa hiyo, mnakaribishwa sana muende hapo mkajifunze kuhusu mambo ya bima na ambayo Kampuni hii inatoa. Tunawatakiwa kila la heri.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, tunasitisha Shughuli za Bunge mpaka saa 10.00, jioni leo. *(Makofi)*

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 10.00 Jioni)*

*(Saa 10.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae, ahsante sana. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Majadiliano yanaendelea, na kwenye orodha yetu tutaanza na Mheshimiwa Esther Edwin Malleko, atafuatia Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga na Mheshimiwa Hassan Seleman Mtenga, ajiandae.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ya kuanza mchango wangu wa jioni hii ya leo. Kwanza nitoe pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Rais wetu mpendwa Mama Samia Suluhu Hassan kwa namna anavyofanya kazi vizuri ya kutuletea maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza pia Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, Waheshimiwa Mawaziri wa Wizara na Naibu Waheshimiwa Mawaziri na Watendaji wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu. Kipekee naomba nichukue nafasi hii kukupongeza sana kwa kuendelea kuaminiwa, umetoka kwenye Uwenyekiti wa Kamati na sasa umekuwa Mwenyekiti wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa nimepata nafasi hii ya kwanza kuchangia, nichukue nafasi hii kukupongeza sana, tuna imani na wewe, chapa kazi, najua unaweza. Kipekee kabisa nampongeza Mheshimiwa Rais wetu mpendwa Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya. Katika miaka mitatu ya uongozi wake tumeona kazi kubwa aliyoifanya, alisema kazi iendelee na kweli tumeona kazi inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona ujenzi wa reli ya kati ya kilometa 1,219, Serikali ikiwa imetoa shilingi trilioni 10.6 tunaona kazi

inaendelea. Mradi wa kufua umeme wa Bwawa la Mwalimu Nyerere, kazi inaendelea, tumeona tayari *Megawatt* 2,115 zinazalishwa na tayari utekelezaji umefikia 96.8% katika mitambo tisa, mmoja tayari umewashwa na tayari *Megawatt* 235 zimeingia kwenye gridi ya Taifa na tunaona tatizo la umeme tayari limepunguzwa, kazi inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona uboreshaji wa Shirika la Ndege Tanzania kazi kubwa imefanyika, Mheshimiwa Rais tayari amelipa kiasi cha shilingi bilioni 753, ndege tatu zilizoagizwa, tayari mbili zimefika, moja itafika mwezi huu. Sasa tunakuwa na ndege 16 katika Shirika letu la Ndege la Tanzania. Kazi inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, Mheshimiwa Rais ameendelea kufanya kazi kubwa, mradi wa ujenzi wa bomba la mafuta ghafi kutoka Hoima - Uganda mpaka Chongoleani – Tanga kilometa 1,443, Serikali katika ushirika wake tayari imechangia katika mradi huo kiasi cha dola 268.7. Kazi inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, kazi inaendelea kufanyika Kiwanda cha Sukari cha Mkulazi, kimekamilika kwa 99%. Serikali imetumia zaidi ya shilingi bilioni 320.5, tayari kiwanda kimeanza kuzalisha na mpaka sasa kimezalisha tani 1,851, kinaenda kupunguza uhaba wa sukari nchini. Siyo hivyo tu, imeongeza ajira 1,996, kazi inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi zilizofanyika ni nyingi sana, hata nikisema hapa nitandelea kusema kwa muda mrefu, lakini nashukuru hata wenzangu wamechangia na kusema ni namna gani Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameendelea kufanya kazi ya kuwatumikia Watanzania na kuwaletea maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niende moja kwa moja kwenye jimbo langu la Mkoa wa Kilimanjaro. Katika Mkoa wetu wa Kilimanjaro shughuli za kiuchumi zinazofanyika ni pamoja na kilimo, biashara na utalii. Tunamshukuru sana Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuongeza bajeti ya kilimo. Leo nitaenda

kuzungumza zaidi kwenye kilimo kwa sababu wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro wanalima ndizi, kahawa na parachichi, lakini wana changamoto zinazowakabili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi kubwa iliyofanywa, na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuongeza bajeti na kuwapatia Maafisa Ugani pikipiki, bado kuna changamoto zinazowakabili wananchi wetu, hasa wakulima wanawake wa Mkoa wa Kilimanjaro. Katika changamoto hizo, ya kwanza ninayoweza kwenda kuisemea siku ya leo ni changamoto ya mbegu bora au miche bora. Hii imekuwa ni changamoto kubwa sana kwa wakulima wetu. Kwa kuwa hawapati mbegu bora au hiyo miche bora, wanaenda kufanya kilimo ambacho kinakuwa hakina mazao yanayokidhi vigezo, wanakosa thamani kubwa au faida kutokana na kile wanacholima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa ninashauri, kwa kazi kubwa iliyofanyika, Maafisa Ugani waweze kuwatembelea wakulima wetu, waweze kufanya utafiti, waweze kujua afya ya udongo na kuwashauri akinamama na wakazi wa Mkoa wa Kilimanjaro ambao wanafanya kilimo ili waweze kulima kilimo cha kisasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nilikuwa nataka kuishauri Serikali ambayo ni changamoto kwa wakulima wetu wa Kilimanjaro ni utegemezi wa mvua za msimu. Mpaka leo sisi tunategemea mvua za msimu. Ina maana kama mvua za msimu hazipo, watu wanakuwa hawapati mavuno yale ambayo walikuwa wanategemea, wanayostahili. Nilikuwa nashauri, Serikali sasa ifuatilie kwenye suala la kilimo cha umwagiliaji, waweke mabwawa ya kutosha. Mvua zinanyesha na kuleta athari kwa wananchi na wakati mingine mpaka mafuriko. Kwa nini basi Serikali isione namna ya kutumia maji haya kwenda kwenye kilimo cha umwagiliaji na wananchi wetu wakaweza kupata faida ya kutosha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni elimu kwa wananchi, hawa wakulima ya namna ya kuongeza thamani ya ubora wa mazao yao. Hii imekuwa ni changamoto kubwa sana kwa wakulima

wetu kwa sababu, unakuta katika mazao wanayolima hasa zao la kahawa, wakulima wale wanauza kahawa ghafi na wanaenda kuuzia nchi ambazo hazina hata mti mmoja wa kahawa katika nchi yao. Nao wanachofanya ni kwenda kuongeza thamani kidogo tu, lakini wanapata faida mara tatu mpaka mara tano ya faida anayopata mkulima ambaye anateseka tangu anapoanza kupanda mti huu mpaka anapovuna. Kwa hiyo, Serikali iweke jicho lake kwenye sehemu hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kusema jambo lingine ambalo linawakwamisha wananchi au wakulima wa Kilimanjaro ambalo ni soko la ndani na nje. Bado tumekuwa na shida kubwa sana ya kupata masoko kwa ajili ya bidhaa zetu. Kama ndizi zetu akina mama wa Kilimanjaro tunataka kuona zinaenda nje ya nchi, zisiishie kupelekwa Mabibo, zisiishie kutengeneza mtori, ziweze kwenda mbali zaidi ili kuwaletea wananchi wetu mafanikio makubwa. Tumeona Mheshimiwa Mama Samia Suluhu ameleta ndege za mizigo, ndege hizo basi zikatumike kwenda kuchukua mazao yetu kutoka Kilimanjaro na kupeleka nje ya nchi na sisi tuweze kujipatia faida na fedha za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo linawakwamisha wakulima wetu ni kutokana na kutokuwa na takwimu sahihi za idadi ya wakulima. Leo ukitaka kuwahudumia watu ni lazima ujue idadi yao. Kama ambavyo nchi inataka kuwahudumia wananchi hawa inafanya sensa, lakini leo hawajui wakulima wapo kiasi gani? Wakulima hawa wanalima kwa kiasi gani? Wakulima hawa wana mashamba kiasi gani? Je, kama tunahitaji mbolea, pembejeo na miche, wanawezaje kujua kama hawajui idadi ya hawa wakulima? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali iangalie ni namna gani itapata takwimu sahihi za wakulima wa kahawa, wakulima wa ndizi, wakulima wa parachichi, wakulima wa maua ili kuweza kuwapa stahiki zao pale wanapokuwa wanahitaji pembejeo na mbolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie na suala la 4:4:2,…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kidogo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa hitimisha kidogo muda wako umeisha, tafadhali.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wetu wa Kilimanjaro wanataka kusikia Serikali inasema nini juu ya fedha inayotoka halmashauri ile ya 10%, kwani wamekaa wakisubiri kwa muda mrefu. Tunajua Serikali inafanya mikakati na mipango ya kuweza kuboresha, lakini basi waweze kupewa taarifa ni lini fedha hiyo inatoka na Serikali itoe tamko ili akina mama wa Kilimanjaro nao waweze kufaidika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Malleko, ahsante sana. Sasa namkaribisha Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga, atafuatiwa na Mheshimiwa Hassan Seleman Mtenga na Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris ajiandae.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu yenye bajeti ya shilingi 350,988,000,000. Awali ya yote, napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu, Muumba wa Mbingu na nchi kwa siku ya leo tena kuweza kupata nafasi ili niweze kuishauri Serikali pamoja na kuwakilisha jimbo langu la Mbogwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kukupongeza wewe kwa kuweza kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti. Mungu akusaidie, akusimamie ili uweze kutuongoza vyema. Namshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa niaba ya wananchi wa Mbogwe, kweli kabisa Mbogwe sasa hivi inaanza kuonekana kwenye ramani ya dunia, mwanzoni ilikuwa haionekani. Namshukuru Mheshimiwa Rais kwa sababu zipo barabara ambazo zilikuwa hazipitiki kabisa, lakini kwa sasa zimeanza kupitika. Pamoja na yote, kuna siku niliwahi kuomba taa za barabarani, nashukuru ninawasiliana na watu wangu waliopo huko Mbogwe wanasema kazi inalendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na shukurani zote, nijikite kwenye kuishauri Serikali kwa sababu muda ni mchache. Kweli Serikali inafanya mambo mengi, inajenga mashule, inatengeneza barabara, inafanya shughuli nyingi kila mtu anaona, lakini unaweza ukafanya mambo mengi ukafeli kwa vitu vidogo. Wapo watu ambao wanamchonganisha Mheshimiwa Rais kwenye hii miradi jinsi inavyotekelezwa. Hii kauli ya kusema kwamba kila mwananchi ahusishwe kuchangia kwenye kila miradi inayotolewa, kwenye jimbo langu imeleta changamoto hasa miradi ya *TASAF*. Utakuta mwananchi anaambiwa kusomba mawe, kusogeza kokoto, kusogeza moramu; sisi wote huwa tunajenga nyumba, lakini kiuhalisia ukija kuifanya hesabu, pesa zilizotumika unaona kama kuna ujanja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, natumia nafasi hii kuiomba Serikali kwamba huu mfumo wa kuwashirikisha wananchi kusomba mawe, kusomba maji na kufanya shughuli za miradi zinazotolewa na Serikali zinaharibu *image* ya Serikali na kuonesha kama wananchi wanateswa kwa sababu wanashinda kwenye miradi hasa miradi ya *TASAF*. Miradi ya *TASAF* inasumbua sana ndugu zetu, unakuta akina mama wanafanya kazi usiku na mchana na baadaye hata malipo yanakuwa ni shida, mara wanaambiwa uwe na namba ya simu, mara mitandao sijui inagoma, wakati bibi zetu wanashinda wanachonga barabara. Kwa hiyo, ili Serikali ilione la maana sana

kuweza kuliondoa, Serikali ifanye mambo yake yenyewe tu na wananchi waweze sasa kustarehe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inakuwa ni karaha ambapo miradi inakuja kijijini halafu mnaanza kuambiwa kusomba mawe, kusomba matofali halafu unakuta pesa zimetolewa shilingi milioni 450. Kiuhalisia ukija kufanya hesabu, hata kama hujasoma unakuta wananchi wameibiwa. Ifikie wakati sasa Serikali iwapunguzie wananchi mizigo, kwa sababu wananchi wapo tayari kulipa kodi, wapo tayari kulipa tozo, wapo tayari kufanya kila aina ya kazi. Sasa iwapumzishe ili wafanye mambo yao mengine ili kusudi Serikali iendelee kutimiza vizuri miradi kama alivyodhamiria Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la maboma. Juzi niliuliza swali hapa nikaambiwa zimetengwa shilingi bilioni 450, nashukuru lakini kwangu bado sijaziona kwenye Wilaya yangu ya Mbogwe. Tunayo maboma 74 katika Wilaya ya Mbogwe, ambayo ni ya afya, shule za sekondari na maboma ya shule za msingi. Naiomba sana Serikali, kabla hatujaingia kwenye uchaguzi mdogo mwaka 2024/2025, iende ikayaezeke haya maboma kwa sababu wananchi waliumia, waliuza kuku wengine wakajenga haya maboma. Sera ya Serikali ilikuja ili kila Kijiji kiwe na zahanati na wananchi wakajitahidi wakafanya hayo mambo. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali yangu iende kukamilisha maboma hayo ili mwaka 2025 tusipate tabu kuomba kura kwa wananchi. Ombi langu kubwa sana ni hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala lingine tunashukuru Mungu, mwaka 2023 kweli barabara zilichongwa, lakini kwa neema ya Mungu mvua zimenyesha, barabara zimesombwa zote na maji. Kwenye Wilaya yangu ya Mbogwe kuna njia hazipitiki, ipo Kata ya Ushirika, ipo Kata ya Nanda, kuna Kata ya Ikundigazi, kuna Kata ya Isebya, hali siyo nzuri. Naomba sana Serikali kwenye hizi fedha walizoomba *TARURA* kwa ajili ya kurekebisha Barabara, itoe haraka iwezekanavyo kabla Bunge hili halijaisha ili kusudi barabara ziende kutengenezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ninaloliomba hapa kwenye Wilaya ya Mbogwe, miradi ya Serikali kutokukamilika kwa wakati. Mwanzoni wakandarasi walikuwa wakifanya kazi, shughuli zilikuwa nzuri, shughuli zilikuwa na ubora. Hizi *force account* miradi inasimamiwa na wataalam, ni kelele tupu. Tumemwona hapa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye ziara zake pamoja na Mheshimiwa Makamu wa Rais, unakuta mtu alisomea kilimo, wakati huo anasimamia jengo, ni injinia. Matokeo yake tunatumia pesa nyingi ambapo tunakuwa tunafanya na watu wengine ambao sio *professional* wa ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tungerudi kwenye miaka ile ya nyuma jinsi walivyokuwa wakitengeneza wakandarasi, ambapo miradi ilikuwa inatengenezwa yenye uimara kuliko ilivyo hivi sasa, kila sehemu ni kelele. Wataalam wanakula fedha, mainjinia wanakula fedha, tunakalia kugombana na kutokufanya shughuli nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, naiomba Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa vile yenyewe sekta zote zinawahusu katika namna ya uendeshaji wa vikao, basi Bunge na vikao vya halmashauri vitengenishwe, kwa sababu muda mwingi Waheshimiwa Wabunge tunakuwa Bungeni, halafu tutakuta mambo yameshafanyika vibaya huko kwenye halmashauri. Mfano, mimi eo ni mwezi wa tatu sijakaa kwenye Baraza la Halmashauri, ukitembea kwa wananchi ukifanya mikutano unakuta kuna kero ambazo zimetengenezwa na wenzangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria zinasema, ukikuta wenzako wameshamaliza kupitisha jambo, hutakiwi kulipinga. Kwa hiyo, Serikali ione kila namna kuvitofautisha vikao ili wakati wa Bunge uwe wa Bunge tu, ili wakati wa Baraza la Halmashauri kule Waheshimiwa Wabunge tuweze kushiriki ili hata wananchi wanapotuhukumu, watuhukumu katika kweli. Sasa hivi mambo mengi yanafanyika Wabunge hawapo kwenye majimbo yao, matokeo yake ni kupata hati chafu pamoja na kuonekana kwamba labda Mbunge hafai hasa unapokuja ugeni wa kitaifa Mbunge unaanza kuulizwa maswali mengine ambayo unakuta wenzio walishapitisha kitu kingine. Kwa

hiyo, Serikali ilione hili suala la umuhimu, kuweza kutofautisha vikao vya Bunge na vikao vya halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine hapa ni kwa watu wastaafu. vikokotoo, nimepokea kero nyingi sana kutoka kwa watu walioitumikia Serikali. Suala hili la vikokotoo ikiwezekana tuliondoe kabisa kwa sababu, linatengeneza chuki kuanzia kwetu sisi Wabunge tunaotunga Sheria. Kila mstaafu ambaye yuko jimboni kwangu amenifikia kulalamika kwa hiyo, ninaiomba Serikali pamoja na Bunge tulipitie upya suala hili tuliondoe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, nizungumze kidogo kwa vile huu ni mwaka wa uchaguzi, tumepitisha hapa Sheria ya Vyama vya Siasa pamoja na mambo mengine. Namwombea Mheshimiwa Rais, kwa roho yake ya upendo kabisa, aendelee kusimama na Mungu hivyo hivyo. Nami nasema, tuko tayari kwa mapambano 2024/2025, afe kipa afe refa, lakini cha msingi, wale watakaoteuliwa kusimamia hizi chaguzi, wawe na hofu ya Mungu kama alivyo Mheshimiwa Rais, ili kuhakikisha kiongozi wanayemtaka wananchi huyo ndiye asimame, kusiwepo tena na ujanja wa kubebana. *Term* hii hakuna kubebana. Naiomba sana Serikali ikae kimya, sisi tulioko majimboni watuache tupambane wenyewe, na kila mtu atatoboa kivyake na tutakutana hapa tena mwaka 2026. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa vile anavyoruhusu kila jambo ambalo tunalitaka. Mimi binafsi nimekuwa na maombi mengi, lakini ananisaidia. Kwa hiyo, hili la kisiasa alione ni la maana sana, achague watu…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa hitimisha hoja yako, uko nje ya muda.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nahitimisha hoja yangu kwa kumwombea Mheshimiwa Rais ili haki itendeke 2024/2025 na kazi iendelee. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Maganga. Mheshimiwa Hassan Seleman Mtenga amepata dharura ya kikazi. Kwa sasa ni Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris atafuatiwa na Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri na baada ya hapo atakuja Mheshimiwa Minza Simon Mjika.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ya Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu iliyopo mbele yetu. Kwanza nitumie nafasi hii kukupongeza wewe binafsi kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Bunge. Tunaamini uzoefu wako kwenye mambo ya sheria na uzoefu wako wa kibinadamu wa mahusiano yako na Wabunge wenzako utakuwa ni chachu ya kuweza kumsaidia Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wenzako katika kuongoza shughuli za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri Jenista Mhagama na wasaidizi wake, vilevile Mheshimiwa Ndejembi na msaidizi wake kwa kazi kubwa ya kumsaidia Mheshimiwa Waziri Mkuu katika utekelezaji wa majukumu yake ya kila siku. Sisi Wabunge wote ni mashuhuda, Waziri Mkuu kupitia Ofisi yake na ninyi wasaidizi wake, mmekuwa ni wasaidizi wazuri kwa Mheshimiwa Rais kwa kutimiza majukumu yenu ambayo ni dhamira ya Mheshimiwa Rais kutupeleka Watanzania katika maisha safi, maisha yenye hadhi na ubora katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo anaifanya kwa Watanzania. Sisi Wabunge wote ni mashuhuda, kila Mbunge anayesimama anampongeza Mheshimiwa Rais. Wako watu wanaona wivu, ni kwa nini tunampongeza? Kwa uhalisia sisi tulioko ndani ndio tunajua ni yapi Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu

Hassan ameyafanya kwa Watanzania katika majimbo yetu na wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la elimu, kule jimboni kwangu mambo ni mazuri. Tuna shule ya vipaji maalum imejengwa kwa thamani ya karibu shilingi 3,700,000,000 madarasa yamekuwa mengi kwenye shule ya msingi na shule ya sekondari. Kwenye masuala ya umeme, vijiji vyote vimepata umeme na sasa hivi tunaelekea kwenye vitongoji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye barabara, kazi imeendelea kufanyika. Juzi, tarehe 5 mwezi wa pili, barabara ya Bigwa – Kisaki yenye urefu wa kilometa 78 imetiwa saini kwa ajili ya ujenzi wa kiwango cha lami kwa gharama ya shilingi bilioni 134. Tuna kila sababu ya kumpongeza Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo kwa Mheshimiwa Rais, nitumie nafasi hii kuishauri Serikali yangu. Kuna suala hapa la utalii, yaani ongezeko la watalii, na kubwa zaidi ni kutokana na jitihada za dhati za Mheshimiwa Rais kupitia *Royal Tour*. Mwaka 2022 tumeona watalii walikuwa ni 1,459,920 lakini mwaka 2023 watalii wameongezeka mpaka kufikia 1,808,205 ni ongezeko *almost* la asilimia nane. Tuna kila sababu ya kumpongeza Mheshimiwa Rais, lakini vilevile ukiangalia mapato ya utalii mwaka 2022 yalikuwa ni dola bilioni 2.53, lakini mwaka 2023 yamekuwa ni dola bilioni 3.37. Tuna kila sababu ya kumpongeza Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu tumeambiwa kwamba pamoja na jitihada hizi zote za dhati zinazofanywa na Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar, bado kupitia filamu ya *Jing Dong* tunatarajia kupata watalii wengi kutoka China. Sasa ushauri wangu kwa Serikali ni kwamba, ukijaribu kuangalia mapato haya ya utalii yanatoka Ukanda wa Kaskazini, lakini bado kuna Ukanda wa Kusini na maeneo mengine ya nchi yetu ambayo yana vivutio vikubwa vya utalii. Mfano, Morogoro tuna

Hifadhi ya Mwalimu Nyerere, Mikumi na Udizungwa, ukienda Iringa kuna Ruaha, ukienda Katavi kuna Hifadhi ya Katavi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina taarifa fupi kwamba kupitia Hifadhi ya Mwalimu Nyerere, mwaka 2022/2023 kulikuwa na wageni karibu 34,189 wa kutoka nje ambao walifika kufanya utalii kwenye hifadhi yetu, lakini wageni wa kazi walikuwa ni karibu 19,800 na wageni wazawa walikuwa 900 na *almost* watalii 54,000 walifika kwenye Hifadhi ya Mwalimu Nyerere ambapo mapato ya shilingi bilioni 11 yalipatikana. Ukijaribu kuangalia ongezeko la watalii, halafu ukiangalia sehemu moja ya Kusini utaona kwamba, bado Wizara ya Maliasili ina wajibu wa kuendelea kutangaza utalii wa Nyanda za Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili nitoe pongezi kupitia Mradi *wa E-Grow,* ambao ni uboreshaji wa utalii upande wa Kusini. Tumeona kwenye Hifadhi ya Mwalimu Nyerere kuna ujenzi wa uwanja wa ndege. Ninakumbuka katika bajeti iliyopita nilipiga kelele kwenye hili, ujenzi wa uwanja wa ndege, lakini kupitia Mradi wa *E-Grow* safari hii uwanja wa ndege umejengwa kwenye lango la kutokea Matemere. Vilevile, kuna ujenzi wa *campsite* yenye uwezo wa watu 100, *rest house* yenye uwezo wa kulaza wageni 20, vilevile kuna ujenzi wa kambi za askari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwako kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, bado kuna changamoto kwenye lango la kupitia Matambwe – Kisaki ambayo ni *Morogoro DC*. Tunaomba Uwanja wa Ndege wa Matambwe uboreshwe ili kuruhusu watalii wengi waje na kuweza kutuletea fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna ujenzi wa madarasa. Katika kuunganisha hifadhi, bado kuna hiyo changamoto kwa hiyo, naomba kupitia Wizara ya Maliasili na Ofisi ya Waziri Mkuu, tuangalie ni jinsi gani tunaweza tukafanya jambo hili likamilike na ndiyo maana nimetangulia kusema tunamshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kujua umuhimu wa utalii kwenye Nyanda za Kusini, na hasa Hifadhi ya Mwalimu Nyerere, ameweza kuidhinisha

kujengwa kwa kiwango cha lami kilometa 78. Hiki ni kichocheo cha kutaka tupate watalii wengi na tupate fedha nyingi za kigeni ili tuweze kuendeleza uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nizungumzie suala la kilimo; mwaka 2023 nilizungumza na mwaka huu ninaomba nizungumze tena, watu wa Morogoro Mungu ametupa bahati, kuna zao la karafuu. Zao la karafuu kwa Zanzibar ndiyo limekuwa zao kuu la biashara, lakini Mungu ni mwema, sisi watu wa Morogoro vilevile tumepata bahati ya kuwa na zao la karafuu ambalo ninaamini mpaka tulipofika ni jitihada za uongozi wa Halmashauri ya Morogoro Vijijini na uongozi wa Mkoa na mwaka 2023 tuliweza kuvuna tani 2,200 ambazo ziliwapatia wananchi wa Morogoro zaidi ya shilingi bilioni 39.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa Serikali, kupitia zao hili kama Taifa upande wa Tanzania Bara, na lenyewe linaweza likaleta fedha nyingi za kigeni ambazo zitaingia kwenye shughuli za kuleta maendeleo kwa Taifa letu. Naiomba Wizara isimame, iungane na viongozi wa Mkoa ili ikiwezakana zao la karafuu nalo litangazwe kwamba ni zao la kimkakati katika kuleta mapato kwa wananchi wa Morogoro na Tanzania kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka nichangie ni suala la kodi. Mimi ni mfanyabiashara na ninaamini watu wengi wanaamini wafanyabiashara ni wezi au wanatamani sana kupata fedha ambayo siyo stahiki. Naipongeza Serikali yangu katika mwelekeo ambao imekujanao katika mwaka huu kuondoa kodi ambazo zimekuwa ni mzigo na zimekuwa ni sumbufu kwa wafanyabiashara kiasi cha kuwafanya washindwe kwenda mbele na kuweza kusaidia kuongeza pato kwenye Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona hapa katikati ya Julai mpaka Januari mwaka huu kwenye mapato ya Serikali za Mitaa yamefikia shilingi bilioni 17, *almost* 95.9%, lakini kwenye *TRA* kuna asilimia…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, hitimisha hoja yako, ahsante.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Innocent. Anafuata Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri, Mheshimiwa Minza Simon Mjika na Mheshimiwa Profesa Shukrani Elisha Manya wajiandae.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nichangie Hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwanza nianze kwa kutoa pongezi na kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anayofanya katika Taifa hili. Pia namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Mawaziri wote katika Wizara zao kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya ambayo Watanzania wanaifurahia. Pia, namshukuru Mheshimiwa Spika pamoja na Naibu Spika na ninyi Wenyeviti kwa kuliongoza vizuri Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, nitaanza kuchangia mchango wangu katika Sekta ya Maliasili na Utalii. Kwanza naipongeza Wizara ya Maliasili na Utalii, Watanzania wote tunaona jitihada ambazo mama anazifanya na jinsi ambavyo sasa hivi watalii wameongezeka katika Taifa letu na kuongezeka kwa fedha za kigeni. Pamoja na mafanikio haya mazuri, lakini kidogo kuna maeneo mengine yanakuwa na changamoto ambazo wananchi wanapata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao Mlima Kilimanjaro ambao umezungukwa na msitu ulio katika baadhi ya kata ikiwepo Kata ya Katangara Mbele. Kata hii imekuwa inakumbwa na tatizo la matukio mengi sana ya kuathiriwa na nyani wanaotoka katika msitu huu. Matukio haya yamekuwa yakijitokeza mara kwa mara na Wabunge wenzangu wa kutoka Kilimanjaro wamekuwa wakiongelea sana hili. Imefika mahali sasa nyani wale ambao wako katika msitu wetu wa

*TANAPA, KINAPA* pamoja na *TSF* wanakuja mpaka maeneo ya nyumba za watu na hata wakati mwingine wakikosa kitu cha kula wanachukua watoto wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la kusikitisha kwa sababu, hili lilitokea Rombo na Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo alifanya mawasiliano na Wizara, akamwita Waziri pamoja na Naibu Waziri na Katibu Mkuu. Walifika Rombo na walifanya mkutano na Wananchi wa Rombo na walitoa ahadi kwamba, watalimaliza tatizo hilo, sasa ni miaka miwili imefika bado halijatekelezwa. Ukweli ni kwamba, asilimia kubwa ya wanaoathirika ni wanawake kwa sababu, wamekosa amani, hawaamini kama wanaweza kumwacha mtoto kwa dakika tano bila kumwona machoni kwa sababu, hawajui usalama wake ukoje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo hiki kilitokea, mtoto alichukuliwa na nyani akapelekwa chini ya bonde. Wananchi waliokuwepo walikimbizana wakaenda kutafuta ndizi, walipopata ndizi wakarusha kule chini bondeni walikokuwa wale nyani, na kwa tabia ya nyani huwa wanapenda sana ndizi, kwa hiyo, yule nyani alimwacha mtoto akakimbilia ndizi ndipo wananchi walipoteremka chini ya bonde na kwenda kumwokoa mtoto. Inasikitisha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni nini Wizara itafanya kwa jitihada za haraka sana ili kuhakikisha kwamba wanawasaidia wale wananchi wanaoishi maeneo yale kuhakikisha kwamba nyani hao wanapotea katika maeneo yale ya makazi ya wananchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa unyenyekevu mkubwa, naiomba Serikali, natambua Mheshimiwa Rais, Dkt. Mama Samia Suluhu Hassan, anamjali sana mwanamke. Ninatambua mwanamke akikaa mahali kama hana usalama wa mtoto wake, hawezi kufanya chochote, anashindwa kufanya shughuli za uchumi, anashindwa kufanya shughuli yoyote, yeye ndiye anakuwa mlinzi wa mtoto. Kupitia Bunge lako, naomba Wizara ichukue hatua za haraka sana kuhakikisha inakomesha jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumaliza hilo nitaongelea tena Rombo kwenye upande wa barabara. Alikuja Makamu wa Rais wakati anafungua Hospitali ya Wilaya ya Rombo, akatoa ahadi kwamba atatengeneza barabara inayotoka Makao Makuu kwenda Hospitali ya Wilaya kwa kiwango cha lami, ambayo ina urefu wa kilometa tano tu. Ahadi ile mpaka leo haijakamilika. Naiomba Serikali kwa kuwa, huduma ya afya ni huduma inayohitaji barabara iwe nzuri, mwanamke anaweza akashikwa na uchungu akajifungua njiani kama barabara ni mbovu. Naiomba Serikali yangu sikivu, zile barabara ambazo zinapeleka huduma muhimu za jamii kama vile hospitali, Serikali izitilie maanani zitengenezwe kwa uharaka wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuongea habari ya barabara kwa maana ya ujenzi, nitaongelea habari ya uvuvi. Kilimanjaro tuna Bwawa la Kalemawe, ambalo liko Wilaya ya Same ya Mashariki. Bwawa hili lina urefu wa kilometa tatu na urefu wa mita 200. Bwawa hili lilijengwa kipindi cha Wakoloni wa Kiingereza. Lengo lao kubwa lilikuwa ni kuhakikisha kwamba wakulima na wafugaji hawaingii katika Hifadhi ya Mkomazi. Sasa bwawa hili limekuwa chakavu, bwawa hili sasa hivi limejaa matope, bwawa hili sasa hivi limejaa magugu, halina tena thamani ya kuitwa bwawa. Naiomba Serikali, ili kukuza uchumi wa wananchi wa eneo lile, ihakikishe inapeleka msaada wa haraka, kwanza wa kutoa yale magugu na pia, kuhakikisha kwamba bwawa linasimamiwa vizuri ili wananchi wa eneo lile waweze kupata samaki na kukuza uchumi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya bwawa hilo, narudi katika ziwa ambalo kila siku ninaliongelea na sitaacha kuliongelea mpaka litakapokamilika. Naongea kuhusu Ziwa Jipe, Mwanga. Nimeongea mara nyingi humu ndani na hata Mbunge wa Jimbo ameongelea Ziwa Jipe. Sijui shida iko wapi? Sijui ni nini kinakwamisha? Tunatambua wazi kwamba, Ziwa Jipe lina magugumaji mengi na yakitolewa, wananchi wa Mwanga watafaidika na samaki na watakuza uchumi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, viongozi wengi wanakwenda kufanya ziara pale na kila kiongozi anapofika anakutana na malalamiko ya wananchi katika mikutano. Mheshimiwa Mwenyekiti, hata juzi Mheshimiwa Makamu wa Rais Mheshimiwa Mpango, katika ziara yake ya Mkoa wa Kilimanjaro mwezi wa Tatu alikutana na hilo. Naona kila kiongozi anapopewa malalamiko anakubali, lakini utekelezaji wake haupo, haufanyiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali yako sikivu, wale wananchi wa Mwanga wanategemea kipato cha mchanga. Kule Moshi tunapokaa mchanga wetu unatoka Mwanga. Hawana kipato kingine zaidi ya mchanga, na Bwawa la Nyumba ya Mungu ambalo sasa hivi samaki wake ni wachache sana, na ni wadogo, kwa hiyo, hawana kipato kingine. Ili kuwasaidia wananchi wa Mwanga, naomba Serikali yako itoe kauli kwa wale wananchi wa Mwanga kwamba ni lini watatoa magugumaji ili nao waweze kuinua uchumi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nitachangia, ni kuhusu…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, hitimisha muda wako umekwisha tafadhali.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri. Sasa namwita Mheshimiwa Minza Simon Mjika, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Shukrani Elisha Manya na Mheshimiwa Anastazia James Wambura, ajiandae.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipatia nafasi ya pekee leo kuwa ndani ya Bunge hili. Mwenyezi Mungu atukuzwe sana. Vilevile napenda kumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano

wa Tanzania, Mama yetu Samia, Mungu azidi kumpa maisha marefu, hekima na busara nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi hii ya kuweza kuchangia bajeti hii ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri ambazo anafanya pamoja na Mawaziri wake. Namshukuru sana dada yangu Mheshimiwa Mhagama kwa kazi nzuri ambayo anaifanya, tunaona anavyopambana akiwa jimboni, anaitumikia Serikali yake na anafanya kazi nzuri pamoja na Mawaziri wake. Hongereni kwa kazi nzuri na Mwenyezi Mungu aendelee kuwapa afya njema ili kazi iweze kwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichangie upande wa elimu. Nashukuru kwamba Rais wetu ametupatia madarasa mengi nchi nzima takribani madarasa 23,000. Madarasa ni mengi na ni ya kutosha lakini tatizo ni moja, hakuna madawati. Japo tunajitahidi, lakini bado madawati ni changamoto. Tunaomba kwa upande wa elimu, madawati yaongezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna shule ambazo ni za muda mrefu, zimechakaa sana, kweli ukifika ukiona yale majengo mapya na hayo ya zamani, yaani hayapendezi na hata shule yenyewe haipendezi. Tunaomba majengo ya zile shule yakarabatiwe ili na zenyewe zionekane kuwa ni mpya na zinafaa. Hata wanafunzi wanaosomea yale majengo mara nyingi hawajisikii raha na wanalalamika sana. Hata tunapokuwa na vikao mbalimbali walimu wanasema hayo yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende haraka. Napenda niongelee habari ya kikokotoo. Kwa kweli, kikokotoo kinawasumbua sana wafanyakazi na malalamiko haya yamekuwa ni ya muda mrefu. Binafsi niliomba mkae na vyama vya wafanyakazi ili kuweza kukiondoa hiki kikokotoo, kinalalamikiwa sana. Mtu apewe pesa yake afanyie mambo yake mwenyewe, na ninaamini kila mtu huwa anapanga utaratibu. Naomba Serikali ilifanyie kazi hilo. Waziri Mkuu

liangalie hili, mama yetu Mheshimiwa Mhagama liangalie hili ili muweze kulifanyia kazi, wafanyakazi wengi wanalalamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua fainali huwa ni uzeeni, mtu anapopewa pesa kidogo, wengi huwa na maradhi mengi katika uzee, ule lakini hana pesa. Pesa imeshikiliwa, huku anapewa kidogo kidogo kiasi kwamba haimsaidii kitu. Tunaomba basi kwenye kikokotoo Serikali iweze kutusikia jinsi tunavyoomba, wafanyakazi hao wa muda mrefu wasaidiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna habari ya mapunjo ya mafao ya wastaafu, wengi hawajalipwa, wengi wanalalamika. Ukizunguka katika halmashauri nyingi utaona jinsi ambavyo wastaafu wanavyolalamika, ni wengi. Kila leo napigiwa simu, natumiwa *message*, jamani tunaomba wale watu basi wapewe mafao yao na walipwe haki zao kwa sababu walifanya kazi nchini Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naingia upande mwingine wa pili ambao nitaongelea Habari ya tembo. Tembo katika Mkoa wetu wa Simiyu kwa kweli wamekuwa ni tatizo kubwa. Nimekuwa nikisimama hapa, leo ni mara ya tatu naongelea habari ya tembo. Tembo wanaleta vurugu ya kutosha. Kuanzia kwenye mashamba, tembo anavamia shambani anakula, anaharibu yaani unakuta kila mwaka ni njaa. Wananchi wanajitahidi kulima, lakini bado tembo wanaingia kule wanafanya vurugu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchini Tanzania tumekuwa na mkakati wa kusema kwamba, tunaomba wafugaji wafuge kisasa. Wanapofuga kisasa ina maana anakuwa siyo mchungaji, bali ni mfugaji na yule mfugaji mifugo yake ile michache inampatia faida kubwa, kwa sababu atapata maziwa, atauza, atafanya hiki na hiki, maziwa yanamsaidia. Kwa hiyo, anapokuwa na ng'ombe wachache anaweza kuwamiliki vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nakuja kwa upande wa tembo; tembo wamekuwa wengi sana. Kwa nini tembo asifugwe kisasa?

Kwa nini tembo wazaliane kama mbuzi kule porini na wanaingia kwenye hifadhi za watu wanawasumbua? Tunaomba kama tunavyowahamasisha wananchi kwamba wafuge kisasa, tunataka tembo nao wafugwe kisasa. Kwa nini wao wawe wengi zaidi ya binadamu? Wanatuhangaisha kwa kweli. Mnapowahamasisha wananchi, hamasisheni na wale tembo wapunguzwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapoona watalii wanakuja kuangalia wanyama, wanapenda sana kumwona tembo. Wanataka tu wamwone jinsi tembo alivyo na siyo wingi wa makundi ya tembo. Wanataka waone tu tembo yukoje. Sasa kama wanataka waone tembo yukoje, kwa nini hata Mkoa wetu wa Simiyu tusibaki na tembo nane tu? Wanatutosha sana kwa ajili ya watalii kuangalia hao tembo, kuliko kuwa wanaua tu watu. Wameua akina mama, akina baba na watoto wanaoenda shule. Kwani tembo anataka kuwa kama nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiangalia katika Kitabu cha Maandiko Matakatifu, Hosea 4:6 anasema, "Watu wangu wanaangamia kwa kukosa maarifa." Mungu alivyoumba hii dunia kwa muda wa siku tano alimwandalia binadamu mazingira mazuri: nchi kavu, bahari, maziwa, mito, maua, miti ya matunda na kadhalika. Siku ya sita akamuumba binadamu na akamwambia uwatawale wanyama na vitu vyote vilivyopo duniani, lakini leo sisi tumekuwa wa kutawaliwa na wanyama. Kila siku akina mama wanalia wamefiwa na watoto. Nikiangalia terehe 2/4/2024 kuna kijana mmoja anaitwa Juma Lucas, alivamiwa na tembo akaburuzwa vibaya sana mbavu tano zikavunjika na ndiyo tegemeo kwa mama yake. Akina mama wanalia kwa ajili ya tembo. Hawa tembo wana tatizo gani kuvunwa? Hilo ndilo swali langu la msingi. Mungu alisema sisi binadamu tuwatawale, je, tumekosa maarifa ya kuwatawala hao tembo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepoteza watu wengi. Kweli watu wanapoongea hapa na wengine wanalia wanatoa machozi, ni kweli! Tunapoenda kule kwenye mikutano mbalimbali, mikutano ya ndani na mikutano ya nje swali ni lile lile. Utaongea mambo yote

mazuri anayoyafanya Rais wetu, lakini mwisho wa siku akina mama watanyoosha mikono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Mheshimiwa Waziri atuambie, wameshindwa kuwadhibiti hawa tembo? Kule tembo wako kama mbuzi, yaani tembo wakitoka ni kundi kubwa kiasi kwamba unaweza ukakimbia na kuvunjika miguu. Tunaomba tusaidiwe kwenye habari ya tembo, imefanya hata watoto wa kule Mkoa wa Simiyu wengi wanashindwa kwenda shule. Anapokuwa akienda, njiani anakutana na tembo, akikutana na tembo, tembo anajua ni halali yake, ni kukanyagakanyaga kisha anakwenda zake. Mwananchi anauawa lakini tembo akiuawa inakuwa *issue*. Yule mtu aliyempiga tembo, atapigwa kama mpira wa kona, mpaka aleweke kwa nini amefanya hivyo, atakuwa ameshateseka sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hili Rais wetu anafanya mambo mazuri sana na inawezekana mambo haya makubwa hayajui jinsi watu wanavyoumia kule tulipo. Tunaomba Serikali yetu isimamie jambo hili ili likome, watu waweze kuishi kwa amani. Hotuba ya Waziri Mkuu ilisema, tunatakiwa kukaa katika hali yenye ulinzi na usalama. Ni kweli ulinzi na usalama upo lakini vipi maisha ya wananchi kwa upande wa tembo? Tembo katika Mkoa wa Simiyu wanaongoza. Ninavyohisi ni wengi hata kuliko watu. Kwa sababu wakitoka porini ni balaa, ni msururu mrefu, unajiuliza hao ni mbuzi wanakwenda mnadani au ni ng'ombe wanakwenda mnadani? Tunaomba jambo hilo lishughulikiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaongea kwa uchungu kwa sababu kesi nyingi tunaletewa; "ooh, mwanangu amekufa, mwanangu amefanyiwa hivi, mume wangu amekufa." Akina baba wa Mkoa wa Simiyu ni walinzi siku zote wanalala nje. Ni walinzi, walisomea mambo ya ulinzi lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa tembo nimekwambia kwamba ni wengi kiasi kwamba hata wale wafanyakazi hawatoshi kuwamudu. Ndiyo maana nimesema wavunwe wote kama ni

kuuzwa wauzwe wabaki hata nane tu Mkoa wa Simiyu. Sisi hatuwahitaji. Wakibaki hao wanatosha kwa ajili ya watalii. Hata sisi wenyewe Watanzania tutakwenda kuangalia hata hao wachache wanatutosha, kwa sababu wingi wa tembo siyo tatizo, tatizo wanaua watu. Tunaomba hawa tembo waondolewe, wapunguzwe na wabaki wachache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda sana kushukuru kwa hilo. Ninakwenda sasa sehemu nyingine ya mwisho. Nimesisitiza sana nikiwa na malengo…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Minza, muda wako umekwisha, tafadhali.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Minza Simon Mjika. Sasa nitamwita Profesa Shukrani Elisha Manya atafuatia Mheshimiwa Anastazia James Wambura, Mheshimiwa Dkt. Alice Karungi Kaijage, ajiandae.

**MHE. PROF. SHUKRANI E. MANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia Hotuba ya Bajeti ya Waziri Mkuu. Mchana wa leo nitapenda kuchangia katika sehemu iliyopo katika aya ya 215 hadi 218 juu ya Serikali kuhamia Dodoma iliyopo katika ukurasa wa 104 na 105 wa Hotuba ya Bajeti ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapochangia hoja yangu, kwanza napenda kutambua jitihada kubwa za Serikali za kuhamisha Makao Makuu kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma. Pia, Watanzania wote wajue kwamba jambo hili lipo kisheria, tayari na hakuna kurudi Dar es Salaam. Maana kuna wakati watu wanadhani kwamba huenda kuna siku tutarudi Dar es Salaam, hapana. Ijulikane pia kwamba

maamuzi haya yameshafanywa pia na nchi nyingine. Mwaka 1991 Nigeria walitoa Mji wao Lagos wakapeleka Abuja. Kwa hiyo, siyo jambo ambalo ni geni kufanywa na Serikali za mataifa duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika kutambua jitihada za Serikali, nitambue kwamba Serikali imeendelea kutekeleza azimio hili la kuhamia Dodoma kwa ufanisi wa hali ya juu. Kwanza ni kwa jinsi ambavyo Serikali imejenga Ikulu, na tutambue kwamba Ikulu hii imesanifiwa na Watanzania wenyewe, Ikulu iliyo katika eneo kubwa ambayo inaleta mandhari nzuri katika Mji wa Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tutambue jitihada za Serikali kujenga Mji wa Serikali Mtumba, mji ambao ni mzuri. Napenda ni-*note* kitu hapa, ukiangalia barabara zilizojengwa katika Mji wa Serikali Mtumba, kwa pembeni wamewekewa waenda kwa miguu, jambo ambalo nadhani ni ujenzi wa kisasa. Kwa hiyo, miji yetu inapojengwa, naomba tuchukue *template* ya Mji wa Serikali Mtumba. Hizi barabara nyingine tunajengea waenda kwa miguu, guta, punda humo humo, hapana. Tuchukue *template* ya Mtumba maana ni barabara nzuri zilizojengwa katika Mji wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia utatambua kwamba mihimili yote kwa kutambua kwamba Serikali imehamia hapa, Bunge linapanua maeneo yake ili kuweza kuweka miundombinu bora kwa ajili ya Wabunge na Watumishi. Pia, mhimili wa Mahakama umejenga jengo kubwa ambalo linaelekea kukamilika la Makao Makuu ya Mahakama hapa Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mambo mengine mazuri ambayo yanaashiria kwamba Serikali imehamia na inakuja hapa, ni kuweka barabara za mzunguko ambazo zitaondoa msongamano katikati ya mji, Kiwanja cha Ndege Msalato na pia Chuo Kikuu Kikubwa cha Dodoma hapa nchini. Utaona katika mipango ya Serikali ya kujenga Bwawa la Farqwa hata kama liko katika mipango, ni jitihada za Serikali kuendelea kutoa huduma bora ya maji katika Mji Mkuu wa Nchi hapa Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu iko wapi ninapochangia hoja ya Hotuba ya Waziri Mkuu? Tunapopanga miji yetu, kuna jambo moja linasahauliwa, lilisahauliwa tukiwa bado tupo Dar es Salaam na bado linaendelea kusahauliwa. Hivyo, napenda kuikumbusha Serikali yangu kwamba hili jambo lisiendelee kusahauliwa. Jambo hili ukiangalia katika mipango yake hautaona mahali ambapo Serikali imetenga eneo kubwa zuri la kupendezesha mji la kujenga makumbusho makubwa ya Taifa *(museum)*. Kwa nini napenda kuongelea habari za *museum*? Yaani ukienda katika majiji makubwa duniani, ndipo ambapo unakwenda kutembelea lakini ukija hapa kwetu sasa hivi, bado hatujaona kama jambo hilo lipo katika mipango yetu. Kwa hiyo, pendekezo langu katika Hotuba ya Bajeti ya Waziri Mkuu ni kwamba, pamoja na mipango mizuri ya kupendezesha Jiji letu, hebu mpango huu tusiuache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu gani nasema hivi? Ninapendekeza Makumbusho kubwa ya Taifa pamoja na maktaba kubwa iwekwe mahali ambapo inafikika...

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa, Mheshimiwa Waziri, Jenista Mhagama.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwanza, nimpongeze sana Mheshimiwa Profesa kwa msisitizo wake wa kuhakikisha tunakuwa na *masterplan* nzuri kwa ajili ya Jiji la Dodoma, hasa eneo hili la *museum*. Naomba nikuhakikishie Profesa, kwenye *masterplan* tuna eneo kubwa sana kwa ajili ya *museum* na tayari *design* ya kuwa na *museum* ya kisasa inayoendana na Jiji la Dodoma imekwishafanyika. Vilevile, tutakapoanza *phase three* ya ujenzi wa Makao Makuu ya Nchi Dodoma, ninaamini kwamba eneo hilo litakuwa ni miongoni mwa maeneo ya kufanyiwa kazi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Manya unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. PROF. SHUKRANI E. MANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipokea taarifa hiyo kwa mikono miwili. Sasa napendekeza mambo yafuatayo: Kama hilo liko katika mpango wa Serikali, unajua unapojenga *museum* na kama huo ndiyo mpango wetu, sasa mambo haya lazima tuyazingatie. Kwenye *museum* kimsingi unajua Serikali lazima ijidai, Serikali lazima iji-*pride* kwamba hii ni mimi na mimi ni Tanzania. Sasa tuna utajiri mkubwa sana, lakini pia tuna urithi wa utamaduni mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni katika *museum* ambayo sasa utajiri wote wa utamaduni ambao ni urithi wa vizazi vyote, historia yako ya Taifa tangu Tanzania kabla ya ukoloni, wakati wa ukoloni na baada ya kuwa huru, historia yote inawekwa pale. Pia ndipo mahali unapotambulisha utajiri wa nchi, wa maliasili na malikale vyote vinawekwa pale. Hata kama kuna uvumbuzi wowote ambao umefanyika hapa nchini, ndipo mahali pa kujidai. Kwa hiyo, kama hili wazo lipo kama alivyosema Mheshimiwa Waziri, tunapenda liweze kupangwa vizuri. Hebu fikiria mgeni akija Dodoma sasa hivi, tukishampeleka Mnadani siku ya Jumamosi kuchoma nyama, halafu atakwenda wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, lazima tuwapeleke wageni wetu mahali ambapo tunaweza tukawaonesha kwamba sisi ni Tanzania. Kwa hiyo, sisi tunasema tuna utajiri mkubwa wa madini, lakini utagundua hata hapa ndani, Mheshimiwa Jenista kwa kuwa yeye anatokea Songea atakuwa anajua makaa ya mawe yanafananaje, lakini siyo wote. Kwa hiyo, tunachofanya, unachukua *block* kubwa tu la makaa wa mawe *cubic meter* nzuri kubwa unaweka pale unawaambia Tanzania huu ni urithi wenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna *Tanzanite*, yale madini ambayo kimsingi Serikali imeyanunua sasa hivi bado yako kule *BoT* tu yamefunikwa. Yaletwe kwenye makumbusho yetu ya Taifa ili kila mtu anayekuja Tanzania, unamwambia angalia utajiri wetu uko pale.

Pia, kabla mtu hajaamua kwenda Serengeti kwa mfano, pale ndipo mahali pa kuangalia *video clips* za wanyama wanapohama, hatimaye anavutiwa na kufanya uamuzi wa wapi aweze kutembelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona unaangalia muda wako, nimalizie tu kwa kusema kwamba, faida za kuwa na *museum* itakayokuwa imepangwa vizuri, kKimsingi inatambulisha urithi wetu wa kitamaduni, utajiri wa nchi, na kutunza vema historia ya Tanzania. Katika hilo ninakumbusha tusisahau maktaba nzuri ambayo nayo inaendelea kutunza historia kwa ajili ya vizazi vyetu vyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Profesa Shukrani Elisha Manya. Namkaribisha Mheshimiwa Anastazia James Wambura, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Alice Karungi Kaijage na Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, ajiandae.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hoja ambayo ipo mbele yetu. Kwanza kabisa, nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema, pia ametujalia tumemaliza Kwaresma salama na Pasaka tumeisherehekea vizuri. Tunamwomba Mwenyezi Mungu aendelee kuwalinda wenzetu ambao wako katika Ramadhani na tuombe pia atujalie Eid tuisherehekee vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kukupongeza kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wetu na kwa kweli tunakuamini sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza sana Serikali yetu ya Chama Cha Mapinduzi ambayo inaongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania akisaidiwa na Mheshimiwa Dkt. Isdor Philip Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Baraza lote la Mawaziri kwa kazi nzuri sana ya utekelezaji wa Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa ninapongeza hotuba nzuri sana ya Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo imetuonesha ni namna gani bajeti ya ofisi yake inakwenda. Kimsingi, hotuba hii imeandaliwa kwa weledi mkubwa, hongera sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, hongera sana Wasaidizi wote, akina Mheshimiwa Jenista, Mheshimiwa Ndejembi na wote ambao wapo katika Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaongelea maeneo mawili tu ambayo ni afya na elimu nikizingatia kwamba Serikali yetu ipo katika maandalizi kwa upande wa elimu kutekeleza mtaala mpya, lakini kwa upande wa afya kutekeleza Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote. Kwa hiyo, nitajikita katika maeneo hayo mawili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vigezo vikuu vinne ili tuweze kuwa na elimu bora katika nchi yetu. Kigezo cha kwanza ni mazingira bora ya kujifunzia, kigezo cha pili ni walimu na ufundishaji bora, kigezo cha tatu ni mtaala bora na kigezo cha nne ni tathmini. Kwa hiyo, hivi vigezo ni vya muhimu sana katika kuhakikisha tunakuwa na elimu bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuna tatizo moja, katika bajeti ya TAMISEMI mwaka 2023/2024 tulisikia kuna upungufu wa walimu kwa asilimia 51 katika shule za msingi na asilimia 51 katika shule za sekondari. Ukija kwenye takwimu mbalimbali za mwaka huu, utaona tuna upungufu wa walimu pia kwa asilimia 48 kwa ujumla wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa utaona kwamba katika kipindi chote hicho, tangu mwaka 2023 tumeweza kupunguza kwa asilimia tatu tu, kwenye upungufu wa walimu. Ninachotaka kusema ni kwamba tusipoangalia azma yetu ya kutekeleza mtaala mpya na

azma yetu ya kuwawezesha Watanzania kuwa na elimu bora, kwa kweli inaweza ikawa ni ndoto. Kwa hiyo, naomba sana, Kamati ilipowasilisha hapa taarifa yake Kamati inayoshughulikia Elimu, Utamaduni, Michezo na Sanaa ilipendekeza kwamba ajira za walimu ziongezwe ili kusudi tuweze kuwasaidia Watanzania na watoto wetu waweze kupata elimu bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata ukisikiliza michango mingi ya Waheshimiwa Wabunge tangu wakati ule wamependekeza walimu waongezwe na maswali mengi hapa Bungeni huwa yanaonesha kabisa kwamba walimu wanahitajika katika shule zetu. Kwa hiyo, naiomba Serikali izingatie ushauri wa Waheshimiwa Wabunge ili tuweze kutoka hapa tulipo na kwenda katika hatua ya mbele zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa afya nichukue nafasi hii kushukuru sana Wizara ya Afya ikiongozwa na Mheshimiwa Waziri Ummy Mwalimu, pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Dkt. Mollel kwa kazi nzuri ambayo wameifanya kule Mkoa wa Mtwara katika Hospitali yetu ya Rufaa. Tuliomba mahitaji mengi sana ambayo yalikuwa ni upungufu karibia *items* 25 lakini waliweza kutekeleza na hatimaye hospitali ile imezinduliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa safari moja huanzisha nyingine, ila siyo *safari lager,* ni safari ya kuimarisha afya ya wananchi. Wameongezeka wagonjwa wengi sana na wengine kutoka nchi za nje kuja katika ile hospitali. Tatizo kubwa ambalo liko hapa sasa ni upungufu wa madaktari. Kuna upungufu mkubwa wa wataalam wa afya katika hospitali hii. Tunahitaji wataalam zaidi ya asilimia 50, ndiyo upungufu uko hapa. Ukiangalia mfano wa *department* ya *radiology* wanatakiwa wawe *minimum* ya watumishi saba, lakini wapo watatu tu na tuna vifaa pale vingi. Kwa hiyo, vingine vinashindwa kutumika kwa muda unaostahili, lakini pia kwa upande wa akina mama kuna kifaa cha *fluoroscopy,* tunahitaji pale tupate *mammography* ili kusudi akina mama wasiweze kupata rufaa kwenda Dar es Salaam kwa kitu kidogo kama hicho waweze kutibiwa pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande mwingine, ile ni hospitali ya rufaa, lakini utaona kwamba watoto njiti wanapelekwa katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa kutoka juu kupelekwa chini, hakuna kitengo cha watoto njiti pale, lakini ajabu ni kwamba jengo la mama na mtoto tayari lina michoro, ila tunasubiri tu ujenzi. Kwa hiyo, nikumbushe Serikali iweze kujenga jengo la mama na mtoto ili tuondokane na hii adha ya kutoa watoto njiti pale Hospitali ya Rufaa Kanda kupeleka katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Bima ya Afya unategemea sana huduma. Tukiwa na huduma karibu na wananchi, wengi wataitikia na wengi wamependa sana hili suala la Bima ya Afya kwa Wote, lakini kinachotia hofu ni zile huduma. Kwa hiyo, naomba sana, Serikali izingatie kila Mkoa uweze kupata watumishi, kila Hospitali ya Kanda iweze kupata watumishi na vile vifaa vya muhimu ili kuondoa usumbufu wa rufaa za kwenda Dar es Salaam na kuleta msongamano. Hii inaweza ikaleta vifo ambavyo siyo vya lazima. Kwa hiyo, naomba hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo napenda kuomba ni Kituo cha Afya cha Likombe. Kile kituo cha afya kina huduma nzuri sana za uzazi, lakini kuna shida ya miundombinu, haitoshi. Imelazimu nyumba ya daktari ichukuliwe, daktari ahamishwe ili kusudi nyumba yake waongeze vitanda sita kwa ajili ya huduma ya wazazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana, Mungu awabariki. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Anastazia James Wambura kwa mchango wako mzuri. Sasa namwita Mheshimiwa Dkt. Alice Karungi Kaijage atafuatia Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege na Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, ajiandae.

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naungana na wenzangu kukupongeza kwa nafasi uliyopata,

hongera sana. Nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Hotuba hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa. Pamoja na mambo yote, tunajua hotuba hii inahusu mapitio na mwelekeo wa kazi za Serikali, pamoja na bajeti wanayoiomba, lakini inatuelezea mapitio na mwelekeo wa kazi za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii Wizara ina mambo mengi sana kwa sababu inaratibu mambo mengi. Nikiwa bado sijajadili sana, kwanza nampongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuwasimamia vizuri Mawaziri wetu akiwepo Waziri Mkuu, Naibu Waziri Mkuu, Dada yangu Jenista Mhagama Waziri *senio*r, pamoja na Mheshimiwa Deo Ndejembi na Manaibu wote, Watendaji na Watumishi ambao wamefanya kazi kwa uadilifu mkubwa chini ya Wizara hii mpaka tunaona matokeo haya yote. Ninapongeza hotuba nzuri sana ambayo imesheheni vitu vingi vyenye mantiki kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naenda kutoa ushauri kwa Wizara hii ambao naamini utaisaidia Serikali kuimarisha utekelezaji wa vipaumbele ambavyo vimeainishwa kwenye Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa mwaka huu 2024/2025. Mpango huu ni wa tatu katika ule Mpango Mkuu wa Miaka Mitano ambapo dhima ya mpango huu ni kujenga uchumi shindani na pia viwanda kwa ajili ya maendeleo ya watu, yaani mtu mmoja mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vipaumbele vya ule Mpango wa Miaka Mitano kipaumbele namba tano kinahusu ukuzaji wa ujuzi. Kwa hiyo, ina maana ni watu au rasilimali watu. Pia Wizara ya Mipango inajipambanua kwamba, katika kutekeleza mpango huu wa tatu wa Taifa wa maendeleo itazingatia misingi kumi ambayo itawaongoza kutekeleza mpango huu. Msingi namba saba unasema, kuwa na rasilimali watu ya kutosha, iliyo bora, inayokidhi matakwa ya wakati huu ambao umetawaliwa na teknolojia na ubunifu, lakini msingi mkuu ambao watakuwa wamezingatia Wizara ya Mipango tunawategemea sana, ni kuwa na nidhamu ya utekelezaji wa mipango yao waliyojiwekea. Hii yote inagusa watumishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mipango haikuishia hapo, tunaipongeza imeendelea kuboresha mazingira bora ya biashara na sasa imeenda kufungua Idara za Biashara na Uwekezaji katika Halmashauri zote 180. Ina maana, kuna uhitaji wa watumishi lakini siyo hivyo tu, imefungua kwenye hizo Halmashauri vitengo vya mazingira ya biashara, hivyo, kunahitajika watumishi huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napongeza kwamba Serikali imekuja na mfumo mpya wa tathmini na ufuatiliaji, jambo ambalo Wabunge tumepigia kelele sana. Katika Wizara zote za Kisekta na Taasisi za Serikali zinazojitegemea zilishakuwa na idara hiyo, lakini kwa changamoto. Ina maana kuna utendaji unaohitaji kuingizwa kwa watumishi, yaani uadilifu na uzalendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mjadala wangu umejikita katika Ibara ya 146, kuhusu wafanyakazi pamoja na watumishi. Nimebahatika kutembelea mikoa michache na Halmashauri kadhaa. Ukikutana na watumishi, kabla amesimama kuchangia au amekuandikia kwa maandishi, jambo la kwanza utakalokutana nalo, wanampongeza sana Mheshimiwa Rais. Kwanza wanasema amejali maslahi yao; pili, ameboresha mazingira yao ya kufanyia kazi. Kwa hiyo, watu wanaanza na pongezi kwa Mheshimiwa Rais, halafu baadaye ndio wanakuja na changamoto wanazokutana nazo. Kwa hiyo, hii inaonesha kwamba wametambua mchango wa Mheshimiwa Rais ambao tunawapongeza Wizara ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kuendelea kumshauri vizuri Mheshimiwa Rais pamoja na kumpa ushirikiano wa Wizara zote ambazo mnafanya, pamoja na Mheshimiwa Rais mkimsaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto nyingi sana tunakutana nazo, lakini nitasema chache ambazo natamani jicho la uratibu la Wizara ya Waziri Mkuu liitazame. Kuna suala la elimu na miundo. Wizara ya Utumishi inafanya kazi kubwa sana, nitasema baadaye, lakini watumishi wanakwenda kusoma, wanajisomesha kwa shida, tena wale ambao wako kazini wanaporudi, anapo-*submit* cheti, kwanza anaogopa aki-*submit* cheti kwani kuna baadhi ya miundo anashuka Daraja. Kwa baadhi ya miundo hawezi

kupanda, matokeo yake wakitoka kusoma wanaficha vyetu vyao, wengine hawavi-*submit,* wengine hawaoni kwa nini waende kusoma. Naomba jicho la pili la Wizara ya Waziri Mkuu, waende kuangalia wawasaidie kwani wanafanya kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, kuna suala zima la vikao, kuna Mabaraza ya Wafanyakazi kule chini, wanakaa baadhi ya Halmashauri na Taasisi hawakai, wakikaa wanakaa Baraza moja na Baraza hilo wana nia ya kupitisha bajeti yao, nasi tunajua kabisa Mabaraza yale hawakai watumishi wote, wanakaa wawakilishi. Baadhi ya wawakilishi ni wale wanaolalamikiwa na watumishi wa kawaida. Kwa hiyo, jicho la Waziri Mkuu liangalie sehemu hiyo wakisaidiana na vyama vya wafanyakazi. Mabaraza yakae kwa wakati na waende watu ambao wanaaminiwa kushiriki kuwasilisha mawazo yao kwenye Mabaraza hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli hakuna haki bila wajibu, lakini watumishi wakifanya wajibu wao walipwe kwa wakati. Kuna baadhi ya Halmashauri unakuta mtumishi, labda ni Mtendaji Kata amefanya kazi kwa miezi saba, anakwenda na kurudi lakini hajawahi kulipwa posho yake. Wapo wengi wa namna hiyo ambao masilahi yao wanategemea mapato ya Halmashauri. Kuna Halmashauri hazina uwezo, tunakubali, alikuwa anasema Mchangiaji wa Kilolo kwamba Halmashauri ambazo zina njia nyingine za ubunifu tuwasaidie, hatuwezi kulipwa na Serikali Kuu vyote, haiwezekani. Kwa hiyo, ni vizuri sana kama kuna haki na wajibu, basi mtumishi wa Tanzania baada ya kutekeleza wajibu wake, apate haki yake kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Ofisi ya Waziri Mkuu, wamekuja na Tume inayotembea, Tume ya Kurekebisha Matatizo ya Wafanyakazi mahali pa kazi. Napongeza, lakini ina kazi kubwa ya kufanya, kuna mambo mengi sana kwenye Halmashauri zetu na Taasisi kule chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo mengi ya kusema, lakini ngoja sasa niongee kuhusu kikokotoo. Katika Awamu hii ya

Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, ndani ya miaka mitatu *almost,* kuanzia Machi, 2021 mpaka Septemba kwa nini watumishi wanamsifu? Ameweza kupandisha vyeo na madaraja zaidi ya watumishi 455,000 ambayo imeigharimu Serikali 1,011,000,000,000/= ndani ya miaka yake mitatu. Siyo hivyo tu, amebadilisha kada na miundo ya watumishi 30,000 na zaidi ambayo imeigharimu Serikali shilingi bilioni 2.5. Hakuishia hapo, kilio cha kulipwa malimbikizo ya mishahara Mheshimiwa Rais ndani ya miaka mitatu anapata keki ndogo, lakini watumishi hajawasahau, amebadilisha madaraja amelipa malimbikizo ya watumishi watumishi 130,000. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba dakika moja nimalizie. Kwa hiyo, kwa yote aliyofanya, haya ajira za kutosha zaidi ya ajira 150,000 na bado tumeona juzi walitoa ajira 8,900 kwenye Idara ya Afya. Vilevile tulimwona Mheshimiwa Rais akiongea na ndugu zetu Askari akasema, ndugu zangu suala la kikokotoo nimelisikia. Sasa mtu mzima akisema hivyo, tumpe nafasi, tumwombee kwa Mungu, suala la kikokotoo aweze kufanya maamuzi yaliyo na tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Alice Karungi Kaijage. Namwita sasa Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, atafuatiwa na Mheshimiwa Constantine John Kanyasu na baada ya hapo atafuatia Mheshimiwa Anatropia Theonest.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niwe miongoni mwa wanaochangia jioni ya leo. Kwanza naomba nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kunijalia uhai ili niweze kusimama leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na wenzangu waliokupongeza kwa nafasi ambayo hakika Kiti kimetulia, umeenea ipasavyo, Mungu akubariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kipekee nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa jinsi ambavyo anawatumikia Watanzania. Hakika sisi sote na majirani wanajua jinsi ambavyo Mheshimiwa Rais amejitoa katika kuwaletea maendeleo Watanzania. Naomba niungane na wenzangu wote ambao wamempongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na wasaidizi wake wote; Mawaziri, na Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu. Hakika kazi mnaichapa, Mwenyezi Mungu azidi kuwajalia afya ili mwatumikie Watanzania, kwani wana matarajio na matumaini makubwa sana kwenu ninyi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mchango wangu nijielekeze kuonesha jinsi ambavyo Serikali hii ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Serikali ya CCM ambayo yeye ndio Mwenyekiti wa Chama chetu cha Mapinduzi, amefanya mapinduzi makubwa katika suala zima la elimu. Sote ni mashuhuda jinsi ambavyo yamefanyika maboresho makubwa sana katika utoaji wa elimu baada ya hamasa ya elimu bila ada, jinsi ambavyo bajeti imekuwa ikiongezeka ya elimu ya kati na elimu ya juu na hivi karibuni sote tunakumbuka jinsi ambavyo vijana wetu waliongezewa posho ambayo ni maarufu kwa jina la *boom* kufika shilingi 10,000. Hakika Mheshimiwa Rais Mungu azidi kukubariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maboresho haya, hakika vijana wengi wa kitanzania wameweza kupata fursa ya kujipatia elimu. Tafsiri yake ni kwamba, ukienda sokoni wamejaa vijana wengi ambao wana matumaini ya kuweza kupata ajira. Ajira zinategemewa kutoka katika Serikali na kutoka kwenye sekta binafsi na kwa mantiki hiyo, pamoja na kwamba Serikali imejitahidi kuajiri walimu, imeajiri kwenye sekta ya afya, lakini bado ukienda mtaani wenye matumaini ya kupata ajira bado idadi ni kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini ambacho nashauri? Kwanza ni vizuri Serikali wakafuatilia, kwani yapo malalamiko mtaani ambayo yanatokea na hasa upande wa walimu wanaoajiriwa. Tunapata malalamiko kwa vijana pale ambapo yule ambaye alihitimu mwaka 2015 hajaajiriwa lakini mwenzake ambaye wako kwenye kada hiyo hiyo *arts* amemaliza 2020 amepata ajira. Wanajiuliza, ni *criteria* ipi ambayo inatumika kiasi kwamba huyu ambaye amemaliza shule hivi karibuni anapata ajira na anaachwa yule aliyetangulia kumaliza? Ni vizuri Serikali mkafuatilia ili tusije kulaumiwa, ikaonekana kuna namna mtu ambaye anafahamiana na mtu mwingine ama *godfather* hao ndio wanapata nafasi ya kajiriwa. Hayo mambo yanaleta malalamiko sana kwa vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoseama, anayetegemewa kutoa ajira ni Serikali na Sekta Binafsi, naiomba Serikali na hili naomba niungane na maoni ya Kamati ambao wamepongeza Serikali kwa kuendelea kutiliana mikataba na nchi ambazo zina nafasi za kutoa ajira. Fursa hii ni vizuri tukaitumia kwa sababu tunao vijana wetu ambao tungependa waajiriwe, lakini nini ambacho tunatakiwa kufanya ili vijana wetu waajiriwe, ambao wataenda kufanya kazi zenye staha? Isije ikawa ilimradi kufanya kazi. Wewe umekuwa ukisikiliza, kuna kipindi tunapata malalamiko, vijana wetu wanaenda kufanya kazi ughaibuni huko, lakini wanakuwa wanatwezwa. Jambo hili halina afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri tukaiga mfano kwa jirani zetu wa Kenya. Kuna kampuni ambazo zimeanzishwa kwa kushirikiana na Serikali ambao wanakuwa wanatafuta ajira kwa ajili ya vijana wao. Pia, wanakuwa na jukumu la kuhakikisha wanawafuatilia kujua kwamba je, katika mikataba ambayo wameingia, zile kazi ambazo waliahidiwa ndiyo hizo ambazo wanazifanya? Pale ambapo kunakuwa na malalamiko, inakuwa ni rahisi wao kujua chombo gani wakifikie ili kuweza kupeleka malalamiko yao. Jambo kama hilo tunaweza tukafanya kama Taifa. Unajua zimetangazwa ajira duniani kwa ajili ya kufundisha Kiswahili. Hebu tuambizane kwa jitihada za makusudi, ni chombo gani ambacho kimefanya uratibu kuhakikisha Watanzania hawa ambao wana uwezo wa kwenda kufundisha

Kiswahili wametafutiwa ajira wakaenda kufanya kazi na tukapata *remittance* hapa kama Taifa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri na ni wakati mwafaka kama Taifa tutumie fursa hizi kwa sababu siyo rahisi kwamba wote wataajiriwa Tanzania. Pia ni vizuri Serikali ikaweka mazingira kwa sekta binafsi ambayo ndiyo inaweza ikawa na uwezo wa kuajiri Watanzania walio wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuchangia upande huo, naomba nitumie fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. *Personally,* alifika mwaka 2020 katika Wilaya ya Kalambo kwenye ziara yake. Wananchi wa Kalambo hususan eneo la Kasanga, wamenituma nimkumbushe maana muungwana akiahidi huwa ni deni. Aliahidi ujenzi wa Kituo cha Afya katika Tarafa ya Kasanga, Kijiji cha Kasanga na tayari eneo lishatengwa, tunasubiri na ninaamini Serikali wakati mnahitimisha Ofisi ya Waziri Mkuu, itoe tamko lini ujenzi wa kituo cha afya utaanza Tarafa ya Kasanga katika Kijiji cha Kasanga?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, tuna uhitaji mkubwa wa Kituo cha Afya cha Mkakati katika eneo la Katete, Kata ya Katete ambayo inapakana na nchi ya Zambia. Ni hitaji kubwa na tulivyopata fursa ya Wabunge kuandika maeneo ya kujenga vituo vya mkakati, nimeandika Katete. Kwa hiyo, naamini Serikali safari hii mtaanza kutenga fedha ili tuanze kujenga hivyo vituo vya afya ambavyo ni hitaji kubwa sana la wananchi wa Kalambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa jitihada zake, naona kuna mapitio ya maboresho kwa ajili ya reli yetu ya *TAZARA,* ni jambo jema sana. Naomba niikumbushe Serikali tutumie fursa hii wakati maboresho yanafanyika juu ya reli yetu ya *TAZARA,* ni wakati muafaka wa kutazama njia pacha kutoka Tunduma kwenda *Border* ya Kasanga kwa sababu tayari tuna bandari. Sisi kama Mkoa, tutakuwa tumepata kiunganisho kizuri, na mbele ya safari na wewe umekuwa ukiniombea ili kama nchi tuweze ku-*access* Kongo DRC kwenda Lubumbashi kwa kupitia Kasanga. Hakika kwa ndoto hii ya

sasa hivi, kwa maono makubwa ya Serikali, naamini ndoto yangu itakuja kufanikiwa ili tuweze ku-*access* kwenda DRC kwa kwenda Lubumbashi bila kupita Zambia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa, naunga mkono hoja, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kandege. Sasa namwita Mheshimiwa Constantine John Kanyasu atafuatia Mheshimiwa Anatropia Theonest na Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi, ajiandae.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naomba nitumie fursa hii kutambua kazi kubwa na nzuri ambayo inafanywa na Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na wasaidizi wake wote. Kama ambavyo wamezungumza wachangiaji wengine, ninaipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu ikiongozwa na Waziri Mkuu mwenyewe na wasaidizi wake kwa kazi nzuri ambayo wanafanya na hasa kazi nzuri ya kuisimamia Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ushauri kwenye maeneo machache. Kwanza, nianze na jambo moja ambalo niliwahi kutoa ushauri huko nyuma. Kwenye mtandao wa kuomba ajira *(Ajira Portal)* ule mfumo umetengenezwa kwamba mwombaji anapoingiza zile *credential* zake siku ya kwanza, akiingiza kwamba amesoma *Fisheries, next time* kama huyo mtu alikwenda kusoma kitu kingine ule mfumo hauwezi kupokea. Sasa hali ilivyo sasa kutokana na uhaba wa ajira, vijana wengi wanakuwa ni *multi professional,* wanasoma vitu vingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mtu aliyeanza akasoma *certificate* ya *Wildlife Management* anapofikisha miaka 25 kwa mujibu wa taratibu za watu wa maliasili, haajiriki tena. Huyo mtu ana-*opt* kwenda kusoma kozi nyingine, lakini kwa sababu kwenye mfumo mle ndani tayari anasomeka aliwahi kuingiza *Wildlife,* ule mfumo unam-*reject*. Mnafahamu vizuri kwamba mfumo

ukishamkataa na umri umeenda, hawezi kuajiriwa tena na kozi ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wengi wanaanza kusoma siku hizi, wanakwenda kwenye *technical schools.* Anaanzia *technical school,* anasoma *diploma,* anakwenda anasoma *degree,* halafu anasoma *masters.* Ukiingiza cheti cha *diploma* ukija kuingiza cha *degree* unaku-*reject.* Sasa sijui huwa wananielewa nikizungumza. Hebu naomba mlichukue jambo hili mlifanyie kazi, kwani linasababisha vijana wengi kushindwa kupata ajira kwenye mfumo. Nalizungumza hili kwa mara ya pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la pili, tunaishukuru Serikali kwamba baada ya hali mbaya ya hewa, barabara nyingi sana ziliharibika. Tumepata pesa ya *emergency* shilingi milioni 400 katika Jimbo la Geita Mjini kwa barabara ambayo inatuunganisha kati ya Geita na Nyang'hwale, lakini pesa hiyo imeenda kujenga daraja moja peke yake. Ile barabara ina madaraja manne yaliyokatika na hakuna tena mawasiliano. Kwa mujibu wa taarifa iliyopo ni kwamba ile shilingi milioni 400 ndiyo imetosha. Kwa hiyo, hamna kilichofanyika pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wa Geita hivi tunavyozungumza hakuna barabara, zote zimeharibika kwa sababu ya mvua nyingi. Sasa naomba jambo hili lifanyiwe kazi kwa sababu katikati ya mji pamejitengeneza vijito, barabara zimekatika, magari yanatitia. Mtu anaacha gari nyumba ya sita ndiyo anakwenda kwenye nyumba yake. Naomba barabara hizi zitengenezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, tunaishukuru Serikali, tumejenga shule nyingi na tumejenga zahanati nyingi. Tatizo kubwa sasa limekuwa ni wafanyakazi. Naiomba Serikali ifanye takwimu. Mimi kwa miaka mitatu pekee ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan nimejenga shule mpya sita. Shule nne nimepata pesa kutoka Wizarani, lakini kwa miaka mitatu wameleta walimu 12. Sasa shule sita *on average* shule moja inahitaji walimu 24, umeleta walimu 12.

Maana yake ni kwamba walimu tumewatoa kwenye shule nyingine zisizokuwa na uhaba wa walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuna shule mpya ambayo tayari ina wanafunzi 4,000 ina walimu watano. Sasa hiki kinakuwa kichekesho. Mwaka 2023 Mheshimiwa Waziri Ndejembi kabla ya kuhama Wizara, aliniahidi ataniletea walimu, hakuleta mwalimu hata mmoja kwenye halmashauri ya mji. Sasa tumejenga shule sita, halafu hakuna walimu kwenye hizo shule, sasa zinafanya kazi gani? Nataka kuiomba Serikali kwanza tupate hawa walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye afya tumejenga zahanati za kutosha na tumejenga vituo vya vitatu, lakini havina watumishi. Sasa pengine ni vizuri Serikali ikatafuta takwimu kwanza za zahanati ngapi ambazo ziko tayari na zinataka watumishi wangapi ili halmashauri ziache kuwekeza kwenye zahanati. Tena watuzuie kabisa msijenge nyingine mpaka tukamilishe hizi waweze kutuletea nyingine. Vinginevyo tutakuwa tunatumia pesa halafu zahanati zinakuwa mazalia ya popo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la nne nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, nilimwona Dodoma akishughulika na migogoro ya ardhi. Nilimpongeza kwa sababu ulikuwa ni ushauri wa Kamati kwamba lazima wale waliotengeneza migogoro ile waweze kushughulikiwa. Sasa mimi ninao mgogoro wa ardhi Geita. Namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, aliushughulikia kabla ya kuondoka na Mkuu wangu wa Mkoa ameushughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Madini, kwani tuna tatizo la wananchi wa Nyakabale. Nyakabale ni mtaa ambao una zaidi ya watu 5,000. Watu hawa wako ndani ya vigingi vya GGM. GGM wanakataa kulipa fidia kwa sababu wanasema hakuna sheria. Serikali kwa miaka 24 imeshindwa kuwalazimisha GGM wawalipe fidia watu wa Nyakabale. Matokeo yake vyanzo vya maji vyote vya Nyakabale vinavujiwa na maji machafu; watu wanakosa maji ya kunywa. Hatuwezi kupeleka

huduma pale kwa sababu lile eneo huwezi kulipima na liko katikati ya mji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye uchangiaji wangu wa mwanzo niliomba, nikasema, kwa sababu ni upungufu wa kisheria, Serikali ndiyo iliyotengeneza sheria kwamba huyu mwenye *mining licence* ana miliki eneo lake na kulilinda na kuzuia watu wasiendeleze, lakini hawawajibiki kulipa fidia mpaka watakapotaka kuchimba. Sasa kwa kuwa wananchi wale wameathiriwa na zuio hilo, Serikali yenyewe iwalipe fidia halafu ihangaike na huyo mwekezaji. Kuliko kuwaacha hawa wananchi wakaendelea kuishi kwa umasikini wao na ardhi ni ya kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tano, nampongeza Mheshimiwa Jerry Silaa, anafanya kazi yake vizuri. Mkuu wangu wa Idara ya Ardhi alitembelewa na Kamishna wa Ardhi na Kamishna wa Ardhi alikwenda na vyombo vya habari. Akafika akaonesha kwamba kuna mafaili ya watu zaidi ya 100 ambayo hayajashughulikiwa, wanasubiri hati. Mheshimiwa Waziri wa Ardhi akampongeza kwenye *Instagram;* "Hongera kwa kufanya kazi yako vizuri." Kesho yake yule Mkuu wa Idara anaandikiwa barua ya kushushwa cheo kwamba amechelewesha majalada 100 kutengeneza hati. Sisi sote hapa ni Wabunge huwezi kuona kwamba ile ilikuwa *drama.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tangu lini kwanza unakwenda kwenye ofisi kukagua kazi, unakwenda na vyombo vya habari? Pia hakuna mafaili 100, yule anashushwa cheo wakati mafaili yaliyokuwa yanasubiri hati ni 30. Halafu naomba nimalizie katika hayo 30, watu hawana *NIDA* na hawana mikataba ya mauziano. Sasa huyu Afisa Ardhi afanye kazi gani? Kuonesha kwamba ni *drama,* siku ile ile Waziri anampongeza, kesho yake huyu Kamishna wa Ardhi anakwenda kuwashusha cheo Maafisa wateule wote kwamba nimewaondoa cheo na kuteua wengine. Tunawaonea watumishi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika moja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Constantine Kanyasu, ahsante.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika moja tu namalizia. Sote tunajua haki ya mtumishi kabla hujamchukulia hatua lazima um-*charge,* umpe nafasi ya kujitetea uone majibu yaliyojificha kama hayana maana ndiyo um-*charge*. Huwezi kumwadhibu kwanza...

**MWENYEKITI:** Ahsante Serikali imesikia.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kanyasu. Sasa namkaribisha Mheshimiwa Anatropia Theonest atafuatia Mheshimiwa Dkt. Florence George Samizi na Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga ajiandae.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi nami niweze kuchangia mawili matatu kwenye hoja iliyoko Mezani. Nitakuwa sio mwingi wa fadhila nisipotambua mchango wa Mheshimiwa Waziri Mkuu hususan kwenye zao la kahawa kwa Mkoa wa Kagera. Ukweli ni kwamba, changamoto zilikuwa ni nyingi sana, nimelia pamoja na Wabunge wengine ambao wanazalisha kahawa na mikoa inayotoa kahawa. Tumeongea mara nyingi tukilia kilio chetu kuhakikisha bei ya zao la kahawa inapanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei hiyo ilikuwa ikipata changamoto ya tozo kadha wa kadha, lakini hizo tozo ziliondolewa na hivyo kusaabisha bei kuongezeka kidogo. Vilevile, kwa Mkoa wa Kagera, moja kati ya kilio changu ilikuwa ni suala la minada kuacha zao la

kahawa likawa soko huria kama yalivyo mazao mengine, mwenye kuwa na bei ya kutosha akaweza kushindanishwa na kuuza kahawa. Nashukuru sana kwamba haya yote yameweza kutendeka na leo tunaona bei ya kahawa imepanda kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tuna changamoto nyingi za msingi kwenye zao la kahawa. Hizo kwanza nazi-*register* kabla sijaanza kueleza hoja nyingine. Kwanza, ni changamoto ya pembejeo. Leo kahawa pamoja na mazao mengine ya migomba yanashambuliwa sana na changamoto inayoitwa mnyauko, lakini nitaongelea kahawa. Kwa hiyo, mikahawa mingi mikubwa inashambuliwa na kuharibika na wananchi kukata tamaa. Pia kuna vidudu vinavyoishambulia hii miche.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tushukuru kwamba kumekuwepo na juhudi za kuwapatia mbegu lakini bado mbegu ni chache ukilinganisha na uwezo wa kuzalisha na nia ya watu wa Mkoa wa Kagera, Wilaya ya Kyerwa na Karagwe kuendelea kuzalisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee upande wa pili, kila neema inakuja na changamoto. Nimkumbushe Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba nili-*register* wakati tunaongea kwenye kikao nika-*register* changamoto ya wananchi wa Kyerwa na hasa maeneo ya mpakani kunyanyaswa kwa sababu ya zao la kahawa. Nikaeleza adha wanazozipata wakibambikizwa na kuambiwa kwamba wanavusha kahawa. Nikaeleza vifo vilivyotokea kwa watu kuambiwa wanavusha kahawa bila Ushahidi, lakini bila kufuata *due process* kwamba mtu kama anavusha kahawa, basi akamatwe, apelekwe Mahakamani ashtakiwe. Mlolongo wa haki jinai tunaoujua ufanyike na mtu apate haki yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitawataja baadhi ya watu. Mtu mmoja ambaye aliathirika anaitwa Jimmy Bagumila Ninondi. Huyu kijana anatokea Kijiji cha Rwabikagati Kitongoji cha Omukagando. Huyu kilichomkuta sasa wakati wanasema huo msako wa kahawa unapita yeye walishamlenga, aligongwa na *defender* mara mbili,

yaani wakamgonga mara ya kwanza, wakahisi kwamba hajafariki vizuri, wakampitia mara ya pili na akafariki hapo hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nijue hao waliofanya hicho kitendo magari yanafahamika, waliofanya hivyo vitendo wapo. Nataka kujua wamechukuliwa hatua gani za kisheria, kwa sababu hiyo siyo namna sahihi. Haki jinai anayoisema Mheshimiwa Rais, siyo ya kugonga mtu na *Defender* na kumuua. Nataka nijue haki ya huyu mwananchi iko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wa pili anaitwa Vadi, huyu anatokea Kijiji cha Nyabiaga Kata ya Bugomora. Alikuwa ni dereva akiendesha gari kwenda kata nyingine ya jirani ya Kaisho, akavamiwa akaambiwa kwenye hiyo gari yako unavusha kahawa. Kukatokea taharuki kubwa sana akakimbia. Sasa wale wanajeshi ambao wanajifanya wanalinda kahawa waliwasha kijiji chote kwa risasi. Nadhani mnakumbuka niliwahi kueleza kwenye *briefing,* risasi za moto zaidi ya 100 zikarushwa zikatafuta hao wanakijiji. Kama haitoshi, huyu kijana akapigwa risasi ya koromeo akapelekwa Bugando. Nilienza *incidence* yake ikiwa ni pamoja na mwenzake ambaye alikuwa anaitwa Monge Vincent ambaye yeye alipigwa risasi ya kichwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niulize, hata kama wanavusha kahawa na hata kama wanafanya nini? Hiyo ndiyo *due process* ambayo tunaiongea kila siku? Hiyo ndiyo haki jinai ambayo Mheshimiwa Rais amekuwa akipigania? Nataka nipate majibu ni hatua gani zimechukuliwa kwa hawa wanajeshi pamoja na askari ambao wamekuwa wakinyanyasa wananchi kwa neno moja tu kwamba wanavusha kahawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sio huyo tu, nakutajia na *incidence* nyingine. Kuna wanakijiji walikuwa kwenye harusi gari ya *defender* imekuja ya hawa wanajeshi wakawavamia. Hawa wanajeshi wakala vyakula vyao, wakanywa pombe zao na wakawapiga kwa sababu ya kile kile kinachoitwa kuvusha kahawa. Nataka nieleze wazi, kuna mwingine anaitwa Charles Amos, Mwenyekiti, Afisa

Mtendaji Mstaafu wa Kijiji cha Mulongo naye amepigwa kwa sababu anatoa kahawa eneo moja kwenye shamba lake moja kwenda kwenye shamba lingine.

**MWENYEKITI:** Nimemwona Mheshimiwa Waziri amesimama. Tafadhali Mheshimiwa Waziri.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakupongeza lakini nataka nitoe taarifa. Wanajeshi kazi yao ni kulinda amani na mipaka. Kwa hiyo, siyo kweli kwamba wanajeshi wanapiga wananchi kama ilivyoelezwa, labda Mbunge atoe uthibitisho wa hilo analolisema, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anatropia unaipokea taarifa ya Mheshimiwa Waziri?

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *with due respect,* naomba Mheshimiwa Waziri afuatilie kinachotokea Kyerwa. Natambua juhudi Wanajeshi, lakini ninavyoongea, inapofika wakati wa kahawa wanatumiwa kwa kile kinachoitwa kulinda kahawa isivuke. Kwa hiyo, ninachokieleza, *it is with facts,* nakielewa. Naomba niendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu cha pili ambacho nataka nieleze ukiachana...

**MWENYEKITI:** Samahani Mheshimiwa Anatropia. Mheshimiwa Waziri, tafadhali.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado naomba uthibitisho wa hayo anayoyasema, atoe ushahidi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anatropia, Mheshimiwa Naibu Spika, alikaa kwenye Kiti hiki asubuhi, akatoa maelekezo juu ya utaratibu

wa vithibitisho pale tunapokuwa na *allegations* kubwa kwa Serikali. Mheshimiwa Anatropia, kadri ya Majibu ya Mheshimiwa Waziri au kadiri ya taarifa ya Mheshimiwa Waziri, wote tunajua kazi ya Jeshi la Wananchi ni kulinda mipaka ya nchi yetu. Kama Jeshi la Wananchi linafanya tofauti na hayo ambayo yanatarajiwa kufanywa na Jeshi letu, basi naomba andaa taarifa yako yenye vithibitisho na uilete kwenye Meza ya Spika, na Serikali chukueni hiyo taarifa kama *alert* ili muweze kufuatialia na ninyi muweze kujiridhisha kwa upande wenu.

Mheshimiwa Anatropia, endelea.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumechukua muda mrefu, naomba niishauri Serikali, na hiyo ndiyo hoja ninayoileta, kwamba uchunguzi ufanyike ili kufahamu nini kilitokea katika msimu wa kahawa mwaka 2023 na kujua matukio yaliyofanywa na wanajeshi na matukio yaliyofanywa na Polisi kwa wananchi. Hapa tupo kwa ajili ya kutetea maslahi ya wananchi, hivyo kila mwananchi aliyeumizwa aidha kwa watu kukiuka sheria kwa makusudi au bahati mbaya, wanapaswa kupata haki yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naiomba Serikali, na nimewahi kumweleza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye kikao kilichofanyika Kyerwa, nikashauri kuwepo na tume ya kwenda kuchunguza na kuondoa changamoto zilizotokea Kyerwa. Hiyo ndiyo nasisitiza kwamba ni lazima ifanyike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaenda kufungua msimu mpya wa kahawa, kama changamoto zilizojitokeza mwaka 2023 zinaenda kujitokeza tena, sisi kahawa siyo neema, ni kifo. Narudia, changamoto zilizojitokeza mwaka 2023 kama hazitafutiwi ufumbuzi na waliofanya kwa makusudi kutesa wananchi, kuiba kahawa zao na kadhalika, wachukuliwe hatua, na kama itatokea basi changamoto itakuwa kubwa katika miaka inayokuja… *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba muda wangu ulindwe.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Anatropia, muda wako wa kuzungumza umekwisha. Naomba kutoa maelekezo ya Kiti.

Mheshimiwa Waziri muda wa mzungumzaji ulikuwa umekwisha. Mheshimiwa Anatropia utaandaa taarifa yako yenye vithibitisho na utawasilisha kwenye meza ya Mheshimiwa Spika.

Namkaribisha sasa Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi, atafuatiwa na Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga na baada ya hapo tutamkaribisha Mohammed Issa, na kama muda utaruhusu atazungumza pia Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi. Karibu Mheshimiwa Florence Samizi. *(Makofi)*

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naungana na wenzangu kwa kuanza kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anayoifanya katika nchi yetu. Sote ni mashahidi, katika Majimbo yetu pesa nyingi za miradi zimekuja. Kipekee katika Jimbo la Muhambwe shilingi bilioni 52 zilizoletwa na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, ndani ya miaka mitatu zimelichechemua Jimbo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi nzuri anayoifanya katika nchi hii. Nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu kwa kazi nzuri anayoifanya, tumemwona anavyokimbia kuhakikisha wananchi wetu wanapata umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri Jenista Mhagama na Mheshimiwa Deogratius Ndejembi, Naibu Mawaziri na Watendaji wote wa Wizara hii kwa hotuba nzuri waliyotuletea na kwa kazi nzuri wanayoifanya kuhakikisha kwamba uratibu wa kazi za Serikali unakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakupongeza wewe kwa kiti hicho ulichokalia, kwa kweli kinakutosha. Unatosha na chenji inabaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio makubwa tuliyokuwanayo katika majimbo yetu, bado ziko athari za mabadiliko ya tabianchi zinazoendelea katika majimbo yetu. Kipekee katika Jimbo la Muhambwe, madhara ya mvua yamesababisha uharibifu wa barabara nyingi, barabara zimekatika na hazipitiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Kichananga – Kigina - Magarama mto mkubwa umekatika. Wananchi wanapita kwa kulipa pesa, ambapo mtu mmoja shilingi 1,000/= na pikipiki shilingi 3,000/= huku magari hayapiti kabisa. Hii ni Kata ya Rugongwe ambayo katika Jimbo la Muhambwe ndiyo kata inayoongoza kwa uzalishaji wa vyakula. Kwa hiyo, unaweza ukaona ni madhara gani wakulima katika Kata hii ya Rugongwe wanayapata kwa sababu sasa mazao yao yanaharibika katika mashamba yao, lakini hawawezi kupeleka sokoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Kifura – Nyange hasa pale Mukabuye imekatika na wananchi hawawezi kupita kabisa kwa sababu mto umekatika na barabara imekatika. Barabara ya Kitahana – Nyange kupitia Mto Kahambwe nayo imekatika, wananchi wanapata shida sana. Barabara ya kutoka Kibondo – Nyaviumbu Mto Nyaviumbu umekatika, wananchi hawawezi kupita. Nimejaribu kusema kwa uchache barabara chache zilizokatika kwa sababu ya madhara ya mvua. Mbali na wakulima kupata shida, sasa imekuwa ni changamoto kusafirisha wajawazito, watoto kwenda shule ni changamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa nasi tulikuwa miongoni mwa wale waliondika maombi ya dharura. Ninavyosikia hapa, wenzangu wamepata fedha za dharura, wanasubiri wakandarasi, mimi nabaki nashangaa kwa sababu, sina hata shilingi moja. Pamoja na wananchi wangu kutaabika kwamba wanavuka mito kwa kutumia fedha, lakini sijapata fedha yoyote ya dharura katika Jimbo hili. Naomba jicho la huruma Serikali hii sikivu, Jimbo la Muhambwe tuko kisiwani kwa sababu ya barabara zilizokatika. Naomba tupatiwe fedha za kutengeneza hizi barabara ili wananchi wangu waweze kusafirisha mazao, kwenda hospitali na watoto waende mashuleni kwa sababu tuko kisiwani kutokana na mvua hizi zinazoendelea katika Jimbo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko ya tabianchi yameenda mbali zaidi, imesababisha tumepata madhara makubwa ya makorongo. Nikisema makorongo, unaweza ukafikiri ni jambo dogo, lakini makorongo ambayo yalikuwa ni mfereji mdogo, sasa yamepanuka sana kiasi kwamba yanaleta madhara makubwa. Makorongo haya yamefikia kiasi yanang’oa miti na hata nyumba. Lile korongo la Migombani pale limeng’oa nyumba ya mwalimu, nyumba ya vyumba vinne imeng’oka kwa sababu ya maji yanayopita kwenye korongo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna korongo la Mto Katunguru ambalo lina urefu wa zaidi ya mita 800 na upana wa zaidi ya mita kumi. Tuna Korongo la Kanyamahela, hili lina urefu wa zaidi ya mita 368 na upana wa mita nane. Tuna korongo la Kumwai ambalo lina urefu wa zaidi ya mita 418 na upana wa mita kumi. Tuna korongo la Twabagondozi ambalo lina urefu wa mita 246 na upana wa mita nne. Tuna korongo la Migombani la mita 625 na upana wa mita sita. Nimeyataja kwa uchache hayo yaliyoko Kibondo Mjini lakini hata Kata za Bitale na Kagezi zina makorongo. Kwa hiyo, madhara ya makorongo katika jimbo hili nayo yanaleta madhara makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, nyumba zinaondoka kwa sababu ya yale maji mengi yanayopita kwenye

makorongo, miti inang'oka, na sasa wananchi hawawezi kupita, na kwa upande mwingine inasababisha madhara ya utoro shuleni kuwa mkubwa kwa sababu hawezi kupita hata kama nyumba iko hapa na shule iko hapa, inabidi mtoto azunguke njia ndefu sana ili aende shule, matokeo yake mtoto haendi shule. Pia wagonjwa hawawezi kupita kwa sababu hakuna barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefanya ziara pale kwenye makorongo na *engineer* wa *TARURA,* lakini akaniambia haya ni makorongo, hii siyo barabara, mimi siwezi kutengeneza. Naiomba Serikali sikivu, kupitia vifungu vya majanga, haya makorongo nayo katika Jimbo la Muhambwe ni janga. Kupitia wadau tulipambana tukampata mdau wa maendeleo Ernesto akatusaidia kujenga korongo moja ambalo lilikuwa karibu na *club* ya akina mama kwa teknolojia ya *gabion*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii teknolojia wanaweka mawe na nyaya na wanapanda miti mle. Hata hivyo, ametengeneza daraja moja tu kwa hii teknolojia ya *gabion*. Halmashauri yetu kupitia mapato ya ndani haiwezi gharama za kutengeneza hayo makorongo. Naiomba Serikali sikivu, waje Muhambwe, kwani haya makorongo nikiyasema mtu hawezi kuelewa. Waje Muhambwe ili waone madhara tuliyoyapata kwa sababu ya mabadiliko ya tabianchi katika Jimbo letu la Muhambwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini kifanyike? Kwa sababu takwimu zinaonesha kuwa hekta 400,000 za miti zinaendelea kuteketea kila mwaka kwa sababu ya moto kichaa na kukata miti ovyo, pamoja na ukataji miti ambao unatumia vibali maalum, nadhani ni muda muafaka, turejee nyuma tuone zile sheria zilizopitishwa za kuvuna miti, kwamba je, ni kweli tunavuna na kupanda? Je, uvunaji miti unaenda sambamba na upandaji? Kama ingekuwa hivyo, madhara haya yasingekuwa hivi. Naiomba Serikali tuachane na habari ya kupanda miti kwa ajili ya kupiga picha na sasa tupande miti ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa sababu kwa kweli madhara ni makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kuishukuru Serikali kwa kazi nzuri ambayo inafanya Jimboni Muhambwe. Kipekee, tunashukuru kwa barabara ya lami kilometa 47 kutoka Kibondo – Mabamba. Barabara hii imeanza ujenzi na mkandarasi anaijenga kwa kasi. Kwa masikitiko makubwa, wananchi walioathirika na barabara ile bado hawajalipwa fidia. Kutokulipwa fidia kwa wale wananchi kumesababisha mkandarasi ambaye tayari alikuwa *site* ashindwe kuendelea na kazi. Wananchi wanadai shilingi bilioni 1.2. Kwa heshima na unyenyekevu naiomba Serikali sikivu iwalipe wananchi hawa ambao wameathirika na barabara hii ili kazi iendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Samizi. Namwita Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga, atafuatiwa na Mheshimiwa Mohammed Issa Khalifa.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naanza kwa kukupongeza wewe Mwenyekiti pamoja na Mheshimiwa Mwanyika kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi sana ndani ya Bunge hili kuwa Wenyeviti wetu, hongereni sana. Nampongeza Waziri Mkuu, Naibu Waziri Mkuu na Mawaziri, Mheshimiwa Jenista na sasa kaingia Mheshimiwa Deogratius na Naibu Mawaziri. Kwa kweli, tunawapongeza kwa kazi zenu nzuri, mnafanya vizuri sana katika kuitumikia nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza mchango wangu kwa kuijadili hotuba ya Waziri Mkuu kwenye eneo hili la kilimo. Sisi Mbinga Vijijini kama tunavyoitwa vijijini, ni wakulima. Tunalima vizuri kahawa, mahindi, maharage, ngano na mazao mengine. Katika kipindi hiki tunamshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa sababu mvua imenyesha vizuri, tumelima vizuri na mazao yameota vizuri. Pamoja na kwamba mvua imekuwa kubwa na uharibifu mwingine uliotokea kwenye miundombinu, lakini kwa upande huu wa mazao, tunamshukuru sana Mwenyezii Mungu kwa mvua hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru pia Serikali kwa mpango ule wa mbolea za ruzuku. Sisi wananchi wa Mbinga hatulimi bila mbolea. Mbolea ndiyo muafaka kabisa, ndiyo mwarobaini katika kilimo chetu. Tunaishukuru Serikali kwamba mpango huu umekuwa endelevu. Mwaka uliopita 2023 na mwaka huu 2024, tumepata mbolea za ruzuku bila usumbufu wowote. Sasa mazao yanaonekana mashambani, kiasi kwamba inasababisha hali ya hofu kwa wananchi. Kwenye zao hili la mahindi hapa karibuni pameibuka hofu kubwa sana kwa sababu mpaka leo ninavyoongea, bado wananchi wana mazao ya mahindi ya mwaka uliopita. Naongelea nini hapa? Kuna shida kubwa ya soko la mahindi ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahindi ya mwaka 2023 bado hayajaisha na sasa tunakaribia mavuno. Kwa namna ilivyo, tutakuwa na mavuno mengi sana katika Jimbo langu la Mbinga Vijijini na hata Mkoa wa Ruvuma kwa ujumla. Wananchi wamenituma, wanaishukuru Serikali kwa kutoa mbolea, lakini wanaitaka Serikali itafute soko hili la mahindi. Kwa namna ilivyo, kwa mazao yaliyopo mashambani mwaka huu, inawezekana tukawa na shida kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe unajua, wananchi wetu hawa wasipopata soko lenye uhakika wanaacha kulima. Wakiacha kulima, nchi yetu itapata shida, itaingia kwenye majanga ya njaa. Kwa hiyo, naiomba sana Wizara ya Kilimo, imefanya vizuri sana kwenye mambo haya ya *input,* sasa ifanye vizuri ili baada ya mazao haya tupate masoko. Ipo hofu kwa wakulima hawa kwamba tumefunga mipaka, lakini nina uhakika mipaka haijafungwa. Kwa hiyo, naomba Wizara hii ipite, iwahakikishie wakulima kwamba awamu hii mazao yao yatapata soko, kwani mazao ni mengi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine ambayo nataka kuizungumzia, ni eneo la ukubwa wa haya maeneo ya kiutawala. Maeneo haya tumezungumza hapa mara kadhaa kwamba yapo maeneo makubwa sana. Juzi wakati Mheshimiwa Kakunda anaongea Mheshimiwa Spika alisema, lakini yako maeneo pia

madogo sana. Sasa ombi langu hapa haraka haraka, haya maeneo makubwa tuyaangalie kwa jicho la kipekee. Haiwezekani Halmashauri ya Mbinga au Jimbo la Mbinga Vijijini lenye eneo kubwa sana, kata 29, tarafa tano, leo hii magari ya *ambulance* yako mawili tu. Hivi yatahudumia wapi? Yatatoa huduma gani? Lazima tuangalie namna tunavyopeleka hizi huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeelewa kwamba sasa hivi Serikali inaboresha miundombinu kwenye maeneo haya, kwa hiyo, haipendi sana kuelekea kwenye kugawa, lakini sasa tutoe kipaumbele. Tupeleke hizi huduma kwa namna ya ukubwa wa yale maeneo, ikibidi hata mishahara mimi mwenye Jimbo kubwa, basi nipate mshahara mkubwa ili niweze kufika haraka kwenye huduma hizo kuwahudumia hao wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa ushauri tu, ikibidi kwenye kupeleka hivi vituo vya afya, basi maeneo haya yenye ukubwa yasiende jumla jumla. Hata kwenye ule Mfuko wa Jimbo najua kigezo kinakuwa labda idadi ya watu, lakini twende mbele zaidi, tuangalie siyo kwa idadi ya watu tu, bali hata ukubwa wa maeneo haya kiwe kigezo. Kwa sababu mwenzako atatumia tenki moja kuifikia jamii lakini wewe ili umalize Jimbo unatumia tenki kumi. Kwanini usipewe kipaumbele wewe kuongezewa hata mshahara, kuongezewa huo mfuko wa Jimbo, kuongezewa *Jimbo Allowance,* ili ufanye kazi hizi na wananchi hawa wafurahie? Watu hawa sehemu nyingine unaona wanasema mtu huyu haonekani, haonekani, ni kwa sababu kuwafikia inakuwa ngumu. Ukiongeza huu mshahara, ukaongeza na *Jimbo Allowance,* huyu mtu atafika kirahisi sana na wananchi wataona Serikali inafanya kazi vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nataka kulisema haraka haraka ni hili eneo la kikokotoo…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba dakika moja tu nimalizie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikokotoo kimezungumzwa vizuri sana na Mheshimiwa Gambo na hapa ndani tuliaminishwa kwamba *formula* hii mpya itawanufaisha hawa watakaopata kikokotoo hiki kipya…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Benaya naomba hitimisha tafadhali, hatuna muda.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nahitimisha. Hapa nina mifano ya watu wa *level* moja, aliye…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Benaya naomba tafadhali hitimisha hoja yako.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, nitaizungumza wakati mwingine. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Benaya. Kwa maslahi ya muda, tutakuwa na mchangiaji mmoja tu ambaye ni Mheshimiwa Mohammed Issa, ndiye atakayekuwa mchangiaji wetu wa mwisho. Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi atakuwa mchangiaji wetu wa kwanza kesho asubuhi.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa kibali cha kuweza kusimama katika Bunge lako hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kupeleka salamu za shukurani kutoka kwa wananchi wa Jimbo la Konde kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Katika Jimbo la Konde, vikosi vya KMKM Askari wake walipoteza silaha. Kadhia iliyowakuta wananchi wa Jimbo la Konde ni kukamatwa, kupigwa na kuzuiwa kufanya

shughuli zao za kijamii ikiwemo kuvua na kulima. Namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais, Mheshimiwa Hemed Abdalla Suleiman na Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba kwa jinsi walivyolishughulikia suala hili likaweza kutulia kwa vile suala hili la kupotea silaha siyo suala ambalo lilikwenda kwa wananchi. Nawashukuru sana na salamu ziwafikie Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza kuchangia, kwanza ni kuhusu upatikanaji wa fedha za kigeni. Fedha za kigeni imekuwa ni suala gumu sana katika nchi hii kupatikana. Kwa kweli suala hili napenda linapokuja kuhitimishwa hapa tupate maelezo ya kina kwamba fedha za kigeni zinapatikana vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda benki unataka dola 1,000 hakuna, ukitaka dola 500 hakuna. Tunajiuliza, biashara zinafanyika lakini benki hakuna. Hii inaonesha kwamba kuna udalali wa fedha za kigeni. Kwa hiyo, hapa tunataka kujua kwamba je, ni *BoT* wanaofanya udalali huu au ni benki? Kwa sasabu biashara zinaendelea kama kawaida, lakini fedha za kigeni hazipatikani. Tunataka Serikali ituambie, je, fedha hizi za kigeni zinapatikana kwa njia gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Zanzibar sasa hivi biashara imedumaa, lakini wenzetu huku Tanzania Bara makontena yanashuka kama kawaida. Hatuelewi ni lipi hapa liko nyuma ya pazia? Tunataka maelezo ya kina kuhusu upatikanaji wa fedha za kigeni. Ni nani dalali wa fedha hizi? La kwanza hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, napenda kuchangia suala la upungufu wa sukari. Upungufu wa sukari umekuwa ni jambo ambalo limetikisa nchi mpaka imeonekana Mheshimiwa Rais hafai, kumbe Mheshimiwa Rais anafanya kazi nzuri tu. Mheshimiwa Rais anafanya kazi nzuri ya kujenga nchi, kuwatumikia wananchi na kwa kweli anahitaji kupongezwa. Sasa jambo hili kwa kweli limeleta taswira mbaya katika nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaambia wahusika hawa wafanyabiashara wa sukari wame-*switch* tu tukifika 2025, hapo ndipo mtajua wamejipanga vipi. Nashauri sheria ya kuwapa vibali wenye viwanda ifutwe na iletwe sheria nyingine ambayo itaruhusu wafanyabiashara wote wenye uwezo waweze kuleta ama sivyo, hawa wafanyabiashara wenye viwanda wametengeneza *syndicate* ambapo wanaamua tu kulangua sukari. Kuna baadhi ya maeneo sukari ilifika shilingi 6,000 kwa kilo na wengine wameshindwa kupata sukari. Kwa hiyo, nashauri sheria hii haifai, irudishwe hapa Bungeni tuichakate ili mwenye uwezo yeyote aweze kuleta sukari kuondokana na tatizo hili ambalo limejitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni Bwawa la Mwalimu Nyerere; Bwawa la Mwalimu Nyerere limetengeneza *disaster* kule Rufiji. Mimi na-*declare interest*…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, naomba nikukatishe kidogo hotuba yako. Nampisha Mheshimiwa Spika, halafu utahitimisha wakati Mheshimiwa Spika akiwa Mezani.

*Hapa Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alikalia kiti*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mbunge aliyekuwa anachangia atatunziwa muda wake, atapata nafasi ya kuchangia siku ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu atahitimisha hoja yake.

Waheshimiwa Wabunge, nimekuja kwenu na Taarifa ya Spika.

## TAARIFA YA SPIKA

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni yetu ya 39(2) ya Kanuni zetu za Bunge, nasikitika kuwatangazia kifo cha Mheshimiwa Ahmed Yahya Abdulwakil, Mbunge wa Jimbo la Kwahani, kilichotokea leo tarehe 8 Aprili, 2024 huko Zanzibar. Mheshimiwa Ahmed Abdulwakil amefariki ghafla kwa shinikizo la damu. Mazishi ya Marehemu yanatarajiwa kufanyika kesho tarehe 9 Aprili, 2024 kijijini kwao Buyuni, Zanzibar.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni yetu ya 173 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, kesho hakutakuwa na Kikao cha Bunge ili kutoa fursa kwa Waheshimiwa Wabunge kushiriki msiba huu mzito. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya Marehemu mahali pema Peponi, Amina.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu kesho hatutapata nafasi ya kurejea hapa, basi kabla hatujaahirisha shughuli zetu za Bunge, kwa mujibu wa Kanuni zetu, tusimame kwa ajili ya kumkumbuka mwenzetu na kumpa heshima yake.

*(Hapa Wabunge walisimama kwa muda mfupi kumkumbuka Mheshimiwa Ahmed Yahya Abdulwakil)*

**SPIKA:** Mungu ailaze roho ya Marehemu mahali pema Peponi, Amina.

Waheshimiwa Wabunge, mkiwa mmesimama, kwa kuwa tulikuwa ndani ya wiki hii tunatarajia mwandamo wa Mwezi Mtukufu, na kwa kuwa, kesho hatutapata nafasi ya kuonana na kufahamu mwongozo wa BAKWATA utakuwa namna gani, kwa sasabu tunavyofahamu kwa Kanuni zetu za Bunge, hatuwezi kuahirisha Bunge bila kusema ni lini tunakutana; na kwa kuwa, hatuna hakika nini kinaweza kutokea wakati gani au mwandamo wa mwezi utakuwa lini, basi naahirisha shughuli za Bunge mpaka Jumatatu 3.00 asubuhi.

*(Saa 12.08 Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 15 Aprili, 2024 Saa Tatu Asubuhi)*